PL
8704
M49855
S23
2009

SAA YA UKOMBOZI

Nkwazi Nkuzi Mhango

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA

ITHIBATI
LUGHA IMETHIBITISHWA NA
BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA
CHETI NA. 09/174
TAREHE 27/10/09
BAKITA

Baraza la Kiswahili la Taifa
BAKITA

Na. 09/174

Cheti Cha Ithibati

Jina la Kitabu SAA YA UKOMBOZI

Jina la Mwandishi NKWAZI NKUZI MHANGO

Mchapishaji TANZANIA EDUCATIONAL PUBLISHERS LTD.

ISBN 978 9987 97 039 8

Kiswahili kilichotumika katika kitabu hiki kimethibitishwa kuwa ni Kiswahili sanifu

Mratibu wa Ithibati

Katibu Mtendaji
Bakita

12,000/=

SAA YA UKOMBOZI

Nkwazi Nkuzi Mhango

TANZANIA EDUCATIONAL PUBLISHERS LTD

Tanzania Educational Publishers Ltd,
TEPU House,
Barabara ya Uganda,
Kiwanja Na. 45, Kitalu MDA,
Simu: 028-2220833, Faksi: 028-2220833,
Baruapepe: tepultd@yahoo.com
S.L.P. 1222,
Bukoba, Tanzania.

© Nkwazi Nkuzi Mhango, 2009
Toleo la kwanza 2009

Mchoro wa Jalada: Idd Marumba

ISBN 978 9987 07 039 8

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kutafsiri, kupiga chapa, kunakili au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi nyingine yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Tanzania Educational Publishers Ltd.

TABARUKU

Kwa mke wangu kipenzi Nesaa, siku zote umekuwa faraja na mwanga katika maisha yangu. Kwa wanangu Kanthethe, Ndidziwa, Nthelez na Ng'ani na watakaofuata. Yote ni kwa ajili yenu. Tunaanza; nyinyi lazima mmalizie kazi hii ya kuusaka na kuupata ukombozi kamili na wa kweli Saa ya UKOMBOZI ni sasa.

SHUKURANI

Daima nitamshukuru Mungu aliyeniwezesha kufanya kazi hii adhimu. Pia, ninamshukuru mke wangu Nesaa ambaye si rahisi kueleza uzito na thamani ya msaada wake. Kwani alikuwa mhakiki, mshauri na mhariri wa awali aliyesikiliza kila mawazo na kuyapa kibali ua kuyapinga ukiachia mbali usumbufu wa kukurupuka ima mezani au kitandani kwenda kuandika jambo. Pia, nawashukuru watoto wangu, Kanthethe, Ndidziwa, Nthelezi na Ng'ani kwani katika maisha yangu yote ya uandishi, wao wamechangia kwa kunikosa. Wakati naandika, huwa mkali na mwenye kuhitaji upweke ili nifikiri. Wao, kwa bahati nzuri, waliishaizoea hali hii. Hivyo, kwa dhati kabisa, sina jinsi ya kuwashukuru kwa kuelewa maana ya kila nililolifanya na kuliwaza.

Shukurani pia ziende kwa wote ambao kwa njia moja au nyingine walinifundisha tabia ya kuwasemea wengine hasa wanyonge. Hawa walinifundisha utu. Na si rahisi kuwataja wote kwa majina. Walinifundisha kuwa mtu bila utu ni mnyama hata kama amesoma au ana mali na madaraka. Walinifundisha jinsi ya kuishi.

Shukurani zangu haziwezi kukamilika bila kuwashukuru, John Njema Ndamu (Mwenyekiti) na familia yake wa Valley Arcade Lavington, Nairobi na Nyeri, Kenya kwa mchango wake wa hali na mali.

Nilianza kutunga kitabu hiki mwaka 2003, mtaani Valley Arcade Lavington, Nairobi baada ya kushuhudia masaibu na mikiki ya viongozi wa SPLA ya Sudan ya Kusini wakipigania uhuru wa kweli kutoka kwa serikali iliyojiita huru lakini yenye kuwabagua na kuwakandamiza. Kiongozi wao, marehemu John Garang de Mabior, alikuwa jirani yangu. Adha na kadhia yao ilinizindua na kunipa muono mpya wa uhuru na kuuchukia uhuru wa bandia, ubadhirifu na ukandamizaji ukiachia mbali ubaguzi, udini na tabaka. Nani alijua nchini Sudan bado ina watumwa na wendawazimu weusi wanaojiita Waarabu wakati ukweli ni kwamba Sudan haina Waarabu bali Waafrika?

Ndamu alinifundisha kuwasiliana na ninaowatetea. Nilitaka kuandika kwa Kiingereza hata Kifaransa. Bila ya kuogopa kuingilia mapenzi yangu hata

kuniudhi, aliniambia kavukavu, "Utawezaje kuwasiliana na unaowatetea bila kutumia lugha yao wanayoielewa,wala kufanana nao." Kuanzia hapo nilijisikia fahari kuandika kwa Kiswahili na kukitetea kama lugha ya Kiafrika. Kutumia lugha ya kukopa kungenitenga na kuwatenga wahusika wakuu ambao ni wale wote wanaojihisi kuwa hawajaonja matunda ya uhuru ambao kwao ni udhuru. Uhuru si bendera na kutangaza kuwa huru. Uhuru haukamiliki bila msukuma mkokoteni na mkulima, mchungaji anayekula mazao hafifu huku akiuza mazao yake bora. Uhuru hauanzii kwa Rais. Unaanzia kwa maskini mtaani na kijijini, ombaomba na wengine kama hao maishani. Si yule anayevaa suti na kupewa asilimia kumi. Hapana. Ombaomba wa kutengenezwa na ombaomba wa wakubwa wa kimataifa. Uhuru si wachache kuwatumia wengi bali kuwatumikia. Uhuru ni heshima na kuongezeka thamani ya mtu bila kutegemea alichonacho kichwani au mfukoni. Uhuru ni kuwajibika, kukosolewa hata kama wewe ni mkubwa. Uhuru si maneno ni matendo. Kwa hakika uhuru ni usawa wa binadamu waliojitenga na kuchukia matabaka ya wenye nacho na wasio nacho.

Shukurani haziwezi kukamilika na utakuwa wizi wa fadhila bila kumshukuru Ndugu Pius B. Ngeze. Namshukuru kwa ushauri na imani yake kwangu. Nakumbuka nilivyokuwa nikimsumbua kwa simu wakati akiwa mikutanoni au amelala akizijibu bila kinyongo.

Shukurani zangu pia ziende kwa Zuhura Machungi (shangazi), Saleh Sharriff as-Saggaf na Maria na Attilio Tagalile mlinipa kila msaada na kila aina ya hamasa kutoa kazi hii.

Dkt. Willy Mutunga na Prof. Makau Mutua wa Kenya Human Rights Commission nao walinipa ushirikiano nilipokuwa nikiishi Kenya. Pia, nawashukuru Kituo cha Haki za Binadamu cha Dar es Salaam (LHRC). Kwani katika kufanya kazi ya kutafiti haki za binadamu kwenye makambi ya wakimbizi ya Mtabira, Mkubwa na Muyovozi, kutaja kwa uchache, niligundua jinsi ufisadi unavyopofua watu bila kujali mipaka. Wengine ambao siwezi kusahau michango yao ni Soshana Wingate, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi cha Writers' Association of New Foundland and Labrador (WANL) St. John's, NL, Kanada, ambacho mimi ni mwanachama, aliyenipokea. Hakika nilipata uzoefu na ujuzi wa ziada kuliko ule niliokuwa nimetoka nao Afrika. Donna L. Jeffry (Mama D) wa

RIAC, Newfoundland and Labrador aliyenitambulisha kwa vyombo vya habari vya Kanada na kunipa uzoefu wa haki za binadamu kwa upande wa Amerika ya Kaskazini. Kabla ya kuwa na maktaba yangu mwenyewe aliniruhusu kutumia maktaba yake bila kinyongo huku akiniulizia maendeleo ya kitabu changu.

Mwisho, namshukuru pacha wangu tuliyeunganika naye, Mpayukaji Msemahovyo. Ni nani na amefanya nini msiniulize bali mtafuteni mmjueni.

Mwalimu Nkwazi N. Mhango
S.L.P. 2374,
Altona MB
ROG OBO
Kanada
Simu: 1204 216 0262
Baruapepe: nkwazigatsha@yahoo.com
10 Julai, 2009

Faslu ya Saa ya Ukombozi

Kabla na baada ya nchi nyingi za Kiafrika kupata uhuru wa bendera, riwaya na tamthiliya nyingi zilizotungwa na Waafrika zilijikita katika kumkomboa mtu kisiasa na kidogo kiuchumi.

Sasa Afrika inao uhuru wa bendera kwa miongo zaidi ya minne. Je, wananchi wetu wameufaidi huu uhuru au wameishia kuusikia majukwani midomoni mwa wachache na kuwa watumwa wa kizazi kipya cha wakoloni weusi? Hili ndilo swali lililolengwa na riwaya ya Saa ya Ukombozi; ukombozi wa kweli wenye kuwafanya watu wote kuwa huru kwelikweli.

Riwaya inaudurusu na kuzulu uhuru na dhima nzima ya kuwa huru. Inaona shaka na uhuru wa baadhi ya nchi barani Afrika unaowanufaisha watawala waliojigeuza miungu pwamwe na walamba viatu wao. Watu wa kawaida hawaruhusiwi kutia mkono kwenye deste nao wale halua!

Riwaya hii inaualika umma kushika hatamu. inashadidisha utathimini na kuuhoji upya uhuru wanaoambiwa ni wake si wake. Katika kufanikisha hili, tofauti waathirika waishio kwa matumaini kuupigania na kuupata uhuru wa kweli kupitia kwenye sanduku la kura.

Hapa muhimu ni ithibati na dhamiri ya kweli kuelekea lengo zima la ukombozi wa kweli kama tutakavyoona kwa wahusika wa riwaya hii.

Hivyo ni jukumu la jamii kukubaliana na kulibeba jukumu hili mintarafu ya hali iliyozoeleka ambapo wanasiasa tu ndio wameachiwa kila kitu kuhusiana na ukombozi. Kwa vile baadhi yao wameshindwa, basi umma uzibe ombwe kwa kulibeba na kulitekeleza jukumu hili adhimu.

Riwaya inahimiza watawaliwa kuhakikisha wanawajibisha watawala kama sehemu ya uwajibikaji wao. Kila mmoja awajibike kwa mwenzake. Inawataka watawala wawatumikie watawaliwa badala ya kuwatumia kama punda wa kuwabeba wao na mizigo yao.

Riwaya inapinga ufisi, ukuku, umbwa, ukondoo, usindano, ukijiko na tabia nyingine kama hizo; inashajihisha usimba, umizani na utambuzi, utendaji na ulinzi wa haki.

Hapa ndipo utamwona mhusika mkuu mzee Njema akipambana na

uongozi mbovu kuanzia kijijini mwake hadi wilaya na, hatimaye, taifa. Cheche ya shujaa inawasha moto unaouamsha na kuukengeua umma kiasi cha kuangusha serikali dhalimu ya Mizengwe kupitia sanduku la kura.

Jamii imekuwa ikilalamika bila kuchukua hatua madhubuti na mujarabu kwa wakati wala kufuruka! Riwaya ya "Saa ya Ukombozi" inalenga kuwaamsha na kuwakumbusha na kuwahamasisha wanajamii kuwa jukumu la kujikomboa halina mjadala wala mipaka hadi haki itakapopatikana kwa gharama yoyote na mahali popote wakati wote. Ni swali wanalolazimika kulifuta kwa wakati na ukamilifu hadi dahari.

Riwaya, licha ya kuwatia shime wanyonge watawaliwa, inawapa changamoto. Inalenga kuamsha ari na mori wa kujiletea ukombozi wa kweli. Wakijitambua na kuamua kwa dhati, kila kitu kinawezekana. Hivyo, riwaya hii ni waraka wa wazi kwa wanyonge popote walipo duniani bila kujali mpaka.

Wanakijiji wa Kithakwa wamejikusuru ili kujinusuru na kushinda hila na njama za wezi wachache wenye madaraka kutaka kubinafsisha kijiji chao kwa tajiri wa kizungu, Bwana Sucker.

Hata baada ya mzee Njema kuleta ukombozi kwa kuondoa serikali kidhabu, hajiungi na serikali mpya; wala hataki kulipwa fadhila wala kuusaliti ukombozi. Kwa sababu ukombozi ni jukumu la kila mwnajamii. Anakaa nje ili awapime na kuwapa changamoto viongozi wapya inapolazimu. Kama nao watalewa madaraka, mzee Njema anadhamiria kurejea kwenye medani ili, ama kuwatia adabu au kuwakumbusha kilichowapata watangulizi wao.

Hakika riwaya hii inafungua ukurasa mpya ambapo kwa mara ya kwanza, wanakijiji wanatoa somo adimu na adhimu kwa nchi. Je, katika Afrika ya sasa kuna Mizengwe na akina Njema wangapi. Wako wangpi walioko tayari kuleta ukombozi wa kweli kama Njema ambaye kwao ni nyota njema?

Ukombozi ni lazima na **Saa ya Ukombozi** ni Sasa.

Utangulizi

Nchi ya Mizengwe ni nchi ya kufikirika. Ni nchi inayoelea kwenye fikira za msomaji lakini inayoonekana kwenye maisha yake kila siku kila mahali. Inavyo vifani vyake ima kwa wanajamii au hata jamii nzima katika ujumla wake. Ni dhana sawa na nchi yoyote Duniani. Kwani nchi huwa ni mkusanyiko wa watu wenye mamlaka moja kisiasa, kijiografia, kimkakati, kimalengo na hata wakati mwingine kiutamaduni n.k. Hivyo, kama itafanana na kuwa na nchi yoyote duniani itakuwa ni bahati mbaya.

Wananchi ni watu wanaosema kuwa wao ni taifa na kitu kimoja ingawaje hutokea wachache wakasema hivyo na kutenda tofauti. Hapa ndipo dhana nzima ya Ukombozi inapochimbuka, kujichimbia, kuibuka na kusambaa kwenye mishipa yote ya jamii hiyo. Kitu kimoja hapa ni muhimu. Mabadiliko ni kama maji, huwa hayazuiliki na yakitokea huwa hayachagui wakati au eneo la kusambaa na kuteka kama ilivyotokea kwa nchi ya Mizengwe kuanzia Kijiji cha Githakwa.

Wananchi wa Mizengwe ni watu wa kufikirika tena Waafrika ambao kwao uhuru bado haujatimia. Ni Waafrika kwa vile mtunzi wa riwaya hii ni Mwafrika kama wao. Uhuru wao utatimiaje iwapo bado kuna watu wanakandamizwa?

Utatimiaje iwapo bado kuna watu wanawanyonya watu. Je, haya hayapo? Japo hili ni swali gumu lazima lijibiwe na wote wanaosoma riwaya hii ili kujiepusha na zahama iliyokuwa imeikumba Mizengwe kabla ya Ukombozi. Jambo moja ni dhahiri: twaweza kujifunza kujikomboa baada ya kusoma riwaya hii. Na hakika hii ndiyo dhima ya riwaya nzima.

Wapo waliokufa wakiwa chini ya ukoloni na kusahaulika. Wapo waliokufa wakipambana na ukoloni. Hawa ni Mashujaa sawa na mzee Njema na wenzake.

Je, Historia inawahukumu vipi na kuwakumbuka au kuwasahau vipi?

Japo waathirika wa Mizengwe hawakufa kutokana na matundu ya risasi za

bunduki. Waliuawa na risasi za ubadhilifu na tamaa ya ndugu zao wachache walioabudia umimi na kuuza usisi. Walishika changu badala ya chetu.

Waliuawa na wakoloni wa kuzaliwa nao ambao wameitumia bendera ya uhuru kama mwamvuli wa kujitajirisha huku maskini wakiongezeka na madhila yao kuongezeka. Hawa ni watu waliouhitaji ukombozi ambao waliuleta kwa kuwa na miili midogo iliyobeba mioyo mikubwa.

Bila uhuru wa mzibua mitaro, mkulima, kuli, ombaomba asiyeomba chini ya bendera akiwa amevaa suti ya bei mbaya,mchungaji wa mifugo auzaye mazao yake bora na kula hafifu na wengine dhalili, uhuru wa jamii yoyote hauna maana. Maana ya uhuru si kuwa na bendera wala neno taifa bali mahitaji ya jamii. Uhuru ni kujenga utu si vitu. Uhuru ni ukombozi wa wengi wanyonge dhidi ya wachache wenye kula na kusaza. Uhuru ni utumishi wa umma. Uhuru ni haki si mizengwe na kuzidiana akili. Na uhuru ni kwa wote na si kwa kikundi kidogo cha watu. Uhuru ni maendeleo na si ahadi za maendeleo. Uhuru ni usawa katika jamii na si mjenzi wa matabaka uchwara na ovyo ya walio nacho na wasio nacho. Uhuru ni kukamilika kwa heshima na masilahi ya umma kwa ujumla wake.

Watu hufikia kiwango cha hupinga hata kuasi mfumo unaowakandamiza kwa makusudi hata bahati mbaya. Lakini siku zote uasi huu huzaa msuguano ambao nao huleta mkakati, mchakato hata harakati za ukombozi kutoka kwenye kongwa, mikatale na dimbwi la kuachwa nyuma kwenye kuyakimbilia na kuyaelekea maendeleo na mafanikio kama ndoto waliyotarajia na kuidhamiria ama kama taifa au mtu binafsi. Hivyo ukombozi unaolengwa hapa ni wa kukomboa matabaka mawili ya watu: wanyonyaji na wanyonywaji. Maana wote wanauhitaji ukoimbozi kwa haraka sana. Kwani wote katika kifungo chao wanaishi maisha yasiyo huru wala kukombolewa. Dhana nzima ni kuleta suluhisho baina ya mahasimu ili kuaminiana na kusaidiana kujenga jamii. Maana dunia wanayoishi ni moja sawa na meli moja yenye roshani mbili tofauti lakini zenye kuwa sawa juu ya sakafu moja. Huwezi kunyonya au kunyonywa ukawa mtu huru. Kwani kupe na ng'ombe wote ni watumwa. Kupe hata anenepe vipi bado ni kupe. Hivyo ukupe,ufisi,ukondoo na upanya ni mifumo inayowafaa hayawani lakini si binadamu.

Fisi, panya hata hayawani wengine hufanya uhayawani kutokana na sababu kuu mbili: ya kwanza ni kutojaliwa akili ya kupanga na kuchanganua mambo na ya pili ni kutojaliwa kumilki mali yoyote zaidi ya kumilkiwa. Mtu au jamii inapofika au kufikishwa hapa lazima ipambane kujikomboa kufa na kupona. Ni kwa njia ya ukombozi tu jamii hii inaweza kuitwa jamii ya watu, si hayawani. Mizengwe ni taifa tofauti kidogo. Japo ni taifa linaloelea kwenye fikira za Mwandishi likiwa ni somo na funzo kwa mataifa yote duniani yanayofanana nalo, ama kwa makusudi au bahati mbaya, bado ni taifa sawa na mataifa mengine.

Ni matokeo ya msuguano wa kijamii uliomo kwenye mkururo mzima wa maisha ya binadamu mmojammoja na kundi.

Kwa hakika, yapo mataifa mengi Duniani hasa yanayoendelea yenye sifa, tabia, hulka, historia, jiografia, ikolojioa, mbinu raia na hali kama Mizengwe.

Mizengwe ina tabia kuu tatu zinazoweza kufananishwa na nchi yoyote, nazo ni matatizo, mafanikio yake na hamu ya kujikomboa kutoka mikononi mwa adha zote zinazoikabili nchi hii.

Tofauti na nchi nyingine iwayo, wananchi wa Mizengwe hasa wanakijiji,wanafanikiwa kuudekua mfumo wa kinyonyaji na wa ukandamizaji uliokuwa ukiwadhalilisha na kuwadhulumu.

Ukiachia mapinduzi ya wafanyakazi nchini Ufaransa, kwa Afrika wanakijiji wa Githakwa wakiongozwa na mzee Njema na wenzake, wanafungua ukurasa mpya kwa kuanzisha na kufanikisha mapambano ya ukombozi kutokea kijijini kwenda mijini na kutoka kwenye mapambano ya bunduki kwenda kwenye sanduku la kura. Pamoja na kwamba wanakijiji walikuwa na uwezo wa kutumia silaha zao kama mapanga, mikuki hata mawe, hawakufanya hivyo. Kwani siyo jibu wala njia ya kistaarabu ya kujikomboa.

Ijapokuwa ukombozi wa taifa la Mizengwe umevunja mwiko kwa

kuanzia kijiji kidogo cha Githakwa, bado hii si kikwako cha mapinduzi na ukombozi kuanzia mijini kwenda vijijini au vijijini kwenda mijini na hata kuanzia kotekote. Maana ukandamizaji na unyonyaji viko kotekote mijini na vijijini.

Hivyo basi, licha ya kuleta somo la Ukombozi uliojikita kuondoa dhuluma bila umwagaji damu bali ithibati na ujasiri, riwaya hii inaleta somo jipya kuwa kila Mwananchi awe mdogo au mkubwa, maskini au tajiri, akijikomboa kifikra, anaweza kuwakomboa na wengine waliotosheka na mifumo ya ukandamizaji. Ni suala la kufanya mapinduzi ya kifikira na kukubali hali halisi kuwa kujikomboa ni jukumu la kila mmoja awe mnyonyaji au mnyonywaji. Wote wanahitaji Ukombozi ili kuleta maana halisi ya maisha yao.

Pia, ni mbiu ya mgambo na hadhari kwa wote wanaofanana na wananchi wa Mizengwe kutoyapa kisogo matatizo yanayowazunguka, bali kuyakabili bila kuleta vurugu. Na zaidi ya hayo, somo kuu ni kwa wananchi kutopoteza
kumbukumbu ya yanayowatokea.

Na badala yake ni kuitumia kura yao kama ngao na silaha bora na salama yenye matokeo ya uhakika kama ilivyotokea kwa wananchi wa Mizengwe.

Yote yaliyomo kwenye kitabu hiki ni ya kubuni na hayamlengi mtu mmoja au nchi binafsi. Badala yake yanalenga kuzindua wahusika kuutambua utu na heshima ya binadamu. Kwani binadamu wote ni sawa na wenye silika, tabia, mahitaji na matarajio sawa bila kujali mipaka yao ya kutengenezwa na binadamu wenzao ama kwa nia nzuri au mbaya.

Mwisho wa yote, **Saa ya Ukombozi** ni wito kwa watu, jamii na mataifa yote yanayoendelea kuumia chini ya aina yoyote ya ukoloni, udhalimu, unyonyaji na mengine kama hayo kusimama kidete kuitetea haki.

1

"Matatizo, Mafanikio, amekusalimia." Huzuni, mama yake Matatizo, anamfikishia salamu mwanawe alizozipata kutoka kwa jirani yake Joy, mke wa mzee tajiri, Livingstone Kupata, aliyekuwa ametoka kuongea kwa simu na mwanaye.

Hii ni baada ya Matatizo kutokeza akiwa njiani kuelekea kwake akitokea kwenye mihangaiko yake ya maisha. Mama yake amekaa nje ya banda la makuti akionyesha dhahiri kuzeeka na kudhoofu. Amezungukwa na alama zote za umaskini na masaibu yanayotokana nao.

Yuko chini ya kivuli cha mwembe, akichambuachambua mboga za majani kwa ajili ya kitoweo cha mchana. Mwembe huu ulikuwa kivutio kikubwa kwa akina Matatizo na Mafanikio walipokuwa wadogo. Walizoea kuja kuchuma maembe na kubembea, hata kujificha wakati mwingine.

Siku moja Mzee Shida, baba yake Matatizo, aliwafuma na kuwatandika bakora si kawaida. Wakati ule kila mzazi alikuwa mzazi wa kila mtoto bila kujali kama ni wake wa kuzaa au vipi. Walikuwa wametoroka shule kuja kucheza na kuchuma maembe. Hivyo, kila Matatizo akiuona mwembe huu huwa ni kama anasoma historia ya maisha yake. Kwake, mwembe huu ni kama kitabu cha historia.

Matatizo anakaa pembeni ya mama yake huku akiwa na shauku ya kusikia kulikoni kwenye salamu kutoka kwa rafiki na jirani yake wa utotoni anayeishi naye Kanada.

Wamekaa chini ya mwembe ambao ndiyo ulikuwa kama nyumba ya Matatizo na Mafanikio. Hivyo, salamu hizi si zake peke yake bali hata mwembe ambao ulikuwa ukiwapa hifadhi na matunda utotoni. Anawaza moyoni na kuvutwa na fikira kama anaongea na mwembe ule kuushukuru

kwa ukarimu wake.

Pembeni mwao kuna kuku na vifaranga vyake. Kuku huyo anacharukacharuka, kama kawaida, kuwalisha vifaranga vyake. Japo ni hayawani, anajitegemea. Isitoshe vifaranga vina raha kuliko hata huyo aliyevifuga.

Kifaranga kimoja kinakuja karibu na alipo mama yake Matatizo. Anakifukuza na kujisemea, "Nenda kwa mama yako. Hapa sina mahindi ya kukupa nenda ule wadudu." Anafukuza kifaranga na kukisindikiza na maneno. Anasema, "Wadudu nyie hamna shukurani. Kwanza waangalie walivyotakata, utadhani matajiri. Ama kweli wa kututenda wametutenda. Kwani tunazidiwa na nyuni." Anatikisa kichwa na kutema mate pembeni na kuendelea na udonozi wake. Kifaranga utadhani kimeelewa. Kinatimka ki- malaika hata kama ni hayawani.

Kifaranga kinaondoka haraka, kinatimka mbio kuelekea alipo mama yake na wenzake wakiendelea na zoezi la kucharukacharuka. Hayo ndiyo majaliwa yao kama hayawani wengine.

Ghafla Matatizo anaamka na kuokota jiwe ili kumfukuza mwewe aliyekuwa jirani akiwinda mawindo yake. Amemwona mwewe akipitapita akiwa naye kwenye mawindo yake. Ndiyo maisha.

Anajisemea, "Juzi vifaranga vyangu sita vililiwa na mwewe." Anatupa jiwe kuelekea aliko mwewe na kurejea akisema, "Inaonekana ni huyuhuyu. Maana naona ana kichwa chenye ubapa kama yule aliyekula vifaranga vyangu. Ndege kajaliwa tamaa! Ole wako siku nikikunasa ama zako au zangu, nyuni we usiye na adabu."

Watu wa Mizengwe wana namna ya kujiliwaza. Wanapoudhika humalizia hasira zao kwa miti hata wanyama. Wakati mwingine huitumia sanaa ya kuongea na vitu kuwafikishia walengwa ujumbe. Analazimika na kurudi kujiunga na mama yake.

Akiwa anaendelea na zoezi la kumfukuza mwewe mama yake naye anatoa kilio chake, "Wewe unalalamikia vifaranga! Hukusikia kuwa juzi mbwamwitu wamevamia mbuzi wa Mipawa. Sijui balaa gani limetuvamia.

Maana huku mwewe. Kule mbwamwitu, ukame na serikali ndiyo usiseme. Yaani, kila balaa linakuja kwetu. Mungu tusaidie."

Matatizo anajibu huku akitupa jiwe la mwisho, "Mama, hapa hakuna balaa wala nini. Tatizo ni kwamba tumeharibu mazingira. Wale mbwamwitu walizoea kuua mbarapi, swala na digidigi. Lakini, baada ya kufyeka miti yote na kuyaacha uchi makazi yao wakajikuta hawana chakula, nao wameamua waje kwenye makazi yetu, maana tumeharibu makazi yao. Yaani, wanyama wana hiana, sina hamu, maana walichinja mbuzi utadhani walifuga wao!"

Anainama na kuokota jiwe jingine na kutupa na kusema,"Mama bado una ndoto za serikali! Hujui wakubwa wa serikali hiyohiyo ndio wanatoa vibali vya kufyeka misitu ovyoovyo halafu wanakuja na unafiki wao kufanya kampeni ya kutunza mazingira! Nchi hii, we acha tu. Mtu anasema hili kumbe anamaanisha lile. Wametugeuza mashamba yao na vinyama vya kufanyia majaribio ya ujinga na tamaa zao."

Anarejea na kujiunga na mama yake ambaye kwa kitambo alikuwa ameachwa peke yake akiwa kainamia ungo wake akichambua mboga zake. Maana, yule kuku na vifaranga wake wametimka harakaharaka kwenda kujificha baada ya kujua kuna adui akiwawinda.
Kifaranga kimoja kimeingia kwenye mzinga wa nyuki uliokuwa pembeni umeanikwa kwa ajili ya kukauka na kwenda kunakopaswa, yaani, porini kwenye mti.
Huzuni, kama si kuzeeshwa na umaskini, bado yu kijana sawa na Joy ambaye kwa kiasi fulani utajiri, kuridhika na kuishi vizuri kunamfanya aonekane mdogo kwa Huzuni ambaye ni mdogo kwa miaka mitatu kwake.

Ni mama aliyedhoofishwa na huzuni kama jina lake kutokana na umaskini na misiba, ya wanawe. Lakini, bado maisha yanaendelea pamoja na yote hayo. Isitoshe ni mama aliyejaliwa uzuri wa asili. Pamoja na mapigo yote ya maisha, bado ushahidi kuwa alikuwa mrembo upo si haba. Sura yake ni kama kitabu cha historia. Ukimwona utasoma aina ya maisha aliyopitia. Ni

kama sarafu. Ana pande mbili. Uzuri wake wa asili na ukatili wa shida. Ni mama wa kizazi cha kale kilicholelewa kwenye maadili na kuyashika, kilichofundwa na kufundika.

Pamoja na umaskini na misiba iliyomzunguka, bado heshima yake na uvumilivu ni mfano wa kuigwa.

Shida za kimaisha na jinsi ya kupambana nazo hazijawa chanzo cha mgogoro katika ndoa yake. Sanasana zimekuwa gundi ya kuwaweka pamoja yeye na mumewe ambaye ni kama upande wake wa pili. Kwani wanapendana utadhani walioana jana! Kumbe kuna kipindi umaskini unakuwa na neema yake. Maana, mke wa mwenye duka pale jirani haishi kupigana na mumewe. Maana tangu zimtembelee naye amekuwa kipanga wa kutembelea nyumba ndogo. Ajabu anachukua hata vitoto vya shule. Juzijuzi alifumaniwa na kisichana cha Darasa la Tano. Alipelekwa mahakamani, akahonga na kurejea, utadhani hakutenda kosa.

Salamu anazomfikishia mwanawe zinatoka Kanada kwa mtoto wa Mzee Livingstone Kupata, aitwaye Mafanikio. Kupata ni tajiri na jirani yao.

Mafanikio anaishi Saskatoon, Sasketchewan nchini Kanada ambako hakuna anayejua kama anafanya kazi, biashara, anasoma au anatumia pesa ya baba yake. Isitoshe kaoa kule. Hivyo, ni kwa wakwe zake.

Angekuwa mtoto wa maskini watu wangesema alioa kule ili aweze kuukata. Lakini, yeye hana anachokata, kiasi cha kufikia kujiweka utumwani kwa ajili ya tumbo. Hata hivyo, nani anajua? Hata ulevi wa sifa kuwa kaoa mzungu unatosha kumfanya mtumwa. Maana, utumwa si wa tumbo tu.

Mafanikio aliacha simulizi kijijini kwao Githakwa alipokuja na mke wa kizungu aliyekuwa, licha ya kutojua kubeba ndoo ya maji na kupikia kuni au mkaa, akivaa suruali na kuvuta sigara ukiachia mbali kumbebesha mikoba mumewe.

Mafanikio aliwaacha hoi wanakijiji waliohoji ilikuwaje akamruhusu

mkewe kuvuta sigara wakati yeye alikuwa havuti. Wapo waliosema kuwa alikuwa hata akivuta sigara kubwa! Aliwaambia kuwa kuvuta au kutovuta ilikuwa ni mojawapo ya haki za binadamu! Walishangaa kugundua kuwa kumbe kulikuwa na haki za binadamu zinazoruhusu mtu kujidhuru na bado zikawa haki kitu!

Wakati wakishangaa hilo, Mafanikio aliwaacha hoi zaidi aliposema kuwa nchini Kanada watu wana haki hata ya wanaume kwa wanaume au wanawake kwa wanawake kuoana. Alisema kuwa mara nyingi kwao ndoa ni suala la muda. Kwani alisema kuwa kwao ndoa zinavunjika sana kutokana na wanandoa kuwa na haki kupita kiasi. Wanagithakwa hawakusita kusema kuwa huo hata kama ulikuwa uzungu, ulikuwa ni wendawazimu na uozo katika jamii, hata kama ni ya kizungu.

Pamoja na baba yake kushabikia vituko vya mzungu, wakati Mafanikio akielezea juu ya ndoa hizi, alionekana mwenye kunyong'onyea. Japo alitabasamu, tabasamu lake lilikuwa la kuudhika na kuadhirika. Lakini, angefanyaje kwa mama wa kizungu ambaye alionekana kama malaika pamoja na uzee na vituko vyake? Kweli, mwenye mapenzi haoni, chongo huita kengeza!

Pia, Mafanikio anasema kuwa kuna kipindi watu wa jinsi moja walioana kila mwaka hufanya maandamano kulaani nchi nyingine zinazopiga vita aina yao ya ndoa. Anasema badala ya polisi kuwapiga kwa kuinajisi dunia, huwapa ulinzi hadi maandamano na maadhimisho yao yanaisha!

Walipomuuliza kama nchi hiyo kweli ina watu wenye akili, aliwajibu kuwa hayo ndiyo maendeleo!

Pia, mke wa Mafanikio alikuwa na vituko vingine. Tangu kipindi walichokuja na mumewe hadi kuondoka, hakuwahi kuwapikia chakula wakwe zake wala wageni wake na mumewe. Kuna kipindi walikuwa wanalazimika kwenda mjini ili kula hotelini na kurudi.

Wakati mwingine ilibidi vyakula vya kizungu viitwavyo pizza, zucchini, kokoteili na vingine vyenye majina magumu viagizwe kutoka Fikira.

Watu walicheka hadi kuvunja mbavu pale aliposema kwao kuna chakula kinaitwa kokoteili. Wanagithakwa walimletea kokotende. Walishangaa aliposema kuwa naye anawashangaa kwa kumletea kokotende badala ya kokoteili. Hakika ilikuwa ni vituko juu ya vituko.

Ndugu zake na wanakijiji walipata taabu naye. Maana licha ya kuwa na shida ya kuwasiliana naye, hawakuwa wamezoea kumwona mwanamke akimbebesha mikoba mumewe, tena bila ya hata chembe ya aibu. Pia, kila walipotaka kupanda gari lao, Mafanikio asingepanda bila kumfungulia mlango mke wake wa kizungu. Wanakijiji walizoea kujisemea kuwa uzungu una gharama, tena si kidogo!

Lakini, Mafanikio hata siku moja hakuwahi kufunguliwa mlango na mke wake.

Pamoja na Mizengwe kupata uhuru miaka mingi, katika Kijiji cha Githakwa hapakuwa pamewahi kuzaliwa mwanamke aliyewahi kuendesha gari hivyo kitendo cha Oraiti kuendesha gari bila hata kuliangusha nacho kiliwaacha hoi wanakijiji, hasa wanaume walioamini kuwa mwanamke asingeweza kuendesha gari maana ni kazi ya kiume. Waliishiwa nguvu Mafanikio alipowaambia kuwa wakati wakija Mizengwe rubani wa ndege kubwa iliyowaleta alikuwa mwanamke.

Vituko vya mama wa kizungu vilikuwa vingi. Maana wakati mwingine alikuwa akishikana na mumewe Mafanikio kiunoni bila hata kuogopa watu! Joy, mama yake Mafanikio, siku moja alimwambia Huzuni kuwa aliwakuta wakilambana midomo, akabaki kupigwa butwaa. Alipomuuliza mwanawe kwa nini walikuwa wanafanya vitu kama hivyo bila kumjali, alijibiwa kuwa hayo ndiyo mapenzi ya kizungu. Mama yake ilibidi akubaliane na mwanawe hivyohivyo huku akiwa amejaa aibu na kihoro.

Bila ya kuwapo mumewe, hakuna mtu ambaye angeongea naye. Maana hakuwa anajua lugha ya Kigithakwa.

Halafu kila akiongea neno alizoea kuweka "oraiti" mwishoni. Wanakijiji

walimpachika jina la Oraiti pamoja na kwamba jina lake lilikuwa Megan Swyers Doug. Yeye hatumii jina la mumewe kama mama wa kiafrika. Mafanikio aliwaambia kuwa kutumia majina ya waume kulikuwa kumepitwa na wakati na isitoshe ulikuwa uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu!

Pamoja na udhaifu huu, Mzee Kupata alijisifu sana kuwa mwanawe alikuwa kasoma sana hadi kukubaliwa kuoa mzungu! Alikuwa akijisifu kuwa ukiona mtu karuhusiwa kumwoa mzungu ujue amesoma sana. Maana wazungu wamemwamini kama mwenzao. Ni tajiri sana na ameendelea sana. Kwake wanakijiji walichoona ni kama utumwa na ujinga wa kizungu, kilikuwa kama manukato na sifa kubwa kwake.

Kwake mwanamke wa kizungu alikuwa akikubali kila kitu, hata upuuzi. Maana wakati wanakijiji wakishangaa vituko vyake, yeye alishabikia tena kwa kukenuakenua meno kama mtoto mdogo! Alikuwa haachi kutabasamu kila akimwona mkamwana wake huku akiongea naye Kingereza chake cha kizamani. Aliwaacha hoi pale alipokuwa akikaa karibu na baba mkwe wakati wa kula bila ya aibu. Siku ya kwanza Mzee Kupata alikataa kula mbele ya mkwewe, lakini, angefanyaje iwapo huo ndio uzungu kwake hata kwa kujidhalilisha. Lakini, mwanawe alipomwambia kuwa hayo ndiyo mambo ya kisasa na ishara ya kuendelea, alisalimu amri hadi akazoea kuwa anakula mbele ya mkwewe tena kwa kujiamini, utadhani naye alikuwa ghafla amegeuka mzungu mweusi!

Oraiti kwa upande wake naye hakuacha kuja na vituko vyake. Alikuja na kijibwa kidogo chenye macho na masikio makubwa. Kijibwa kiliitwa Brown. Kilikuwa na sura mbaya kwelikweli.

Wanakijiji ambao walizoea kuwaona mbwa kama wanyama wachafu, walishangaa kuona yule mama alivyokuwa akikibusu kile kijibwa chake utadhani mumewe au mwanawe. Wakati wakimshangaa Oraiti kwa kumwendekeza mbwa wake, naye aliwashangaa sana kuona wanalala na mbuzi kwenye nyumba moja. Alizoea kumwambia mumewe kuwa alikuwa akiwaonea wanakijiji huruma maana wangeweza kuambukizwa magonjwa na wanyama, asijue nao walikuwa wakimshangaa kulala na

mbwa nyumbani hadi kwenye chumba cha kulala! Kweli mtu chake.

Siku nyingine alipokuwa kwenye gari lake peke yake, alikikalisha kile kijibwa kwenye kiti cha mbele na kukiendesha utadhani binadamu. Wanawake wa Githakwa walishika viuno wakishangaa jinsi ambavyo mbwa anaweza kukaa kwenye kiti cha mbele cha mumewe! Kutokana na kitendo kile, kuna wanawake waliozoea kumwita mwanamke wa mbwa kwa maana ya kupenda kuwa na kijibwa chake karibu kila mahali.

Wakati wakimshangaa hata yeye alikuwa akiwashangaa kwa jinsi walivyokuwa wakimnyanyapaa mbwa wake kipenzi. Ajabu naye alikuwa akiogopa hata kumgusa mbuzi au kondoo. Maana alisema wangeweza kumwambukiza magonjwa. Ndipo wananchi wakamuuliza Mafanikio kama mbwa wa kizungu hawana magonjwa kama mbuzi wa Githakwa. Aliwajibu kuwa mbwa wao alikuwa akipimwa afya yake mara kwa mara, tena alikuwa na daktari wake maalumu. Kuongeza maajabu alisema kuwa analipiwa kwa dola. Wanakijiji walibaki vinywa wazi maana ni wachache walikuwa wamewahi kuiona hiyo dola. Kwao dola ilikuwa ni pesa ya utajiri. Kuna kipindi walikuwa wakibishana kuwa ukipata dola umeukata wasijue dola ni pesa kama nyingine. Pamoja na Mizengwe kuwa huru, wananchi wake hasa wa vijijini walikuwa hawajawahi kuuonja uhuru. Kwao dunia ilikuwa ni pale walipoishi. Hivyo, suala la dola ni nini lilikuwa sawa na kumuuliza kuku jinsi ya kujenga nyumba.

Wanakijiji, hasa wasio na kipato, walibaki hoi, Oraiti alipokwenda buchani na kukinunulia kijibwa chake figo na maini na wakati mwingine samaki na siagi! Waliishiwa nguvu pale walipokuwa wakimwona Oraiti akiamka asubuhi kukipeleka kijibwa chake kwenda kujisaidia. Alasiri alikipeleka matembezi ili kipate mazoezi. Pamoja na mapenzi yote hayo,bado mbwa ni mbwa. Kwani licha ya kumpa kila kitu, hakukitafutia mke! Kuna siku kilimtoroka kikaenda kuchakura jalalani tena jalala lenyewe la jirani yake Baba yake Matatizo!

Kwa Oraiti, Brown alikuwa kila kitu. Aliingia kila mahali kuanzia sebuleni hadi chumba cha kulala. Pia, alizoea kumbusu na kuongea naye utadhani alikuwa mtu! Alikuwa akisema kuwa hata asingalizaa asingalikaa mpweke.

Angecheza na mbwa wake aliyependa kumuita *my dear pet*. Pia, alisema kuwa kwao kulikuwa na watu, tena matajiri, ambao walikuwa wakifa na kuwarithisha mbwa au paka wao maelfu hata malaki ya dola!

Mzee Kupata, pamoja na ukali na jeuri yake yote, akitaka aonekane kama mzungu aliyekuwa bosi wake alipokuwa shambaboi zamani, alisalimu amri kwa Brown. Maana alikuwa akiingia nyumbani kwake na kumnusanusa huku naye akikenua meno kushangilia uzungu wa mwanawe!

Brown, ilisemekana alilipiwa nauli ya ndege sawa na ya mtu kutoka huko kwao Kanada kuja Mizengwe. Inasemekana huko kwao Kanada, Brown kakatiwa bima kubwa tu sawa na Waziri wa Mizengwe!

Mafanikio alisema kuwa nchi ya Kanada ilikuwa tajiri sana kiasi cha kuweza kumlisha na kumvika mkazi yeyote ambaye hakuwa na kazi. Lakini, alisema viongozi wake hawakuwa wakwasi sana kama wale wa Mizengwe. Maana walikuwa hawawaibii wananchi wao. Anasema nchini humo wizi katika ofisi ya umma licha ya kuwa aibu kubwa hauvumiliki. Aliongeza kuwa nchi ile haina watawala bali viongozi wanaofurahia kuona watu wao wakiendelea na kuishi maisha ya maana tofauti na wa Mizengwe waliokuwa na mtimanyongo, si kawaida. Maana wengi walikuwa hawiibi kwa ajili ya shida bali roho mbaya na uroho.

Pamoja na utajiri wa familia yake, Mafanikio alioa mwanamke mzee hata kama ni wa kizungu. Sura yake ilionyesha kuwa alikuwa mzee kuliko mumewe, tena kwa miaka mingi tu. Umri wake ulijificha kwenye vipodozi na ile hali ya kutofanya kazi ngumu kama mwanamke wa Githakwa. Pia, wapo waliosema kuwa wazungu huwa wanakula dawa za kuongeza umri na kuficha uzee.

Kulikuwa na uvumi kuwa mke wa Mafanikio kama angezaa, basi asingezaa watoto wengi kama Mwafrika. Licha ya umri wake kwenda, wazungu huwa hawazai watoto wengi. Pia hawanyonyeshi sana kama wanawake wa Githakwa ambao hunyonyesha hadi miaka mitatu.

Pia, Oraiti alionekana kuwa na mamlaka kuliko Mafanikio. Huo ndio uzungu. Yaani, mama akisema baba hawezi kukohoa! Watu hawakuacha kushangaa kumwona Mafanikio akiomba ruhusa kwenda matembezi peke yake. Kituko zaidi kilitokea Mafanikio alipokuja na shangazi yake. Oraiti alimuuliza kwa hasira yule mwanamke alikuwa nani. Ghadhabu za Oraiti zilitulia alipojua kuwa yule alikuwa shangazi yake. Hata hivyo, alikubali jibu lile kwa shaka. Alisema kwao huwezi kumwamini mtu hata kama ni mama au baba mkwe lolote linaweza kutokea.

Siku nyingine alivalia nguo aina ya kimini yaani, nguo fupi, ikiishia juu ya magoti. Wanakijiji walishangaa alivyoweza kutoona aibu kwa kuonyesha mapaja yake. Wakati mwingine alivaa kichupi na kukimbia ovyoovyo huku na kule huku akiwa na kijibwa chake kikihema kwa taabu. Alizoea kusema kuwa alikuwa akijiweka imara. Wanakijiji hawakuelewa maana yake. Walizoea kumwita mkimbia na mbwa. Wanawake wengine walifikia kupiga yowe. Maana walihofia kama angeinama angemwaga radhi, isitoshe mbele ya wakweze. Lakini, yeye hakujali. Aliona kawaida!

Githakwa hawakuwa wamewahi kuona mwanamke, mtu mzima akijiumbua kiasi hiki. Walizoea kuona visichana limbukeni vilivyokuwa vikitoka kusoma sekondari vikijaribu kuvaa hivyo bila kufanikiwa. Ni mzazi gani angekubali binti yake ajidhalilishe hivyo? Kwa Wanagithakwa nguo zile zilikuwa ni za malaya hata kama alikuwa mzungu. Kuna wazee walikuwa wakiwatahadharisha watoto wao kutopita kwa Mafanikio asubuhi maana wangekutana na yule mama kavaa vinguo vyake vya nusu uchi, huenda angewasababishia mikosi. Hiyo ndiyo ilikuwa imani yao.

Pamoja na udhaifu huu wa waziwazi kwa wanakijiji wa Githakwa,bado Mafanikio aliwafanya vijana wengi watamani angekuwa ni wao. Maana wao shida zilishawafunga ubongo kiasi cha kutaka kufanya lolote liwalo waweze kuishi uzunguni ambako walizoea kupaita majuu, wasijue kuwa ulaya hakuna milima mirefu kama Githakwa ambako kuna mlima wa saba kwa ukubwa duniani uitwao Rojamaliki na mwingine uitwao Mlima Rume!

Kitu ambacho Oraiti alikuwa hafichi wala kuonea aibu ni wivu. Mama alikuwa na wivu si kawaida. Maana kila mwanamke aliyeongea na mumewe ilikuwa ni lazima amwelekeze mkewe baada ya maongezi. Alikuwa akimtafsiria kila kitu, tena kwa unyenyekevu huku akitabasamu kwa kujipendekeza. Wakati mwingine alifoka kwa kusema "Hapana! Hapana."

Siku moja shangazi yake mumewe aliudhika na kulalamika kwa nini mke wa mwanawe alikuwa hamwamini hata yeye. Mafanikio alimwambia kuwa kwa vile mke wake alikuwa amezaliwa na kukulia uzunguni hii ilikuwa ni mila yao. Kwani kwao hata mtu na shemeji yake, wifi, mjomba, kaka hata dada kuna kipindi hawaaminiani. Maana wanaweza kuwakiana tamaa wakati wowote. Pia, talaka kwao ni jambo la kawaida. Wanawake wanawawakia tamaa wanawake wenzao na wanaume kwa wanaume wenzao!

Kutokana na uhuru wa kujifanyia mambo hakuna anayeweza kuwazuia wala kuwashtaki! Hizo ndizo haki za binadamu ambazo Mzee Njema alizoea kuziita haki za kiwendawazimu, maana binadamu hujiharibu. Japo alikuwa mpenzi wa haki za binadamu, alipenda haki za binadamu zinazomfanya mtu kuwa mtu zaidi badala ya zile za laana zilizomfanya mtu kuwa mnyama. Alilaani, kwa mfano, haki ya watawala wa Mizengwe kukaa kwenye madaraka wakati hawakuwa wakiwatumikia wananchi, badala yake walikuwa wakiwatumikisha. Alizoea kumwita Rais wa Mizengwe mwizi na mnyonyaji ambaye alikuwa akihimiza watu walipe kodi wakati yeye hakuwa akilipa kodi, bali kuziiba!

Kitendo cha kuishi "Majuu" kama vijana wa kijijini kwao Githakwa wasemavyo, na kuoa mzungu licha ya kuonekana mzee, kinamfanya anaonekana kuukata kuliko hata ndugu zake walioko nchini Mizengwe.

Japo waliona kama wazungu walikuwa na mila chafu, lakini kwa vile walikuwa ni wazungu kwao kila upuuzi haukuwakatisha tamaa ya kutamani uzungu na kuishi uzunguni kama wangejaliwa.

Maana wananchi wa Mizengwe wana ugonjwa wa kupenda nchi za

wenzao na kuchukia yao. Wanachukia hata vitu na mila zao na kupenda vya wenzao, tena vingi vya ovyo. Ni vijana waliokata tamaa kiasi cha kutojithamini! Lakini, si kosa lao. Maana kuna kipindi magazeti yaliandika kuwa hata viongozi wa Mizengwe hufanya ziara nyingi ulaya kuliko vijijini walikovuna kura nyingi. Pia, magazeti yaliendelea kusema kuwa viongozi wengi wa Mizengwe walikuwa wakitibiwa,kusomeshea hata kuweka pesa zao Majuu. Kwao majuu ilikuwa ni kama mbinguni. Hii ndiyo sababu hata wakati wa Vikao vya Bunge la Mizengwe wabunge wengi walikuwa wakichanganya Kimizengwe na Kimajuu ili waonekane wamesoma sana. Hata wataalamu wa Mizengwe waliokuwa wamesoma hawakuthaminiwa. Kwani serikali ya Mizengwe ilikuwa ikilipa pesa nyingi kuagiza wataalamu kutoka nje bila kujali kama walikuwa wataalamu kweli au wasasi wa ngawira.

Hii ni baada ya uongozi na usimamizi mbaya na ubadhirifu kuifilisi Mizengwe hadi kubakia neema ya wachache wenye mali au vyeo ilhali maskini walio wengi wakijilaumu kuzaliwa nchini humo.

Mlevi mmoja anayeitwa Ndirangu Mwai alizoea kulaumu tabia hii ya viongozi. Alizoea kusema kuwa jogoo aliwafundisha vifaranga kunya ndani. Maana kama si wao kuichukia Mizengwe na kuiharibu, watu wa Mizengwe wangalipenda nchi yao na mila zao.

Pia na ukoloni ulichangia kwa namna moja au nyingine, ingawa wengi wa waliosoma na kufanikiwa ni watoto wa wale walioiasi Githakwa na kutumikia mila na dini za kigeni. Ila cha ajabu hata hizo dini bado hazina huruma. Pamoja na kusomesha Wanamizengwe na kuwafundisha wizi, nazo kama wao bado ziko zinawanyonya Wanamizengwe. Kwani kila wiki ni sadaka bila kujali hata maskini hawa. Mungu wao amekuwa wa kuchangiwa badala ya kuwachangia wananchi. Maana tunaambiwa ni tajiri kuliko matajiri wote duniani. Mlevi mmoja aliwahi kuuliza kama ni kweli mbona anachangiwa tena pesa ya mabua ya Mizengwe?

2

Kabla ya kuoa, Matatizo alijaribu mara nyingi kudandia meli ili angalau akafanye kibarua chochote ulaya hata kama ni kudeki vyoo au kutunza vikongwe vya kizungu au kuhudumia mbwa wa wazungu, bila mafanikio kama jina la rafiki yake Mafanikio.

Alidandia meli mara nyingi akaambulia kukamatwa mara tatu na kurudishwa na kutumikia vifungo. Kuna kipindi alisema kuwa Giriki alitaka kumtosa baharini baada ya kumvumbua kwenye chumba cha jenereta ya meli kama alivyowaambia wenzake kuwa alimvumbua Matatizo utadhani alikuwa kiumbe mpya.

Alibembeleza sana na mwishowe kutupwa Pwani ya Visiwa vya Solomon alipokamatwa na kusafirishwa kurejeshwa Mizengwe. Alikuwa akiwachekesha sana vijana alipokuwa akieleza jinsi alivyovumbuliwa na jinsi alivyobembeleza hadi kuzawadiwa kifungo.

Alizoea kuwasimulia vijana wenzake kuacha mawazo na tamaa ya kudandia meli. Maana kuna kipindi marafiki zake wanne walitoswa baharini na kuishia kuwa kitoweo cha papa.

Mwishowe alikubali kushindwa na kurejea na kutulia kijijini Githakwa ambapo anapambana na dhiki kama wanakijiji wengine waliokata tamaa ya maisha. Tofauti ni kwamba angalau ameona mwanga katika safari zake za kudandia meli. Hivyo hajakata tamaa. Bado ana imani kuwa ipo siku atafanikiwa. Hili linaongezwa nguvu na maongezi na misimamo ya mzee Njema ambaye anaamini kuna siku wananchi watajikomboa kutoka kwenye kongwa za kunyonywa na kikundi kidogo cha watu.

Wakati ule kulikuwa na usemi kuwa ni heri kuzaliwa ukiwa paka Ulaya kuliko mtu Mizengwe! Hii ni alama ya kukata tamaa iliyokuwa imewakumba vijana wakati ule. Japo haikuwa hivyo, kwao Ulaya ilikuwa ni alama ya neema na kila vinono.

Kwani kila walichojaribu kufanya, walisalitiwa na kuangushwa na kikundi cha watu, tena wachache madarakani. Wapo waliojaribu kilimo na kukatishwa tamaa kwa mazao yao kukosa wanunuzi, kukopwa au kulanguliwa na walanguzi wa mazao waliokuwa wametapakaa nchi nzima. Hawa walikuwa na baraka zote za serikali kuwanyonya wakulima!

Wengine walijaribu kuvusha mazao yaliyopewa jina zuri la mazao ya biashara kimagendo kwenda nchi jirani bila mafanikio.

Mazao haya nayo yaliwaletea ukoloni mwingine. Maana hayaliwi au kuwa na matumizi mengi katika kijiji hata nchi yao. Hapa ndipo serikali ya Mizengwe ilipowabana. Kwani ndiyo iliyokuwa ikishughulikia kupanga bei na kutafuta masoko.

Wakati mwingine wananchi wa Mizengwe walikosa chakula kabisa. Kwani walihamasishwa na waliaminishwa na watawala wao wa Mizengwe kwamba mazao ya biashara ni bora na yanawapatia pesa. Matokeo yake walitumia ardhi na nguvu yao yote kwenye kulima mazao haya ya kuuza ughaibuni badala ya yale ya chakula.

Askari wa mipakani nao pia walitumia mwanya huu. Kwani waliwatoza rushwa kubwa kiasi cha kujikuta wakiambua hasara ukiachia mbali mara nyingine kutekwa kwenye msitu wa Nthethe na majambazi wakielekea mpakani usiku kuwaepa askari wa doria waliokuwa wametapakaa barabarani wakifanya kazi ya kusaka ngawira kwa kisingizio cha doria.

Ilifikia mahali nchi ikawa kama haina mwenyewe. Maana wale waliokuwa wakiwalangua wananchi mazao yao wengi walitoka mataifa ya kigeni.

Pamoja na matatizo haya yote, wakulima wa Mizengwe walijaribu kwa kila hali kutorosha mazao yao kwenda nchi jirani kwa imani kwamba wangefanikiwa kukwepa adha zinazoambatana na utoroshaji wa mazao hayo, ili angalau kurudisha robo tatu ya gharama walizotumia kuzalisha. Ukweli ni kwamba kama wangeuza nchini mwao wasingeweza hata kurudisha robo kutokana na mipango mibovu ya soko "holela" ambalo walizoea kuliita soko huria.

Nchi jirani ilikuwa na mfumo unaofanana na ule wa Mizengwe. Kuna swali lililokuwa likiwasumbua Wanagithakwa. Nalo ni kwa nini mfumo wa soko holela uliopo Mizengwe ni sawa na wa nchi hiyo, lakini kwa nini bei ya nchi jirani iwe bora kuliko ya Mizengwe? Mizengwe kwelikweli!

Pia, hali hii ilikuwa ni ukumbusho kwa serikali ya Mizengwe kuchukua hatua mujarabu na madhubuti za kuboresha maisha ingawa hali ilikuja kuwa tofauti.

Serikali haikujihangaisha nao isipokuwa wakati wa uchaguzi ambapo waliletewa kila aina ya vitu hata ambavyo hawakuvihitaji. Zililetwa bendi za muziki na ahadi za kupewa mikopo ya kuanzisha biashara. Baada ya uchaguzi ahadi walizozitoa zilitoweka, wakabaki kwenye dhiki zao.

Kilichoongeza pigo ni ile hali ya uchumi wao kutegemea kilimo ambacho kilikuwa kimesahaulika kiasi cha kukosa motisha. Hili lilifanya vijana wengi wenye nguvu kukimbilia mijini kuuza bidhaa ndogondogo kwa ajili ya kupata pesa ya kula.

Pamoja na kufanya hivyo, bado walichezea kwenye nyavu za adui yuleyule. Maana licha ya bidhaa hizo kuwa na kiwango dhaifu, ziliagizwa kutoka nchi za nje, hivyo kuchangia uchumi wa nchi hizo badala ya Mizengwe.

Nchi ya Mizengwe ilikuwa ikiagiza nje hata juisi bandia wakati matunda yakiozea mashambani mwa wakulima.

Watu wake walilima pamba na kuvaa mitumba! Walikuwa na maisha sawa na ya kuku ambaye "huzaa" asichokula na kula asichozalisha. Maana kuku hutaga mayai na kuishia kula nafaka, tena kavu.

Pamoja na kuwa na ardhi yenye rutuba na watu wenye nguvu, kuna kipindi wananchi wa nchi hii walikuwa wakisumbuliwa na njaa mara kwa mara hadi kuagiza vyakula kutoka nchi zenye udongo na hali ya hewa mbaya zikilinganishwa na Mizengwe.

Hivi vikichangiwa na usimamizi na uongozi mbovu wa Mizengwe, viliongeza uzito kwenye maisha ya wananchi walio wengi. Huku watawala wao wakitapanya pesa kwenye mambo yasiyokuwa na maana kama ziara za ugenini,sherehe na ubadhirifu.

Ajabu viongozi wa Mizengwe walikuwa ni watu wenye utajiri mkubwa lakini wakiwa wanaongoza nchi iliyoishi kwa kuombaomba kutoka mataifa ya nje. Ajabu hata wao hawakuona aibu kuomba. Sanasana waliona fahari. Maana kwa ombaomba, baadhi yao walikuwa wakijiingizia pesa nyingi ya kuficha Ulaya na kuchezea.

Hali hii ilimfanya Matatizo kujiuliza mara nyingi bila kupata jibu, kwa nini ndege wasio hata na nusu ya akili walikuwa wakila na kunenepa, wakati watu wake walikuwa wanakula kwa kubabaisha wakiishia kukonda na kunyauka?

Kuna kipindi alikuwa akitamani angeumbika ndege. Maana ndege, licha ya kuifaidi dunia kwa kuruka na kupaa na kula bila kuzalisha, kuna kipindi wanakuwa na aibu kuliko binadamu ambao hawakuonea aibu udhalili wa wenzao, bali kuutumia kuchuma.

Matatizo aliwapenda ndege na maisha yao. Hawakuwa wakiamriwa kupanga uzazi wala kufunga mikanda. Wanaishi watakavyo na walivyo bila ya kumwathiri yeyote.

Alikuwa akikumbuka kanga aliyemnasa mtegoni mwake alipokuwa mdogo. Alitaka amfuge. Alipomfikisha nyumbani na kumpa mahindi, kanga hakuyala hadi alipotoka. Maana aliona aibu kulishwa wakati alikuwa amezoea kujilisha.

Watu wa Githakwa hawakuwa na mwanga. Walikuwa wamepotea kwenye kiza cha njaa. Maana wengi wa vijana walikuwa na mawazo ya kutafuta pesa ya kula wasijue ya kuolea, kujengea, kulelea, kusomesha hata wakati mwingine kuburudika wangeipata wapi. Hili pia liliongeza tatizo la vijana kutooa na kuolewa kwa wakati, kiasi cha kuwafanya mateka wa matendo

na tabia mbovu za umalaya, uvivu, uzururaji na UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa, ukiachia mbali ujambazi, uvutaji bangi, ulevi, udokozi na hata utapeli.
Walikuwa wakijiona kama taifa lililopotea. Ilifikia mahali mpaka wakosoaji wengine wakawapachika jina la 'Matching guys' au Wamachinga na bomu lililokuwa likitika likingoja kulipuka wakati wowote.

Mzee Kupata ni msomi na kuwadi wa zamani wa ukoloni ambaye mwanzoni alikuwa shambaboi wa mzungu.

Alifanikiwa kumaliza Darasa la Nane baada ya bwana wake mzungu aliyeitwa Livingstone Harry, ambaye alichukua jina lake, kumlipia karo wakati wa ukoloni.

Ni tajiri na baba wa watoto saba. Mtoto wake wa kwanza ni rubani. Wa pili ni mwanasheria ambaye taaluma yake imemfanya atokee kuwa tajiri kuliko hata baba yake. Huyu utajiri wake umetokana na kusainisha serikali na wawekezaji mikataba mibovu ambapo hupewa kamisheni kubwa. Kimsingi fedha yake ni matokeo ya jinai ya kuuza nchi na watu wake mwenyewe.

Wa tatu ni Mbunge wa Jimbo la Mazonge kwenye mkoa wa Chelewa katika nchi ya Mizengwe. Huyu anaitwa Harry. Alichukuwa jina la baba wa baba wa bosi wa baba yake Livingstone Harry. Wananchi humwita Heri. Ni heri kwelikweli kwa familia yake ingawa ni shari na sumu kwa wananchi.

Maana alizoea kurejea na kukaa kwao kila ulipokaribia uchaguzi ambapo ungemkuta kajichanganya na wananchi kama mwenzao. Lakini, kila alipochaguliwa ulikuwa ndio mwisho wa kuchanganyikana na watu wala kuishi jimboni mwake.

Muda mwingi alikuwa akiishi mji mkuu wa Fikira akishughulikia maslahi binafsi.

Kwani akishirikiana na wakubwa wenzake, amekula njama ya kuwahamisha

wanakijiji cha Githakwa ili kupisha upanuzi wa mradi wa kuchimba vito unaomilkiwa kwa ubia kati yake na wenzake na mwekezaji wa kizungu aitwaye Glutton Sucker.
Mradi huu, licha ya kutishia maisha ya wanakijiji kwa uchafuzi wa maadili na mazingira yao,hauna faida kwao.

Hii inawafanya watu wa Githakwa, licha ya kumchukia, wamwone kama mkoloni mweusi na wa kisasa.

Mtoto wa nne wa mzee Kupata ni mfanyabiashara maarufu nchini Mizengwe. Huyu licha ya kuwa na biashara na pesa nyingi, biashara zake zinatia shaka hasa ulanguzi na utoroshaji nje wa pesa, nyara za taifa na vito. Yeye na familia yake, ingawa wanaishi kwenye mkoa wa Chelewa, hawakuchelewa. Waliwahi tena sana! Wanaishi kwenye nchi ya Mizengwe, hawakuzenguliwa, wanaula na wanazengua. Maana kila mwanakijiji angetamani awe na maisha bora kama wao.

Wao ni vizito, walao kwa mirija, wakasaza na kumwaga wakati wengine akina yahe kama baba yake Matatizo, ni watu wa kufunga mkanda na kufa hata kwa njaa. Kila mwaka serikali ya Mizengwe huwaambia wakaze mikanda maana ipo siku mambo yatanyoka, ingawa hayanyoki.

Wanashiba kwa imani wakati wenzao wanajiuliza leo wale nini. Wanachagua vyakula na kula ya siku kwao si jambo la kuwahangaisha! Wana pesa na utajiri wa kumwaga. Wakati wananchi wa kawaida wakifunga mikanda, watawala wao wanapanua matumbo ili kula zaidi na zaidi na kutapanya zaidi na zaidi! Walijisemea wahenga kuwa kweli dunia ni tambara bovu.

Wakubwa na wenye nazo wanaishi kwenye pepo na kisiwa cha amani kilichozungukwa na jehanamu ya imani ya kuwa na amani bila ya kuionja hiyo amani. Kwa lugha rahisi sana kinachokosekana nchini Mizengwe ni vita vya mtutu wa bunduki. Lakini, wananchi walio wengi wanatambua fika kwamba amani kwa upana wake haipo hata chembe. Wanajua wazi kuwa nchi yao iko kwenye vita vya kitabaka ambapo wachache wanawatumia wengi.

Kwa walio wengi Mizengwe hakuna amani. Kuna vurugu za kichinichini kati ya walio nacho na wasio nacho ambao wanatamani kuwapindua na kuwateketeza wenzao walio nacho.

Kwa upande wa walio nacho, nao wanawahofia wasio nacho kiasi cha kujizungushia kuta kama wafungwa kuepuka kudhuriwa na maskini waliowanzunguka ambao kimsingi ndio waliowapandisha huko juu walipo.

Woga ndio mtawala mkuu wa watu hawa. Haya ndiyo matokeo ya kutoweka kwa haki. Haki imetoweka na woga na jinai zimechukua mahali pake.

Wana Mizengwe matajiri wanaaminisha wanuka njaa kuwa Mizengwe ni nchi ya amani. Wengine hujiuliza kama amani ni imani au kushiba na kufaidi maisha. Wengi wamejaribu kuhoji. Lakini, wakubwa wamewapachika majina ya kuwa ni maadui wa amani. Amani kwa wakubwa ni wao kushiba kwa kuwanyonya maskini. Kwa maskini amani ni kukubali kunyonywa na wakubwa! Hiyo ndiyo Mizengwe.

Mtoto wa tano wa mzee kupata ni mke wa waziri, tena Waziri wa Fedha ambaye mwaka jana alisababisha kizaazaa baada ya kugundulika kuwa wizara yake ilikuwa ikikopa pesa nje na kuzitumia vibaya kiasi cha kuwaongezea mzigo walipa kodi maskini wa Mizengwe.

Yeye waziri na wenzake walichokuwa wanajali ni kupewa asilimia kumi yao na kuiingiza nchi na hatima yake msibani.

Hata hivyo, pamoja na hujuma hii na shinikizo kuwa afukuzwe kazi na kufungwa, bado anachapa kazi maana anafahamiana na kiongozi wa nchi ya Mizengwe ambaye walisoma pamoja. Isitoshe yeye aliwahi kuukata kiasi cha kumdhamini kiongozi huyo kwa kumchangishia pesa za kuwahonga wapiga kura, hali iliyosababisha awashinde wapinzani wake waliokuwa maskini.

Wakati wa uchaguzi mkuu inasemekana alichangisha pesa nyingi kutoka kwa wafanyabiashara wengi. Hii ndiyo siri ya serikali ya Mizengwe kuwa karibu na wafanyabiashara badala ya wananchi.

Hii ndiyo maana hata wafanyabiashara wanaojulikana kwa madhambi kama kuuza mihadarati,kutorosha pesa hata kufadhili jambazi hawana wasiwasi na jinai yao. Watakuwaje na wasiwasi iwapo mtu wao ndiye yuko jikoni?

Pia, inasemekana ana biashara nyingi nje ya nchi ambazo anazimilki na watu wengine wazito serikalini. Kimsingi, serikali ni kama yake. Ameiweka mfukoni mwake na wenzake wenye madaraka.

Kweli, siku zote maji hufuata mkondo. Baba nyumbani atokako anazo na mumewe anazo, tena ndiye bosi mwenyewe wa fedha! Ila siku hizi kutokana na kukua kwa teknolojia kuna kipindi maji yanapanda mlima kupitia kwenye bomba ambalo huweza hata kuuziba mkondo.

3

Ama kweli siku ya kupata, Mwenyezi Mungu hakutumii barua! Wahenga walisema.

Hata hivi ukichunguza kila kùpata, kupata kwingine kuna mengi tena machafu nyumaye na yenye wingi wa utata japo si wote wapatao ni wachafu.

Wengine wameua tena watoto,wake zao hata ndugu zao ama kwa maelekezo ya waganga au kwa kutumia nyadhifa zao, wengine kwa dhuluma na wengine hivyohivyo.

Wengine waliopata kupitia mgongo wa nyadhifa zao waliwauza wananchi wao na kujineemesha wao na familia zao huku wananchi wakizidi kudhoofika!

Familia ya Kupata ina kila aina ya watu tena waliofanikiwa. Ni familia yenye vyote. Ina ukwasi na watoto waliosoma hata kama bongo zao hazikuwa zikichemka vilivyo kama za watoto wa mzee Shida ambaye aliangushwa na umaskini. Ni familia ya pekee kijijini Githakwa hata mkoani Chelewa. Ina jina na nafasi.

Pia, inasemekana Mzee Kupata alikuwa akinunua nafasi za watoto wa maskini walioshinda kwenda sekondari kutoka kwa walimu wakuu zilizowawezesha watoto wake kusoma bure wakati elimu ilipokuwa bure.

Anayefuatia mke wa waziri naye ni wa kike. Licha ya kuwa daktari tena bingwa naye kaolewa Ulaya. Anaitwa Dolly.

Watoto wa Kupata walilogewa kwa wazungu. Maana huyu binti naye aliwahi kuja na mume wake mzungu. Mume mwenyewe alikuwa ni mzee hata kuliko mzee Kupata mwenyewe, ingawa ilisemekana kuwa alikuwa tajiri huko kwao. Aliitwa Mann Younghusband. Dolly alipenda sana kujiita bibi Younghusband. Dolly aliolewa na mzungu mzee sawa na kaka yake

Mafanikio aliyeoa mzungu mzee.

Wanagithakwa huwa ni watu wacheshi wanaopenda sana utani. Kwani kama dada yake, yaani, mke mzungu wa Mafanikio, naye walimpatia jina lake la utani. Walimwita Chimbuchimbu kutokana na kupenda sana kuwachokonoa wadudu na kuwapiga picha.

Baadaye iligundulika kuwa kumbe naye alikuwa daktari kama mkewe. Alikuwa akifundisha chuo kikuu kwao. Hivyo katika safari yake ukweni, alifaidika kwa kukamilisha utafiti wake wa wadudu wa kitropiki uliompatia pesa nyingi baada ya kuandika matokeo ya utafiti huu na kuiuza dunia nzima ikiwamo Mizengwe.

Ilisemekana kuwa huyu mzungu alimuoa Mwafrika ili kumtumia kuja Mizengwe kufanya utalii na utafiti kwa gharama nafuu wakati na binti Kupata naye alikubali kuolewa na mzungu ili afaidi kurithi mali zake atakapokufa. Wote walikuwa wanatumiana.

Mdogo wake daktari, mke wa mzungu, ni Ofisa wa Mamlaka ya Mapato. Huyu kwa kutumia mwanya wa kushamiri rushwa kwenye nchi ya Mizengwe, alifanikiwa kuiba pesa nyingi alizopata kwa kutoa misamaha ya kodi na kukwepa kodi. Hujuma hii ilifanikiwa sana kutokana na shemeji yake kuwa Waziri wa Fedha. Inasemekana ana majumba na vitegauchumi karibu kila mji nchini Mizengwe. Tena yu bado kijana mdogo tu!

Kuna siku Matatizo alimtolea uvivu na kumwita mhujumu wa uchumi. Baba yake alikuja juu na kumlazimisha baba yake Matatizo, mzee Shida, kuomba msamaha. Maana alikuwa ametishia kumshtaki kwa kosa la kukashifu familia yake.

Hivyo aliyepewa, kapewa vyote. Hata kama akikuonea kwenye mfumo mbovu wa Mizengwe angefika polisi au mahakamani na kununua haki yako na kukuacha wewe matatani. Hivyo, baba yake Matatizo kwa kujua udhaifu huu alikubali yaishe. Aliona ni bora kufunika kombe na mwanaharamu kupita.

Alifikiria mambo mengi wakati akiamua kukubali yaishe. Kwao kuna kipato

naye ni Ofisa Mapato. Kupata juu ya kupata! Ama kweli riziki ikikulenga hakuna awezaye kuiziba. Isitoshe kutokana na haki kulanguliwa, kama dagaa sokoni, angepoteza muda wake kubishana na mwenye nazo. Alijua fika kuwa nazi haiwezi kushindana na jiwe. Pia, hata jiwe likae majini miaka mia haligeuki kuwa nazi. Hivyo, alitumia busara ya kiutu uzima kuepusha shari.

Funga kazi ni Mafanikio anayeishi Kanada akiwa na mke wake wa kizungu.

Kupata na mkewe Furaha walikwisha kupata wanachotaka na wanafurahia maisha. Wana mali. Wamesomesha watoto wao wote, tena kwenye shule za bei mbaya.

Wameozesha watoto wao tena kwa watu wenye nafasi kama wao na wana wajukuu wenye kila dalili za maisha mazuri. Mungu awape nini? Kwao maisha ni jambo la kufurahia na kujisikia. Wanajulikana nchi nzima ya Mizengwe hata Ulaya.

Hata hivyo, mzee Kupata pamoja na kupata kwake, haishi kuishi kwa wasiwasi. Majumba yake na ya wanawe yamezungushiwa kuta kama magereza kwa kuhofia kuibiwa, hata kuuawa na jeshi la majambazi wasio na ajira wala matumaini ya maisha.

Alitumia gharama kubwa kwenye ulinzi kuliko hata ujenzi wenyewe. Haya ndiyo maisha ya kila siku ya nchi ya Mizengwe. Kujifungia kwenye ngome kama wafungwa.

Mtaalamu mmoja aliwahi kuonya kuwa dawa ya usalama si kuta bali kuachana na uchoyo na wizi wa mali ya umma na badala yake kuwawezesha vijana kujitegemea kwa kujenga mazingira mazuri ya uchapaji kazi na uwajibikaji serikalini. Bahati mbaya hakuna aliyemsikiliza.

4

Wakati Kupata na mkewe Furaha wakitanua na kufaidi, upande wa pili wa maisha tena mtaa mmoja jirani ipo familia ya Mzee Shida Molowo. Huyu kama jina lake ni shida kwelikweli. Kwani licha ya shida kuwa maisha yake, shida huwa hazimwishii. Akitembea ni shida. Akilala ni shida. Maana ya maisha kwake ni shidashida.

Lugha ya mitaani inayotumika kuelezea njaa waliyonayo familia ya Mzee Shida ni kwamba njaa imefanya makao tumboni kwao, huku kwa watawala imefanya hivyo vichwani mwao. Maana hawaibii njaa ya tumbo bali ya ubongo.

Yeye ni kati ya wale wanaojiona wako sehemu mbaya kwa wakati mbaya. Amekata tamaa kwa kiasi fulani kutokana na aina ya maisha anayoishi na mfumo unaomwongoza kila siku kutokuwa na haki wala huruma bali dhuluma na ukandamizaji.

Huyu sawa na mkewe na wanawe, anaona amesalitiwa na wale aliotegemea wangemkomboa,kumthamini na kubwa katika yote kumpa na kulinda haki zake kama mwanajamii katika nchi huru.

Hutupa lawama zake zote kwenye siasa. Anaichukia siasa. Huwa hata hahudhurii mikutano ya kisiasa zaidi ya kujichimbia kwenye dunia yake ya kuhangaika na maisha yake ya kijungujiko.

Matatizo, mtoto wa Bwana Shida na bibi Huzuni, licha ya kuwa matatizo kweli ana matatizo. Hana elimu wala ajira. Haujui mwisho na mwanzo wake ni upi. Yeye kwake maisha ni kama adhabu na matatizo kama jina lake. Ila anayo sifa moja kuu.

Sifa yake nyingine ni kujaribu kila anapopata upenyo. Yeye hujiita fisi. Maana fisi huwa haridhiki au aache kupambana hadi kapata akipatacho. Pia, anayo sifa nyingine. Nayo ni kujiamini na kutokata tamaa. Pamoja na

kuwa na kisomo kidogo, huwa haachi kutafuta jibu la misiba ya familia yake. Hii ndiyo siri ya kufahamiana na Mzee Njema Waithaka ambaye anaogopewa kijiji kizima kwa ujabali wake.

Licha ya kuwa na kichwa kinachochemka, nafasi yake ya kwenda sekondari ilisemekana iliuzwa. Kuna wanaosema kuwa ilinunuliwa na jirani yake Mzee Kupata na rafiki wa Mafanikio ndiye aliyekwenda sekondari badala yake. Huenda hii ndiyo imefanya Mafanikio amtumie salamu kutoka Kanada.

Wakati ule serikali ilikuwa ikitoa elimu bure kabla ya kuharibikiwa na kuanza kuiuza kama nazi baada ya wazungu kuiamuru ifanye hivyo ili kuzalisha taifa la mbumbumbu na wasomi wachache ambao ni watoto wa watawala na kuwanyonya kiulaini.

Ana bahati mbaya. Alizaliwa baada ya ukoloni wa wakoloni weusi na sasa atazaa watoto wake kweye siasa za uwekezaji na ubinafsishaji ambako wakoloni weusi wamefunga ndoa na wakoloni weupe. Si wakati wa mwanzo ambapo elimu ilikuwa bure. Ukoloni ndani ya ukoloni na juu ya ukoloni!

Bahati mbaya sana wakati wa mwanzo alichelewa kuanza maisha kutokana na umaskini uliomfanya achelewe kuoa hadi alipompata maskini mwenzake.

Alipoteza miaka mingi akijaribu kudandia meli kwenda ughaibuni ili apate kibarua aweze kuikwamua familia yake, hata kujiendeleza kielimu, bila mafanikio. Alijikuta akikamatwa mara tatu na kuishia kutumikia vifungo hadi alipokubali yaishe na kurejea kijijini kwao. Maana nyumbani ni nyumbani hata kama ni pangoni.

Nani mwenye kipato chake atapenda kuoa au kuolewa kwenye familia ya maskini? Matajiri wanaozeshana na maskini wachache wenye bahati wanaozesha kwa matajiri. Watoto wengi wa matajiri wanafungiwa kwenye shule zao za bei mbaya zilizozungushiwa kuta na zinalindwa na walinzi wenye mitambo ya hadhari.

Wakati maskini akihangaika na pesa ya matibabu, kula au elimu, mtaa wa pili matajiri wanaandaa sherehe za harusi na kuzaliwa ambazo ni mara mia ya kusomesha mtoto wa maskini! "Kweli dunia ya leo imebadilika na kupinduka kichwa chini miguu juu!" Aliwahi kuimba mwanamuziki mmoja wa Mizengwe.

Binadamu anamla binadamu mwenzie. Hata wanyama wamewazidi watu wa Mizengwe. Kwani simba hawezi kula nyama ya simba mwenzie. Hata fisi na uroho wake wote hawezi kula nyama ya fisi mwenzie.

Kuna hili balaa jipya. Linaitwa utandawazi na uwekezaji unaolenga kuleta na uchumi wa kisasa. Matatizo huuita utandawizi unaolenga kuleta uchumi wa kisasi. Maana kwake utandawizi ni kuigeuza Mizengwe kuwa jalala la kila uchafu kuanzia wa vitu, sera hadi maadili unaofanywa na nchi tajiri.

Bahati mbaya sana serikali ya Mizengwe bila hata hadhari imeuingia mtego huu kwa kishindo kama Tsunami! Zamani ilikuwa ikitoa mikopo na ruzuku kwa wakulima. Baada ya kuuvaa utandawizi wazungu waliamuru iache kufanya hivyo. Kuhakikisha hili linafanikiwa, waliyanunua mabenki na taasisi zilizokuwa zikitoa mikopo na motisha kwa wakulima.

Ngonjera nyingi na mashairi vimeimbwa kusifia uzuri wa ubaya na uchafu huu. Lakini, ukiangalia hali za wananchi unapata kitu tofauti kabisa. Bahati mbaya watawala wameziba masikio kwa vile wanapata mradi wao.

Japo watandawazi na wawekezaji wanachuma bure, kwa mlalahoi wa Mizengwe hana chake bali kuliwa tu. Analiwa bure kwa kukamuliwa kodi na kuambulia bure!

Kwa upande mwingine Shida, baba yake Matatizo, ni mtu anayejiona kama mwenye nuksi duniani. Anajihisi ana bahati mbaya na ni mwingi wa hasira. Kwake maisha ni kama adhabu. Matatizo yake yalianzia pale alipokataa kuabudu dini za kigeni ambazo kwake hadi leo anaziona kama nyenzo za kumdhoofisha, kumdhalilisha na kumnyonya mtu mweusi. Kwani katika mji mkuu wa Fikira na miji mingine ya majimbo kuna mashindano ya kuanzishwa kwa dini hizi ambazo licha ya kupigana vita

zinachuma pesa nyingi huku madhambi yakiongezeka. Huwa anashangaa dini hizi zinavyotapanya mamilioni ya pesa kutangaza biashara zao kwenye televisheni wakati watu maskini kama yeye wanateseka kwa shida za kawaida.

Pia, dini hizi taratibu zinaanza kuwagawa wana-Mizengwe ambao kiasili ni watu wamoja. Yote hii inasababishwa na kugombea waumini kwa ajili ya kuwanyonya na kuwatumia.

Pigo linaongezeka zaidi hasa pale viongozi wa dini na serikali yao wanapokuwa wamoja.

Huwa haishi kujiuliza sababu za ushirika huu baina ya viongozi wa dini na watawala ambao ni wezi wa Mizengwe. Mzee Njema hudai wanalala kitanda kimoja na kufanya ufuska wa kuwauza wananchi.

Wakati kwa wengine maisha ni sherehe, kwa wengine ni kizunguzungu, hasa mzee Shida na ukoo wake! Yeye ana kifungo cha maisha.

Kwa tajiri ni fedha ukwasi na ufanisi. Kwa wenye madaraka maisha ni madaraka na kwa akina Shida maisha ni shida.

5

Kwa upande wa Matatizo, licha ya nafasi yake kununuliwa na kushindwa kwenda sekondari, mdogo wake Masumbuko yupo anasumbuka gerezani. Masumbuko alishiriki ujambazi na kupatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha maisha. Alifanya ujambazi kwa kutumia bunduki. Laiti angalisoma asingalifanya ujambazi wa kutumia kalamu ambao si kosa la jinai nchini Mizengwe. Maana unafanywa na wakubwa.

Kama Masumbuko angalikuwa amesoma, asingalifungwa. Angefungwaje wakati ujambazi wa ofisini ndiyo umegeuka njia ya kutajirikia? Watu wa Mizengwe wamezenguliwa hadi kuwachoma vibaka huku wakiwaabudia vibaka na majambazi wa kalamu.

Hapa ndipo familia ya Kupata na wengine wa kada yake inapowazidi kete akina Shida na kada yake.

Kwenye tukio hilo la ujambazi alioshiriki Masumbuko,watu watatu walijeruhiwa. Hata hivyo, kesi yake ilisababisha hisia nyingi.

Wapo wanaoamini alifungwa kwa sababu ya kuwa mtoto wa maskini na wapo wanaoona alistahili. Maana kuwa maskini si kigezo cha kuiba.

Inasemekana alikuwa ameajiriwa na tajiri fulani mjini kufanya ujambazi. Baada ya kukamatwa tajiri wake alimtelekeza na wala hakutaka ijulikane kuwa ndiye alikuwa akiwafadhili bunduki na kuuza mali walizokuwa wakiiba akina Masumbuko. Sasa yupo anasumbuka gerezani wakati tajiri anatumbua jasho lake la ujambazi.

Wala ukimwona huyo tajiri-jambazi aliyekuwa akimtumia Masumbuko, huwezi kuamini. Anatoa sadaka makanisani hata michango ya kuyajenga. Ni mtu na sifa zake. Anatembelea na kubadili magari. Amejenga majumba mjini na ana biashara kubwa tu. Ni mtu wa haja kwa juu japo ndani ni uoza kama kaburi. Maana kaburi hung'aa juu japo ndani kuna uoza.

Juzijuzi kwenye bahati nasibu ya kuchangisha pesa ya ujenzi wa kanisa kuu alishinda gari! Yeye kila Jumapili ni mtu wa kuondoka na baraka kutoka kwa watoa baraka wanaosalisha kwenye nyumba ya Mungu asiye Mungu.

Ana uhusiano mzuri na hawa viongozi. Kwani hivi karibuni alichaguliwa kuwa kiongozi wa wazee wa kanisa! Kweli huyu Mungu!

Kweli mwenye nacho huongezewa na asiyenacho hunyang'anywa hata kidogo alicho nacho.

"Kwanza tangu lini nyumba ya ibada ikachangiwa na bahati nasibu?" Aliwahi kuuliza Ndirangu ambaye viongozi wa dini walipomsikia walisema alikuwa na mapepo yaliyomfanya apinge "kazi" ya Mungu.

Watu wa Mungu kwa kusema hivi waliwataka waumini kufunga na kumuombea Ndirangu apone mapepo yaliyokuwa yakimsumbua hadi kuhoji kazi ya Mungu!

Kazi ya Mungu siku hizi imekuwa tata. Maana kila atakayetaka kuchuma hufanya hivyo mgongoni mwa Mungu. Wapo wanaothubutu hata kuwaombea viongozi wezi wa Mizengwe kumbe nao wagawiwe chumo lao la wizi. Wanawaombea na kuwabariki badala ya kuwakemea na kuwalaani!

Ukimwona jamaa anavyoheshimika utadhani mtu, kumbe nyamamwitu, tena hatari. Makazi ya sasa ya Masumbuko ni gerezani. Akitoka si kurejea nyumbani bali kwenda kaburini. Inasemekana hata akifa atazikwa hukohuko gerezani. Hivyo, yeye awe hai au mfu ni mfungwa milele! Huyo ndiye Masumbuko na masumbuko yake.

Masahibu ya familia ya Mzee Shida hayaishii hapa. Binti yake Aibu, kazi yake kuzaa watoto bila hata kujua baba zao nani! Yeye na kuku jike hawana mpaka wala hawachekani. Heri hata ya kuku maana kuku ni kuku kuliko Aibu binadamu kuzaa wanaharamu.

Hata hao jogoo wamzalishao anawajua mwenyewe au hata asiwajue maana ni mwingi kwelikweli.

Watu wengi hulaumu kubadilika kwa mfumo. Maana mabinti wa Mzee Shida hawakwenda unyagoni wakafundwa. Wangeendaje iwapo viongozi wa dini waliwaambia kuwa kufanya hivyo ni kumtumikia shetani wasijue ndiyo walikuwa wakimfungulia! Hii ilimwathiri hata dada yake Vishawishi.

Mdogo wao Hasara, kama jina lake, alikula hasara. Kwani alizikwa mwaka jana baada ya kuukwaa UKIMWI. Alikonda kama ng'onda kiasi cha kufa akiwa kilo mbili. Jamani, usiambiwe UKIMWI si mchezo.

Hasara alipata kibarua cha utingo kwenye gari la mizigo la mtoto wa Mzee Kupata. Alisafiri nchi zote za jirani. Huko ndiko alikoupata UKIMWI. Haijulikani aliupata nchi gani.

Watu wengine wanasema aliupata mgodini kijijini Githakwa alipokuwa akihangaika kabla ya kupata kibarua cha utingo.

Kama si UKIMWI kumkatili, alikuwa aibadili historia ya familia ya Mzee Shida. Maana alikuwa anacho kipato si haba. Hata hivyo, alipenda sana kutumia.

Inasemekana pesa yake nyingi alikuwa akiitengeneza kwa kuwavushia watu bidhaa za magendo mipakani. Alikuwa akijuana na maofisa wa mipakani waliokuwa wanamwamini na kumtumia.

Kwenye msiba wake wafanyabiashara wengi wa magendo walionekana kulia si kawaida. Hasa akina mama waliokuwa wakihangaika kuvuka mipaka kuchuuza vitu vidogo vya akina mama, kama vile vipodozi, mikorogo na nywele za bandia. Kutokana na kunogewa na maisha ya ujana, alikufa hata bila ya kuoa.

Alikufa mwezi mmoja na yule waziri wa wadudu, marehemu Kibina Kibeho, ambaye inasemekana alikufa kwa UKIMWI. Lakini, wakubwa

hulindana. Badala ya kutangaza alikufa kwa UKIMWI, walitangaza alikufa kwa shinikizo la damu. Wanaona aibu. Lakini, UKIMWI si aibu. Maana nao ni binadamu, hata wangejidanganya vipi ukubwa wao hauwafanyi wawe malaika.

Ng'ombe wa maskini hazai. Kwani alipokufa tajiri wake hata hakutoa ubani, achilia kulipa haki zake nyingine. Siku hizo matajri walikuwa wana uhuru wa kuajiri na kufukuza. Si kama siku hizi ambapo sheria ilimlinda mwajiriwa dhidi ya unyanyasaji na unyonyaji wa waajiri.

Historia ya familia ya Mzee Shida ni mazonge kama jimbo lao. Majaribu naye alihukumiwa kifungo cha miaka 75. Mbali na kushikwa na dawa za kulevya, alikuwa na makosa mengine ya ubakaji na ugomvi. Aliwahi kumtandika polisi kama mtoto mdogo. Walikuwa wakigombea mwanamke.

Inasemekana kuwa hakimu aliyemhukumu alitaka rushwa ya shilingi laki mbili ili amfunge kifungo kifupi lakini hakuwa na pesa hiyo. Hivyo, alifungwa kutokana na umaskini wake. Siku hizo hata ungeua, kama ungekuwa na pesa au kujulikana kwa wakubwa usingefungwa. Haki ilikuwa ikiuzwa sokoni kama karanga na dagaa! Ua mtu, fanya biashara ya mihadarati hata hujumu nchi, usingefungwa. Ungefungwaje na una pesa na mtandao wa kujuana serikalini?

Huwezi kuamini kuwa dume zima lilipitisha kete za dawa ya kulevya nyuma na kuyasheheni tumboni utadhani kiribatumbo! Kweli dunia imekwisha, tena vibaya.

Alipokuwa akirejea kutoka Pakistani alikamatwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Fikira na kuishia gerezani ambako yamegeuka makazi yake ya kudumu. Hata pasipoti yake aliyotumia kwendea India na Pakistani kutafuta unga bado imo kwenye mali zake alizoziacha.

Wenye pesa waliokuwa wakikamatwa walihonga na kuachiwa. Lakini, kutokana na Majaribu kutokuwa na pesa wala mtu wa kumpigania baada ya wazungu wa unga kumruka, ilibidi amwagiwe mvua zake 75! Siku zile rushwa ilikuwa imeiozesha nchi. Iliitafuna ikatafunika.

Biashara ya unga na ujambazi haitofautiani, kwani ukikamatwa wenzio wanakutosa ili wasijulikane wakaharibu biashara zao na heshima zao. Maana wengi wa wafanyabiashara hii na ujambazi ni watu wenye majina yao, tena hata wenye madaraka. Kuna kipindi waziri mmoja wa Mizengwe alinusurika kuumbuka uwanja wa ndege aliposachiwa na bahati yake siku hiyo hakuwa na mzigo. Ukiwaona wazungu wa unga mchana huwezi kuwadhania.

Pia, ilisemekana kuwa Majaribu aliwadhulumu maofisa wa uwanja wa ndege pesa yao. Kwani mara nyingi alikuwa akipita bila kugundulika kutokana na kuwapatia chao.

Baada ya kujiona amekubuhu aliamua kuwazima, nao wakaamua kumzima kabisa. Kwani miaka 75 na kifo havina mpaka wala tofauti.

6

Yupo huyu Maanguko. Kaanguka kama jina lake. Kwani tangu azaliwe licha ya kutojiweza kwa lolote kuanzia kibarua hata maisha, hakuwa amewahi kuoa. Hakuwahi hata kusingiziwa mtoto. Yeye na utu uzima wake ni sawa na mtoto. Hata mtoto ana afadhali maana akikua anaweza kuwa dume. Hujisikia kuwa majogoo yote uyaonayo yalikuwa ni mayai?

Wazazi wake walikwisha kukubali kuwa alikuwa mtoto si riziki. Japo inauma, ilibidi wakubaliane na ukweli kuliko kuukimbia ukweli usiokimbilika.

Funga kazi ni huyu Vishawishi. Licha ya kuwa gwiji wa kutoa mimba, yeye ni changudoa. Inasemekana huishi kwa kuhama nyumba kila wakati. Maana kila nyumba anayopanga kisipookotwa kichanga kwenye jalala kitaopolewa chooni. Amewahi kufikishwa polisi mara nyingi na kuachiwa baada ya kutoa kitu kidogo.

Huyu hata idadi ya mimba na vitoto alivyokwishavinyonga haijulikani. Maana kuvichomoa ni kama anakwenda msalani. Ajabu hana hata huruma navyo mradi anaponda maisha asijue yanamponda!

Yeye ni mwindaji hodari wa usiku. Asimwone mume wa mtu tena mwenye kuwa nazo na macho juu. Lazima atamwiba na kumpiga teke baadaye. Mwanamke hatosheki. Si Wazungu, si Wahindi hata wabeba mizigo bandarini. Anapoishiwa yeye ni zoazoa. Yeye alikuwa kalowea Fikira kwenye mitaa ya Sexon na Kinongo makaburini alikokuwa akifanyia uchafu wake huu usiku. Inasemekana wateja wake walikuwa ni hata watu wakubwa wenye madaraka ambao hakuna ambaye angetegemea wangefanya uchafu kama huu. Inasemekana huko mjini mambo yalikuwa yameharibika. Maana watu walifikia kufanyia ufuska hata makaburini. Kuna kipindi vyombo vya habari viliripoti kuwa padri mmoja alikamatwa na polisi kwa tuhuma ya kufanya tendo la ndoa na mwanafunzi wa shule huku mwingine akifungwa kwa kosa la kulawiti!

Yeye mwili wake aliugeuza duka. Alimuuzia kila mwenye rupia. Hakujali sura, harufu wala umri. Ukiwa na pesa twende kazini! Hata ungetaka amhudumie mbwa wako mradi pesa ya chapchapu ipo. Utu kwake ulikuwa ni msamiati usiokuwa na maana. Wazazi wake kawatia aibu si kidogo. Wanamwomba Mungu siku zote asije kuufanyia ufuska wake nyumbani kwao.

Mwaka jana baba yake alinusurika kifungo alipotaka kumchoma mkuki pale alipokuja na nguo nusu uchi zenye kuonyesha mapaja yote tena mbele ya baba yake, akiwa kabadili rangi yake kwa mikorogo na kuvalia nywele za maiti. Kalaaniwa mtoto yule!

Msafara bado haujaisha. Yupo huyu kitindamimba, mtoto wa mama. Huyu si mwingine ni Tujaribu. Yeye kazi yake vibarua kuanzia kuchinja kuku, kupiga zege hata kuchimba vyoo

Ni bingwa wa kuvuta bangi na kupigana. Haishi kuwekwa ndani. Hata polisi wanamjua. Mabwana jela nao wanamfahamu. Kwani ni kijelajela.

Hiyo ndiyo familia ya Mzee Shida na mkewe Mateso. Kama majina yao, Shida na Mateso licha ya kujaribu, kujaribiwa, kuteswa, kuanguka na maisha, bado walikuwa wakijikongoja wakitumaini ingetokea siku Mungu asiyebagua huenda angewakumbuka lau, kuyapunguza kama si kuyamaliza mateso yao duniani.

7

Kwa upande wa salamu maalumu kutoka Kanada, Matatizo licha ya kwenda shule na Mafanikio, mtoto wa Mzee Kupata,walikua pamoja kama watoto majirani wasiojua mipaka ya kupata na kukosa, utajiri na umaskini, usomi na ujinga, dini, kabila, rangi wala mbari.

Wakati ule wa utotoni Matatizo alikuwa hata akiingia kwenye jumba la Kupata. Kwa sasa hawezi kuingia kwa uhuru kama zamani, vinginevyo aitwe kusaidia kazi yoyote.

Isitoshe kutokana na tofauti ya kipato iliyopo, hata akiingia lazima familia ya Kupata haiwezi kumvamini kama alivyokuwa mtoto. Kwao kila maskini ni mwizi.

Walicheza wote na kuwinda vinyama vya kufikirika pamoja. Wakati wa makuzi yao hapakuwa na wanasesere na vinyago vingine kama vile vya magari hata majumba na michezo ya kompyuta.

Wakati ule watoto hawakuwa ndondocha wa kununuliwa vinyago na wanasesere yaani vitu vilivyoagizwa kutoka Ulaya. Watoto walijifunza uvumbuzi na utatuzi wa matatizo kwa kujitengenezea zana zao za kuchezea.

Wakati ule watoto walikuwa hawachungwi kama mbuzi. Walikuwa huru. Ila baada ya watu kugeuka wanyama, watoto ghafla walifungiwa ndani ya kuta, hasa wale wa mijini.

Wakati ule watoto walikuwa ni mafundi wa kutengeneza magari, nyumba hata ng'ombe. Hawakuisha kugombana na kupatana kama watoto wengine. Maana watoto ni kama vichaa, lakini malaika. Wanagombana leo kesho wako bega kwa bega kana kwamba hakuna lililotokea jana! Kweli utoto kichaa! Ndiyo maana walipokuwa wakipigana wazazi wao hawakusumbuka au kufarakana. Walijua ni utoto, wakikua wangeacha.

Licha ya kuwa rika moja, walikuwa marafiki wa kweli kabla dunia na hali ya kipato cha familia havijawatenganisha na kuwagawanya, vikimwelekeza kila mmoja kwenye dunia yake, tena tofauti kama mbingu na ardhi.

Walikatiana maembe bila kujali huyu ni mtoto wa tajiri na huyu maskini. Hawakuwa wakibaguana au kujali nani kapiga mswaki au la. Dunia wakati ule ilikuwa na thamani na utamu wa aina yake. Si kama iliyofuata ambapo dunia iligeuka gunia.

Watu huzaliwa huru na sawa lakini walimwengu huwageuza watwana na mabwana. Ila bado wote hufa na kuzikwa chini hata wawe na tofauti ya kipato. Hapa ndipo asili yao, yaani usawa hurejea na kuungana.

"Hakika dunia hii ni tambara bovu na wala si mbaya bali walimwengu." Alizoea kujisemea mzee Shida kila hali ilipomtatiza. Hali hii imekuwa ikiwasumbua Matatizo na Mafanikio hata katika ukubwa wao.

Urafiki wao wa utotoni, japo umevunjika, lakini bado haujavunjika na kutokomea kabisa. Bado vipande vya utu na ubinadamu asilia hujitokeza japo kwa kitambo.

Kila wanapojitahidi kuikimbia jana yao, huwafuata katika kesho yao kiasi cha vile vipande vidogovidogo vya utu na ubinadamu vilivyosalia huwavuta na kujikuta wakikumbukana hata kama ni mara moja kwa muhula.

Kwani hujawahi kusikia kuwa usiache mbachao kwa msaala upitiao? Kwani kiumbe duniani ni nini na nani hadi ajijengee madaraka na matabaka? Tulikotoka kumoja na tuendako kadhalika.

Pamoja na kuwapo pengo kubwa hata pazia kati ya vijana hawa wawili, silika ya utu huwavuta wakajikuta wakikaidi mipaka na mikatale bandia ya ibada za mali na vitu na lau kujuliana hali.

"Kweli mama! Mama kumbe Mafanikio pamoja na kuwa majuu bado ananikumbuka?" Matatizo alishangaa na kuuliza akiwa amebung'aa na

kuonyesha furaha yake juu ya salamu kutoka kwa rafiki yake wa utotoni. Pamoja na kuficha furaha yake, moyoni alikuwa na furaha kuliko hata hayo matone ya furaha yaliyoonekana usoni mwake.

"Kwa nini asikukumbuke. Hata kipato kiwatenge vipi nyinyi bado ni binadamu tu? Kinachowatenganisha ni mifumo hii michafu yenye uonevu na onevu ya binadamu. Lakini kwenye mifumo ya Mungu nyinyi mtakufa marafiki na ni marafiki tu." Alijibu Huzuni mama yake Matatizo.

Yule kuku na vifaranga vyake naye amerudi kuja kusikiliza maongezi ya mama na mwana.

Anajongelea karibu na ungo. Huzuni anamfukuza. "Mama kachokore kwingine, hapa hakuna wadudu wala mchele." Anaongea na kuku na kurejea maongezi na mwanawe.

Wakati akifukuza kuku Matatizo anaangalia zoezi zima akiwa na mawazo. Moyoni alikuwa anamwonea wivu yule kuku anavyofaidi utitiri wa vifaranga vyake.

Baada ya kuutafakari ujumbe huu muhimu, mara ghafla hasira ilimlipuka Matatizo kiasi cha kuitia nyongo furaha na heba aliyokuwa amepata kutokana na kupata salamu kutoka kwa rafiki yake wa utotoni.

Hali hii ilimfanya Matatizo awe njiapanda. Kwani hakujua kama amechukia au amefurahi. Kwa ndani alijihisi kama mjinga kiasi fulani.

Badiliko hili la ghafla halikumpiga chenga mama yake. Alijikuta akijibu "Usichanganyikiwe mwanangu. Dunia yetu ndivyo ilivyo. Wanadamu wameiharibu. Vitu vimeupindua utu na mtu kawa mtukitu na mtu asiye na kitu si mtu tena."

Alivutavuta kanga yake chakavu na kuifunga vizuri na kuendelea. "Huna haja ya kujitesa. Usijali kuna siku tutakuwa sawa kama si hapa, basi ahera. Hii minyororo tuliyofungwa ni ya muda. Tunaweza kuikata siku moja tukawa kama wao." Alisogeza ungo na kujipanga vizuri huku akimtupia

jicho kuku aliyekuwa yumo kazini kuwalisha vifaranga vyake.
"Mama wewe unangoja ahera! Mla mama kala leo kesho mama ya manani." Alijibu Matatizo.

Matatizo anaendelea, "Hebu mtazame huyu ndege mdogo anafurahi na watoto wake huku akifaidi ulinzi wetu."

Huzuni anaingilia bila kungoja mwanawe aendelee, "Mwanangu hilo nalijua sana. Ila kuna haja ya kuamini, kwani, ipo siku wote tutakufa kama tulivyozaliwa. Hakuna atakayeondoka na utajiri wake. Kila mtu ataondoka kama alivyokuja. Maana ukishakufa unabakia maiti."

Alisita kidogo ili kumeza mate na kuendelea, " Maiti iwe ya Rais, tajiri au maskini hata mzoga wa mnyama vyote sawa vimekufa. Kuku naye ana masahibu yake."

Alijikakamua kidogo na kuendelea, "Tajiri akifa huliliwa na maelfu. Lakini, kumbuka huwa hawamlilii yeye bali wanajililia kwa kukosa huduma yake. Hata maiti ya tajiri izikwe kwenye jeneza la bei mbaya ikiwa imevishwa suti na kutiwa manukato, mwisho wake itaoza sawa na maiti ya mbwa. Haya ndiyo maisha," Alizidi kusema Huzuni.

Huzuni alimkazia macho mwanawe Matatizo na kumalizia, "Mwanangu, maiti ni maiti hata iwe ya tajiri,mkubwa au maskini wote ni maiti hawana faida tena kwa wanaoendelea kuishi zaidi ya kuwafukia kuzimu." Aliwatupia wale kuku majani kidogo ambayo yalikuwa hayafai na kuendelea, "Hawa kuku, kumbuka tunawala baada ya kuwahudumia. Hawana utashi wala uhuru. Tofauti ni kwamba angalau tunawala baada ya kuwalisha na kuwalinda hata kama hatuwafugi kwa kuwapenda."

Kabla ya Matatizo kujibu, alijisemea moyoni, "Ama kweli binti wewe wa babu ulijaliwa akili. Kama si dunia kukuadhibu huenda ungekuwa daktari kama Dolly Kupata."

Ghafla Matatizo alikuta mama yake amemtumbulia macho asijue alikuwa akimjadili kimoyomoyo na kujibu. "Hivi mama, maiti ya mbweha na simba ni sawa?"

Mama yake hakungoja aongeze swali jingine. Alijibu ghafla, "Ndiyo. Zote zinaitwa maiti. Tofauti ni kwamba maiti ya mnyama huitwa mzoga. Haioshwi ingawa hubebwa sawa na ya mtu. Maiti kusema ukweli ni maiti bila kujali ni ya nani katika maisha."

Alinyamaza kidogo na kuendelea, "Hukumbuki marehemu mdogo wako alivyozikwa makaburi ya Mulago na waziri Kibina Kibeho?"

Inaonekana majibu haya ya mama yake yalimwingia Matatizo, Kwani alijibu kwa kuridhika, "Ahaaa!" alishusha pumzi kuonekana kukubaliana na busara za mama yake ambaye kwake alikuwa ni mama aliyejaliwa kipaji kikubwa, lakini dunia ikakipora.

Alipokuwa akitafakari majibu ya mama yake, mara ghafla utadhani mama yake alikuwa amegundua kuwa mwanawe alikuwa akisifia kichwa chake.

Aliandelea kusema, "Hata kiporo ni kiporo hata kiwe cha pilau au tunguja na mgagani bado ni kiporo. Mwisho wa kiporo siku zote ni kuvutia nzi na wadudu wengine wanyevuao. Hivyo, unautesa bure moyo wako kwa kuwaza kurudi nyuma. Amini, kuna siku haya yote yatakwisha kama ambavyo hayakuwapo. Haya ni mambo ya muda. Ni changamoto ya maisha na tafsiri ya maisha hakuna aijuaye."

Aliendelea, "Haya matabaka unayoyaona ni matokeo ya ufinyu na ujinga wa binadamu." Alijisogeza kwenye kivuli. Maana jua lilikuwa limesogea. Aliendelea, "Je, unajua kuwa kuna kipindi wanyama ni bora kuliko watu? Hawanyonyani wala kuuzana. Ajabu mbuzi anazaliwa hadi kufa hajapiga mswaki, lakini hanuki mdomo na wala kinywa chake hakisemi uongo." Aliweka uongo wake pembeni na kujinyoosha kidogo na kuendelea.

"Si unaona wale kuku. Wakimwona mwewe wanahamiana kwa kelele na hadhari. Lakini, siku hizi binadamu wanakuwadiana maadui. Hapa ndipo ubinadamu unaanza kuwa mbaya kuliko unyama na uhayawani."

Matatizo hakungoja mama yake amalize naye alijibu, "Mama nakuelewa.

Lakini, kubali kuwa viporo vinazidiana. Kiporo cha pilau ni cha pilau na cha mchunga mama ni cha mchunga. Maharage hugaga baada ya kuingia ubaridi lakini pilau mama huchukua muda." Alijibu Matatizo ambaye naye kama mama yake kama si nafasi yake ya kwenda sekondari kuuzwa, si haba alijaliwa kichwa.

"Hebu tuachane na mafumbo ya maisha. Nimekumbuka. Baba yako alikuwa analalamika panga lake limeisha makali. Hivyo ngoja nililete umnolee." Alisema Huzuni akiamka na kuweka uteo wake pembeni tayari kuelekea bandani kuleta panga la mumewe.

Alimkabidhi panga mwanawe na kuendelea na maongezi.

"Panga hili linaonekana limeanza kuchoka. Hapa baba lazima atoboke mfuko kununua lingine. Nayo yamepanda bei siku hizi" Alilalamika Matatizo.

"Yatashindwaje kupanda bei iwapo serikali nayo imepandisha ushuru huku wafanyabiashara wakitumia nafasi hiyo kutukata mikono, nani anajali?" Alilalamika Huzuni kujibu kilio cha mwanawe juu ya bei ya mapanga.

Mama na mwana waliongea kwa mafumbo, misemo na nahau utadhani watu wazima sana. Kiasi fulani walijiliwaza na kujipa moyo kuwa kesho yake ingeweza kubadilika kama wataamua kupambana.

Pamoja na kuridhishana kimantiki, ukweli ulibakia palepale kila mmoja moyoni mwake kuwa umaskini hata uwe wa kusababishiwa ni mbaya hata kuliko baadhi ya maradhi. Mafua na kikohozi husumbua, lakini hayaumbui wala kusumbua kama umaskini. Magonjwa haya huwa hayamzuii mtu kuhangaika kama umaskini umfanyiavyo mtu.

Umaskini mara nyingine huwa kama pingu. Humfunga mwenye kuwa nao kiasi cha kufinya dunia ikaonekana kama chumba kidogo cha mahabusu. Uzuri wa familia ya Mzee Shida, umaskini bado haujapanda kichwani kiasi cha kukata tamaa au kuridhika nao.

Maana watu wengi waliopandwa na umaskini vichwani, huwa kila balaa

wanamtupia Mungu utadhani ni kweli.
Wakati Matatizo anajiandaa kuuliza maswali mengine, mama yake alikumbuka kuwa alikuwa hajatwanga kisamvu kwa ajili ya mlo wa jioni. Maana ule mchicha aliokuwa akiuchambua ulikuwa ni chakula cha mchana.

Huzuni akiashiria kuvunja kikao alisema, "Matatizo, hungoji angalau ule ndiyo uende uendako!"

Matatizo alijibu, "Mama nawe, yaani mchicha wenyewe haujainjikwa hata mekoni ningoje hicho chakula kitaiva lini? Ingekuwa nyama ningengoja hata siku nzima."

"Mwanangu we, enzi za nyama zilikwisha zamani. Nani ataweza kuikwea bei ya nyama?" Alitabasamu na kuendelea, "Nyama ni ya akina Kupata. Yetu sisi majani kama mbuzi."

"Usijali siku Mkweo akijifungua nitawachinjia kuku." Alitania Matatizo.

"Hiyo itakuwa ya mzazi. Isitoshe kuku huyo mdogo ataweza kumaliza hamu ya nyama niliyo nayo?" Alizidi kutania Huzuni.

Walicheka angalau kwa kujiridhisha. Maana maisha ndivyo yalivyo. Hata kama kuna dhiki kiasi gani ukifika wakati wa kucheka mja atacheka. Hata awe na raha kiasi gani,ukifika wakati wa huzuni mja atahuzunika tu.

Hivyo waliachana kila mtu akaenda kwenye mihangaiko yake.

8

Matatizo aliendelea kuwaza kwa kitambo kidogo na baadaye naye kutimkia alikokujua.

Aliondoka akiulaumu mfumo mzima wa utawala wa Mizengwe, kwani alikuwa akisonya na wakati mwingine kutukana, utadhani kuna mtu alikuwa akimsikiliza!

Alipofika chini ya banda la baba yake alijisemeza, "Hata watunyonye vipi ipo siku watakufa na kufukiwa, wakiacha mali zao zikiliwa na wengine. Lakini, kwa nini kungoja wafe wakati hakuna ajuaye watakufa lini?"

Hapo ndipo ulipo mzizi wa chuki ya Matatizo kwa serikali ya Mizengwe. Huwa anaitwisha lawama kwa yote yaliyomsibu maishani. Huwa anasema hataisamehe hata siku moja. Huwa anasema msamaha anaoweza kutoa kwa serikali ya Mizengwe ni kuiangusha. Hana simile na hali ilivyo na hapendi kumsukumia lawama Mungu.

Uchungu wake huzidi apatapo magazeti kutoka mjini yakielezea wizi wa pesa nyingi na uchafu mwingine. Hutamani ageuke kimbunga aende akaibomoe na kuwaokoa wenzake wote wanaoteseka kama yeye mikononi mwa serikali ile ya Mizengwe.

Akiangalia kijiji chao kilivyosahaulika kimaendeleo na kutumika kama shamba la wajanja wachache, hutamani kuikimbia nchi. Alijaribu mara nyingi kuzamia meli akakamatwa na kurudishwa kuishia kutumikia kifungo.

Ameamua kukaa kijijini kwao na kuwaza jinsi ya kujikomboa. Japo watu wa kijijini ni wagumu kujiamini. Anao marafiki wachache walioona mwanga.

Miaka imepita tangu Matatizo apokee salamu kutoka kwa rafiki yake wa utotoni Mafanikio. Anaendelea na maisha kama wanakijiji wengine akisubiria kusikia kutoka kwa rafiki yake. Leo amemuwaza sana rafiki yake huyo.

Matatizo ndiyo katoka zake porini kukagua miti ya kukata mbao usiku. Maana wao hawaruhusiwi kukata mbao. Wanaoruhusiwa ni wale wanaopewa leseni na serikali au vibali vya magendo kutoka kwa Ofisa Misitu wa kijiji ambaye pesa zote huishia tumboni mwake.

Hapa ni kama kuna mashindano kati ya serikali na wananchi na Ofisa Misitu. Wakimzidi ujanja wanaingia usiku wanakata magogo yao na kuyaficha au kuyasafirisha usiku huohuo au kuwauzia matajiri wa pale waliokuwa wakiyanunua kwa bei ndogo na kuyasafirisha nje ili kuyauza kwa bei mbaya.

Yaani, kinachofanyika hapa ni sawa na mtu anakwenda kuhenyekea vijisenti kwenye kibarua ili ampelekee mkewe. Baada ya kumkabidhi mama hivyo vijisenti ulivyohenyekea, kesho unaviiba au kuvikwapua! Yaani, ni kwamba kinachoendelea Mizengwe kwa watu maskini na hata serikali ni kuiibia ili kuteseka baadaye.

Matatizo anaingia ndani na kwenda moja kwa moja chumba cha kulala ili kujipumzisha kwenye kitanda chake cha kamba.

Mateso, mke wake, naye hamsumbui. Anajua mumewe amechoka. Yeye anaendelea kuguguna dongo lake.

Hakupenda kumsemesha mume wake. Maana kama angehitaji hili angeanza angalau kwa kutoa salamu. Siku zote mke na mume wanajuana tabia. Maana ndoa mara nyingi ni kama taasisi ya vichaa. Kichaa kikilingana furaha. Kikizidiana karaha.

Isitoshe watu maskini huwa mara zote wana hasira. Hivyo, mke wa Mateso alimwacha mwenzie ajipumzikie.

Mateso ana kila dalili za kukaribia kujifungua. Amechoka sana na siku hizi anachagua vyakula. Shingo yake kwa nyuma imetuna kama kitoto kinachonyonya vya kutosha. Hata rangi yake usoni inaonyesha kuiva. Imepita miezi saba tangu ianze hali hii. Sasa si siri tena. Tumbo linasema ukweli wote.

Juzi alikosana na vijana wa pale kwa fundi seremala walıposema eti mumewe kamuwaisha. "Vijana wa siku hizi hawana hata adabu, wanaweza kuparamia na kusema lolote." Alijisemea.

"Lakini, wajinga wengi wanasema hayo ndiyo maendeleo na kwenda na wakati! Maendeleo yenyewe ni vijana kuigiza mambo ya kipumbavu, wasijue hatima ya maisha yao! Hili halikuwashughulisha vijana hawa. Maana ujana siku zote ni maji ya moto, yakipoa watajua." Mateso alijisemea moyoni na kuamua kuachana nao na kupita.

"Aliendelea kuhoji kutokuwa na fahamu kwa vijana wale wahuni kuzikabili changamoto zao zaidi ya kuishi kwa kukidhi njaa za matumbo yao!" Alizidi kujisemea moyoni.

Sambamba naye, Tonga mke wa Heri naye kadhalika. Mimba hıi ilimfanya ampende Mateso. Kama si daktari kumshauri asipande ndege au kufanya safari ndefu, angekuwa Fikira akijichana vinono vya mjini.

Tonga ana bahati. Hasengenywi na vijana wa kwa fundi seremala. Mume wake licha ya kuwa tajiri ni mbunge. Wangemchokoza wangeishia gerezani. Maana wakubwa wa Mizengwe siku zote ni kama miungu-watu.

Hali hii ilimlazimu kuuguzia tumbo lake Githakwa. Hii ilikuwa kama bahati kwa Mateso. Kwani alimpenda kiasi cha kutaka waonane mara kwa mara. Kweli, ujauzito kiboko. Maana kabla ya hali hiyo, pamoja na kwamba walikuwa majirani, Tonga hakuwa na muda na Mateso. Kwani yeye ni maskini na wao ni matajiri.

Kama ada,tatizo ni kwamba Mateso hakuwa na uwanja mpana wa kuchagua vyakula. Pia, alikuwa akimchukia shemeji yake Tujaribu ambaye kabla

ya ujauzito alikuwa ndiye rafiki yake na mtani wake mkuu! Kila akirudi kutoka zake kwenye vibarua au mihangaiko yake alikuwa hakosi zawadi kwa shemejie. Mara leo kaja na makanyagio. Kesho vipapatio. Mradi raha tu. "Kweli, ujauzito sikia usiambiwe raha na karaha zake," Alikuwa akijisemea Mateso mara nyingi.

Kila mara akitematema mate ovyo. Ila si haba. Kwani alikuwa mng'avu utadhani akipaka mkorogo. Shingo nayo ilikuwa inatuna utadhani alikuwa anakula vizuri kama jirani yake Tonga ambaye alikuwa amekonda baada ya kuwa mjamzito!

Alikonda utadhani ana UKIMWI! Wakati mwenzie Mateso nguo zilikuwa zikimbana bila ya kuwa na ya kubadilisha, Tonga zilimpwaya na shukuru Mungu mumewe alikuwa anazo, angeweza kununua nguo yoyote ya bei yoyote. Mateso alifikiria kumwomba nguo moja lakini aliogopa akikataa ingekuwa aibu. Isitoshe mumewe king'ang'anizi asingekubali afanye hivyo. Ni maskini jeuri. Kwake kuvaa mtumba wa mzungu aliyekufa ulaya ambaye hamjui ilikuwa bora kuliko wa yule anayeishi kwa kumwibia yeye.

Ukiachia mabadiliko hayo, Mateso alikuwa kageuka mbuzi. Kwani aliuguguna udongo utadhani mnyoo! Yeye na udongo, udongo na yeye.

Yeye Tonga yake ilikuwa kutapika. Alipenda vitu viwili tu. Alipenda sana miwa na udongo ingawa alikuwa akila japo si sana.

Kwa upande mwingine, mimba ya Tonga ilimfanya mumewe angalau kutulia kitambo kwenye jimbo lake. Maana kama si kuwa karibu kumhudumia mkewe aliyezuiliwa na daktari kusafiri, angekuwa zake mjini kwenye dili na biashara zake. Maana watawala wa Mizengwe na wafanyabiashara hawana mpaka.

Siasa za Mizengwe ni biashara inayolipa sana. Maana hakuna wa kukuuliza. Kila mtu anajihomolea kwa nafasi mahali alipo. Ila wananchi walio wengi wanateketea kwenye mchezo huu wa tamaa. Maana si viongozi wa serikali wala dini wanaowatetea wala kuwajali. Wamewafunga mikanda na kuwatwisha misalaba na kila aina ya uozo huku wao wakitumbua maisha.

9

Juzijuzi Mateso alikosana na mumewe akitaka amnunulie utumbo na mapupu! Ama kweli mimba kishawishi. Kwani badala ya kutamani salala,figo na maini yeye anatamani utumbo na mapupu! Mungu hujua kumlinda mjawe. Angetamani vinono hivyo si angemtoa roho mumewe hata naye kutoa mimba kabla ya wakati wake!

Maskini mumewe,hakuwa hata na chapa mfukoni. Wacha ahangaike na kuhangaika. Hali hii ilimletea mtafaruko si kawaida.

Pia, Mateso si mpenzi wa makande. Lakini, siku hizi anayabugia utadhani bungua mdudu apendaye maharage na mahindi utadhani anajua kulishika jembe!

Kwa vile Matatizo anajua matatizo ya mkewe, hana tatizo. Amekubali kuyalimbika na kuyapokea yote. Analaumiwa hata mahali pasipostahili. Lakini, afanyeje! Huo ndiyo ukubwa na ukubwa siku zote ni jaa. Huu kweli ndiyo ukubwa. Kwani Mateso alikuja peke yake na sasa karibuni ataongezeka mwingine!

Mbali na madai ya utumbo na mapupu, kulikuwa na tatizo jingine. Matatizo kama jina lake nayo yanaalikana. Kwani gauni la Mateso sasa lilikuwa linambana. Haya nayo ni mateso mengine.

Kwani inabidi kichwa kizungushwe ili kununua jipya kwa ajili ya ujauzito. Pia, vinatakiwa vikorokoro vya kichanga. Uzuri Waafrika huzuia kukata mbeleko kabla hujamwona kichanga. Hivyo, hili hata kama hajaanza kulikamilisha bado lipo mlangoni likimtumbulia macho!

Matatizo hawezi kulala sana. Alijitupa kwa muda kugaragara na kuamka na kurudi kujiunga na mkewe.

Katika kulikabili hili Matatizo anajisemea kimoyomoyo huku kijasho chembamba kikimchuruzika, "Kweli mwaka huu nimeumbuka. Walionishauri kuoa siwaoni kuja kunichangia lau nipambane na mahitaji haya! Wao lao ilikuwa ni kuchangia harusi kunywa kula na kuserebuka. Sasa yaliyobaki yangu, wao hawamo."

Alizidi kujipa moyo, "Hata hivyo nawalaumu bure. Kwani mke wao au wangu?" Anachekea moyoni kwa kujiuliza na kujijibu hata kujisuta.

Kwa kumbukumbu ni kwamba gauni alilovaa Mateso aliliopoa kwenye kafa-Ulaya-mazishi Afrika. Kwa wasiojua hili ni mtumba au nguo iliyoingizwa kwenye nchi inayolima pamba kwa wingi lakini watu wake wanavaa mitumba,wanaendesha magari ya mitumba na wengine husema kuwa wanafikiri kimitumbamitumba. Viongozi nao wana akili-mitumba waliyoipata walipokwenda kusoma ulaya! Hayo ni ya wanasiasa.

Alipoopoa gauni hili alikuwa bado yu mwembamba kabla hajala na kushiba. Sasa linambana kwelikweli. Alikuwa ki-potabo na bonge ya toto wakati ule akimeta na kuvutia kama sarafu ya kwenje.

Sasa tumbo ndiyo hilo linazidi kuumka, utadhani kameza hamira. Mateso kweli anahitaji nguo mpya. Lakini, pesa yenyewe kichere na saa nyingine mfukoni hakuna!

Sasa Matatizo atakopa kwa nani iwapo ameishagonga milango yote ya marafiki,jamaa na majirani? Hili ndilo swali linalotaka jibu sahihi tena kwa wakati sahihi.

Nyonyo alizokuwa kavuna kiasi alikuwa kalanguliwa na walanguzi walio kuwa wamehalalishwa na serikali huku kidogo kilichobaki kikikopwa na serikali hiyohiyo. Hategemei kulipwa mpaka msimu ujao! Nani anajali?

Mbao alizomuuzia mhindi kwa mkopo hategemei kulipwa karibuni. Maana walikubaliana kuwa mhindi aende auze, akirudi kuchukua mzigo mwingine ndiyo amlipe.

Wakati Matatizo na Mateso wakiteseka kwenye shida yule Kitumbotumbo anayepima mazao yao anazidi kuwa na kiribatumbo.

Wasomi husema ana kiribatumbo au kitambi. Ana kitambi kisichokuwa na tambi. Kitambi chenyewe ni cha kula bila mpangilio kwa vile pesa anayokula haitokani na jasho lake. Anawaka utadhani malkia wa mchwa! Yote juu ya nini? Jasho la wakulima wa vijijini ambao kama kondoo huliwa wakijiona hata wasilalamike! Wangemlilia nani iwapo walishasahaulika na waliopaswa kuwasikiliza walikuwa wakipata chao cha juu?

Wakati mahitaji na madai ya Mateso yakiongezeka, banda lao la mbavu za mbwa linayo madai yake. Kwanza linavuja. Kulikuwa na uvumi kuwa serikali ina mpango wa kuvunja mabanda yote yaliyojengwa karibu na barabara ili kupisha barabara iendayo kwenye machimbo ya vito yaliyoko jirani. Siku ya kufa kwa nyani miti yote huteleza.

Wengine walikuwa wanasema kijiji kizima kingevunjwa kupisha upanuzi wa mgodi. Matatizo ameamua kuyapuuzia yote maana watu wa vijijini huzua mambo! Kila mtu na redio mbao yake anazua lake mradi siku ziende. Ujinga kweli ni mzigo. Yote haya yanasababishwa na ujinga na umaskini.

Machimbo haya yanamilikiwa na wageni waitwao wawekezaji. Yamekuwa chanzo kizuri cha uchafuzi wa Mto Chania ambao ndiyo chemichemi ikatayo kiu ya wanakijiji wa Githakwa.

Wanakijiji wamelalamika hadi wamechoka. Kila wakilalamikia uchafuzi huu wa mazingira wanaambiwa mwekezaji analipa kodi nono kwa serikali!

Sasa wanakijiji wanaona kama serikali imeamua kujali kodi badala ya afya zao. "Penye udhia penyeza rupia." Wahenga walisema.

Wakati serikali ikila vinono vya muwekezaji, wanakijiji wanakula chungu ya madhara ya biashara yake ya uchimbaji madini! Nani anajali iwapo hata mbunge wao anafaidi na maji safi ya bomba mjini? Isitoshe yeye

hategemei maji machafu ya vijito. Ana matanki na kisima chake. Hivyo matatizo yao si yake japo ni wajibu wake.

Nani anajali iwapo serikali inapata chake? Hata Msitu wa Kololo unaanza kuteketea. Maana wakata magogo walioruhusiwa na serikali hawasikii la muadhini wala mchota maji msikitini. Hakika wanakijiji wanapoteza imani kwa serikali yao. Maana kila tatizo linasukumwa kijijini.

Kwa upande mwingine, serikali nayo ina imani kuwa wanakijiji hawawezi kuipinga, ingawa ni dhana potovu. Maana na wanakijiji ni watu. Isitoshe hata hao wenye madaraka wanaojidanganya hivyo walitokea hukohuko. "Nyani haoni makalio yake." Alizoea kujisemea Ndirangu.

Kila alipolewa na kushauriwa aachane na ulevi alizoea kujibu kuwa kama angeacha ulevi angekufa kwa ugonjwa wa hasira kutokana na alivyokuwa akiteswa na maisha.

Kila alipolewa alizidi kuwalaumu wananchi kwa kukubali kuwa kondoo. Alikuwa na msemo wake maarufu uliojulikana kama, "Siku tutakapowatolea uvivu watahama nchi hii."

Alikuwa akisema eti Wanagithakwa walikuwa wavivu wa kufikiri na waoga wa kuamua na kutenda.

Mwanzoni watu walikuwa wakimchukia. Lakini, baada ya kumzoea walimpuuza. Wapo waliomjadili kuwa alikuwa akisema ukweli na wengine walimchukulia kama mlevi na kichaa.

Lakini, cha ajabu alikuwa rafiki mkubwa wa Mzee Njema. Huyu ukiachia watoto wa Mzee Njema na watu wachache, ndiye alikuwa akiongea, tena kwa muda mrefu na Mzee Njema.

Walikuwa wakijiona kama wasomi pale kijijini, kwani Mzee Njema alisoma wakati wa mkoloni japo hakufanya mtihani wake wa 'Cambridge'. Juzi serikali ilifukuza wazururaji na vibaka. Ajabu iliwafukuzia vijijini! Wanakijiji wanaona kama serikali inaona kuwa kwao ndiyo sehemu ya

kulimbikizia matatizo yote ya Mizengwe.

Vijana wa Githakwa waliofukuzwa mjini waliporejea, mlevi maarufu Githakwa kama ajulikanavyo, Ndirangu, aliwatania na kuwadhihaki kwa kusema kuwa walikuwa wamezidi kwenda mjini kuwabana wakubwa na kuwasababishia msongamano barabarani wasifaidi mashangingi yao na kuwabughudhi wenye pesa na madaraka ili kukimbia kelele zake.

Alizoea kusema kuwa mwenye pesa amalizapo kumnyonya maskini huwona kama kinyaa. Hivyo huwa hapendi kumwona pale amalizapo haja zake naye!

10

Juzi Mateso alikwenda kwenye ile asasi isiyo ya serikali ambayo walitangaziwa kuwa ina mitumba ya kuwasaidia akina mama.

Ajabu alipowaeleza tatizo lake alionyeshwa chumba kilichojaa mitumba chakavu isiyofaa kwa matumizi! Kumbe kila kitu kimeharibika. Maana kila mitumba ikiletwa wahusika huchagua iliyo safi na kuwapa wauza mitumba wawauzie!

Kilichomkera ni kuambiwa atie saini yake kuwa amehudumiwa. Kumbe wenzake wanataka wamtumie kuwaridhisha wafadhili wao. Hasaini. Anaamua heri kufa kwa heshima akiwa na matatizo kuliko mbwa akiwa hana tatizo isipokuwa fedheha. Aliudhika na kushangaa sana. Yaani, kuingia kwenye chumba chenye madaso na manyang'unyang'u ndiyo asainishwe kana kwamba alikuwa amepata alichokitaka!

Anaichukia ile asasi isiyo ya serikali maana inawatumia wanakijiji kujipatia ulaji kutoka kwa wafadhili walioko Ulaya. "Halafu inasemekana asasi hii ina uhusiano na ile ya mke wa Mkuu wa Mkoa. Siku hizi asasi zisizo za serikali ni kama vyama vya kisiasa, zimekuwa biashara inayoingiza mamilioni ya pesa hapa Mizengwe." Alijisemea na kuendelea, "Hujasikia wake wa wakubwa wanavyoshindana kuzianzisha? Kuna za UKIMWI, unyumba, watoto,wadudu, bado ya ndege ndiyo sijaisikia wala ya wanakijiji wanaodhulumiwa na watawala! AZISE zinazolipa pamoja na dini mpya, vyote vimejichimbia mijini kwenye mapesa ya kuchota na washamba wengi." Alisemea moyoni kana kwamba alikuwa na mtu aliyekuwa akimsikiliza!

Kinachomuumiza sana Mateso hata mumewe ni ile hali ya kifunguamimba wao kukaribia kuzaliwa kwenye taabu kama Yesu wa Nazareti. Heri hata ya Yesu kwani wazazi wake walikuwa na pesa ya kulipia Nyumba ya Wageni kama si vyumba kuisha.

Matatizo, mumewe yeye hana pesa. Hana hata jinsi ya kuipata hiyo pesa ya kumwandalia kifungua mimba wake! Ama kweli hujafa hujaumbika na siku uliyovaa vibaya ndiyo unakutana na mama mkwe.

Wakati Mateso akiwaza na kuwazua hayo, Matatizo naye ana yake kichwani mwake. Kichwa kinamuuma. Atauweka wapi ugeni wa kichanga kinachotarajiwa? Hili ni swali ambalo lazima lipatiwe jibu mujarabu tena haraka.

Kinachoumiza zaidi ni je, mama mkwe mzaa chema, anyeshewe na kuvujiwa kwenye ubavu wa mbwa ambao ndilo banda lake? "Aibu" Bila hata kutarajia, Matatizo anajikuta akijibu utadhani alikuwa akiongea na mtu asijue ni mahojiano ya ndani kwa ndani ya moyo wake!

Huku mke yupo anaongea na nafsi yake na huku mume kadhalika!

"Mume ni mume ingawa gumegume anayo sifa ya mtume." Anazidi kujipa moyo. Anajipa matumaini kama mbwa akaliaye mkia wake na kujidhania yuko kwenye sofa ya tajiri wake. "Lazima nipambane." Anazidi kujipa moyo. "Lazima nishinde na ni mimi huyuhuyu." Anazidi kujipa matumaini.

Kinachozidi kumsononesha ni kwamba hata mkewe ana wasiwasi na hali hii ya ukata. Kitendo cha mkewe kuhangaishwa na hali hii kinamzidishia wasiwasi kuwa huenda kinaweza kuathiri ujauzito wake.

Atapataje usingizi iwapo hata hayo maisha ya kawaida bila ya ujauzito ni kijungujiko? Mara anajisemea tena, "Maisha ni sawa na kaburi, sharti uingie mwenyewe. Akipatikana wa kukusaidia ni kulichimba na kukuingiza ili uonje adhabu yake." Anazidi kuukubali ukweli ulioko mbele yake.

Wakati Matatizo akijihoji na kujijibu, Mateso alikuwa kimya akibwia dongo lake. Tangu apate tumbo ni mgugunaji mzuri wa udongo. Kiasi fulani asingejua kilichokuwa kinaendelea kichwani mwa mumewe. Kwani licha ya kuushughulikia udongo wake, naye alikuwa na mawazo yake moyoni.

Alikuwa akiomba Mungu mumewe aende kwenye mihangaiko yake ili

atoroke aende kwa shoga yake mpya Tonga ambaye ujauzito umemfanya ampende japo kabla alikuwa hana muda naye. Maana wao ni matajiri na isitoshe ni mke wa mbunge wakati Mateso ni mke wa kabwela.

Mara ghafla alishtuliwa na sauti ya Matatizo aliyejisemea, "Mbona dunia hii haina huruma wala mizani ya haki hata kidogo!"

Alitikisa kichwa na kuendelea."Wakati mimi na mke wangu tunahangaika tusijue kichanga chetu kitafikia wapi,kuna watu tena wanaojiita wenzetu wanatapanya pesa yetu ya kodi tunayolipa kwa kujidhiki!"

Mateso alikubaliana na mumewe, "Hawa si wenzetu. Wangekuwa wenzetu wangefanana nasi. Pia, wangejua shida zetu tungejua maisha yao." Alitema mate na kuendelea, "Maisha yao ni siri."

"Nakubaliana nawe mke wangu. Huwaoni wanavyojificha nyuma ya magari yenye kiza huku ofisini mwao wakifichwa na makatibu muhtasi. Maana nasikia akina Mzee Njema walikwenda wilayani kumpelekea matatizo juu ya uchafuzi wa mazingira, ukataji miti na utoroshaji wa vito na magogo wakafukuzwa na Katibu Muhtasi wa mbunge." Matatizo aliongezea.

"Hata Shoga yangu Tonga ana wasiwasi na Katibu Muhtasi huyu asije akafanya uhtasi ukaisha kumletea uasi. Si unajua tena wanaume hamwaminiki" Alisimulia Mateso.

Baada ya kuguguna dongo lake aliongezea, "Hukumbuki yule mwanamuziki wa enzi zile nchi ilipokuwa na wanamuziki, si hawa wanamuziki? Aliimba: naepuka vigeugeu, enyi wanaume ahadi hamna?" Alisema Mateso huku akivuta hisia za muziki ule.

"Sasa mama unakokwenda kubaya. Kumbe hata nami huniamini? "Aliuliza Matatizo kwa hasira.

"Mume wangu, kwani wewe una huyo muhtasi? Wewe una Mateso na Mateso ana wewe. Wewe si mwanamume, ni mume wangu." Alijitetea Mateso.
"Mwanamke umejaliwa raghba sina mfano! Ukweli ni kwamba wanawake

hamumwamini mwanamme kadhalika na wanaume wengi hawawaamini wanawake isipokuwa mimi nakuamini wewe hata kama unakera." Alitania Matatizo.

"Unasemaje? Ninakera! Kuna kiumbe duniani anakera kama wewe? Kama yupo basi ni serikali hii." Alijitetea Mateso huku akiguguna dongo lake.

"Kweli mke wangu umejua kunitenda! Yaani, mimi nakera kuliko hata serikali ya Mizengwe! Ama kweli akuchaguliaye tusi hakutukani." Alijibu mapigo Matatizo.

Kwa kiasi fulani maneno haya yalimliwaza Matatizo, akajua kuwa kumbe yu mtu wa pekee na kuna mtu anayemchukulia hivyo.

Matatizo hakutaka mjadala wa kijinsi. Aliamua kupuuzia kila kitu na kurejea kwenye mada waliyokuwa nayo kabla mke wake hajamchokoza kwa kushambulia wanaume. Maana anamfahamu mkewe. Akiamua kushikilia jambo huwa haliachii na isitoshe akiongezea na ujauzito ndiyo basi.

"Mke wangu ungesoma! Ama kweli kama si kuwa Rais wa kwanza mwanamke wa nchi hii basi ungekuwa Waziri Mkuu." Alitania Matatizo.

"Inaonekana huyo atakayezaliwa atakuwa mwanasiasa. Maana huwa unachukia siasa. Lakini, tangu upate ujauzito huu unapenda sana siasa." Alitania Matatizo.

"Hizo ni ndoto. Sisi tuliozaliwa wakati mbaya na nafasi zetu kununuliwa na matajiri hatutanyanyuliwa na mfumo huu uliotukalia" Alitema mate na kuendelea, "Na isitoshe siasa za nchi hii zimeanza kugeuzwa za kifalmefalme. Huoni watoto wa wanasiasa wanavyokwea nafasi za kisiasa kwa kasi ya ajabu?"

Alimega dongo lake tena na kuendelea, "Na huyu ataathiriwa na huu utandawizi,uwekezaji na ugenishaji maana kila kitu tulichochuma zamani sasa kinapigwa mnada na wakubwa wachache wanachukua chao. Hiyo

elimu ya bure itapatikana wapi?"

"Mwenzangu ulijaliwa kichwa lakini dunia ilikipora maana una ubongo unaochemka kama tanuri." Alizidi Matatizo kumsifia mkewe ambaye ni kweli ubongo wake kama si kufungwa na vibanzi na minyororo ya dunia haukuwa wa kawaida.

Mateso alitabasamu tu huku akiendelea na dongo lake akimsikiliza Matatizo akimmwagia sifa. Lakini, ni kweli Mateso hata Matatizo ni watu waliokuwa na vichwa vinavyochemka ambavyo vilizimwa na umaskini wa koo zao.

Alinyamaza kidogo na kuendelea, "Hawa watu tusipotafuta jinsi ya kuwabana watazidi kutuua kwa matatizo tena kwa mtaji wetu wenyewe. Wanamkaanga samaki kwa mafuta yake." Alijikakamua kidogo kuondoa kohozi lililokuwa limemkwama kooni na kuendelea, "Si unaona familia ya Ssebagala ilivyobadilika ghafla baada ya Heri kuanza kufanya uhawara na Cecilia binti wa Ssebagala. Amemwanzishia biashara ya duka, mradi wa kuku wa mayai wa kisasa ambao mayai yao yanasemekana yana sumu na kumnunulia gari wilayani. Taratibu familia inaanza kuuaga umaskini."

Kabla ya kuendelea Mateso aliingilia kati, "Hao mume wangu hatuwawezi. Huoni jinsi vizalia vyao waliotusaliti kwa wazungu vinavyoishi kizungu wakati sisi tukiishi kama vinyamamwitu?"

Alibwia dongo na kuendelea bila kungoja mumewe ajibu. "Hebu mwone mzee Kupata na wanawe na biashara zao haramu. Kama si baba yake na yeye na sasa mwanae kutusaliti na kuwa boi wa mzungu angekuwa na ukwasi huo alio nao?"

Walimaliza maongezi yao na kuhamia nje mbali kidogo chini ya mti wa mkungu. Baada ya kufika kwenye mkungu waliendelea na maongezi yao ambayo hayakuwa rasmi.

Baadaye maongezi yao yalikuwa yakikatishwakatishwa na miziki ya ndege waliokuwa nao wametoka walikotoka kwenda kwenye mti kufanya sherehe zao za kukaribisha kiangazi. Mateso alianza kujiimbia wimbo

wake aupendao:

Kilio, kilio, kilio kimetufika.
Walio, walio, walio wetu wametuuza.
Hakika wametuchuuza, chuuza kama dagaa.
Vipofu, vipofu, vipofu wasio na macho.
Kwani wameishatuuza na wao wamejiuza.
Wameuza mali zetu
Wameuza utu wetu
Hata makaburi yetu
Wameuza roho zetu
Wameuza kila kitu
Wanauza miili yetu
Imeshuka thamani yetu.
Hawa ni adui zetu.

Aliendelea kughani bila mume wake kuingilia kwa kitambo. Mwishowe Matatizo alimsifia mkewe. "Kweli umejaliwa sauti kama ninga! Laiti kungalikuwa bado na bendi za muziki hata taarabu ningalikutafutia bendi." Mateso aligeuka na kumwangalia tu. Matatizo aliendelea, "Mie tangu muziki ufe uje huu utapeli wa kupiga kelele watu wakasema ni muziki unadhani nina hamu tena na muziki?"

Mateso alianza tena kuimba bila hata kujali kama mumewe alikuwa akisikiliza.

Wakati akimsikiliza mkewe, Matatizo alionekana kama mwenye kushtuliwa na jambo fulani.

Alikuwa akijipapasa mifukoni kana kwamba amevamiwa na siafu. Ghafla alijisemea, "Hii pesa imedondokea wapi? Nilikuwa na kwenje mia mbili humu." Alizidi kujisakanya zaidi na zaidi kuisaka hiyo sarafu ya kwenje mia mbili. Kwenje ni sarafu ya Mizengwe. Kwenje elfu moja na mia tatu ni sawa na dola moja ya Kimarekani.

11

Wakati Matatizo akijisanyasanya na Mateso akiutesa udongo, ndege aina ya kichungi walikuwa ndiyo wamehanikiza na kelele, wakiimba na kuvuta sigara zao na kushangilia jambo fulani walilolijua wenyewe. Inawezekana walikuwa na harusi, maana kuna ndege kama wawili waliokuwa wamezungukwa. Hawa huenda walikuwa ndio wanawali au mabwana harusi wenyewe. "Je, na ndege hufundana?" Alishangaa Matatizo.

"Hata kama hawapakani hina na piko, wanafurahia harusi yao. Hata kama hawatoi wala kupokea mahari wala kusainishwa vyeti vya ndoa, wanafurahia. Kwani furaha ni nini iwapo maisha hayana maana?" Aliwaza na kuwazua.

Walikuwa na furaha hata kuliko yeye binadamu! Hili halikuwa na ubishi kwa Matatizo hata kama alikuwa hajui matatizo yao.

Ghafla alisonya na kuendelea kujisachi.

Wakati akiendelea na zoezi la kujipiga sachi, Mateso alijizoazoa na kuondoka bila hata ya mumewe kujua.

Matatizo alipostuka mwenzie hamwoni. Alijisemea, "Au huyu chaudongo kaishaikwapua pesa yangu? maana analo dongo jingi na sijaleta dongo muda mrefu" Ghafla alijikuta akiyaelekeza tena mawazo yake kwenye ndege. Alianza kusema nao utadhani wanamwelewa! Alisema, "Nanyi mmezidi. Kila siku sherehe haziishi!"

Alisogea karibu na mti ili kuona vizuri vituko vya sherehe ya viumbe hawa. Alijisemea tena, "Lione lile. Lina kitambi utadhani DC! Inaonekana na hawa ndege wanao maskini na matajiri. Maana naona lile linavyoongea bila kukoma nadhani ni li-mwanasiasa, tena mwanasiasa mwenyewe Heri wa Kupata, tapeli mkubwa duniani na alaaniwe. Lile jingine limenuna utadhani mkufunzi wangu wa mgambo!"

Alipokuwa akizidi kuongea na ndege ambao hawakumjibu, mara likatua kundi jingine la ndege. Kelele ziliongezeka, shamrashamra na salamu huku nyimbo zikihanikiza.

Alisahau kuwa alikuwa na mtihani wa kununua utumbo wa mjamzito.

Alizidi kuongea na ndege, "Yaani, hata ndege mnatuzidi sisi binadamu. Mnachangamkiana wakati sisi tunachukiana! Naona yule anamlisha kinda wake! Heri yake ana cha kumpa huyo mwanawe wakati mimi sijui wangu akizaliwa ataishi vipi?"

Alijisemea tena, "Ila inabidi mjiandae kuteseka maana naona miti inavyokatwa na magogo kusafirishwa nje, karibuni mtakuwa hamna pa kutua. Sijui nanyi mtaambiwa mpange uzazi!"

Aliendelea, "Nyinyi mnakula na kulala bure na tena hamlipi kodi. Pia, hamnyonyani kama sisi. Hamnyenyekeani kwa sababu ya kitu alichonacho mtu, bali utu wake"

Alichomoa tumbaku yake mfukoni na kibiriti na kuwasha msokoto wake na kuendelea, "Nanyi kama mngeletewa pesa sina shaka mngejenga matabaka kama yetu" Alinyamaaza na kuwatazama ndege na kuendelea, "Na kama mbunge wenu angekuwa kama Heri nanyi mgenyonywa tu na kama mngekuwa raia wa Mizengwe mngetapeliwa tu."

Alikohoa na kuendelea, "Jamaa, hili lina mkono wa tumbaku! Tumbaku yake ni kali kweli." Aliendelea, "Yaani, umaskini huu. Kijana mzima navuta tumbaku badala ya sigara! Lakini, sigara ni za wenye pesa na wakazi wa mijini" Alijiliwaza huku akipuliza moyo kwa ridhiko.

Ghafla ndege waliruka kuelekea wakujuako. Hapa ndipo Matatizo alirejea kwenye zoezi lake la kusaka Kwenje mia mbili.

Alijisemea, "Ukiwaona wanaanza sherehe zao,ujue kiangazi ndiyo kinaingia. Kumbe nao ni kama sisi! Kwani kiangazi ni wakati wa sherehe, ndoa hata ngoma."

"Ila nyinyi pamoja na miziki na furaha zenu hamna vyombo." Aliwaambia ndege waliokuwa kwenye mkutano wao kwenye mti wa mkangazi utadhani watu! Alizidi kunogesha hotuba yake kwa ndege, "Nyinyi nawapenda sana. Kwani muziki wenu hauna matusi wala ubabaishaji na kelele. Wanamuziki wenu hawavai nguo za aibu na kujichorachora huku wanaume wakitoga masikio kama wanawake. Naona yule anachezacheza. Hayuko uchi kama changudoa wa Mizengwe."

Baada ya kuridhika kuwa kwenje yake haikuwamo mifukoni alijisemea, "Kwa nini huyu kaondoka kama mwizi? kaishachomoa pesa yangu na kwenda kununulia udongo!" Alijiuliza na kujijibu.

Aliendelea kusema, "Ngoja nimfuate nyumbani nimuulize. Maana usiku nilipolala kuna kipindi aliamka na kwenda kwenye kamba nilipotundika nguo zangu."

Alitimka kuelekea bandani alikokuwa mkewe akimpikia majani ya kunde na bada.

Akiwa anatweta na mwenye kuudhika kidogo aliingia bandani mwao akitaka kujua kama mkewe ndiye alikuwa amechukua pesa yake.

Hakungoja. Alimuuliza mkewe, "Mama Katumbo, wewe ndiye ulichukua pesa yangu mfukoni?"

Bila ya haraka Mateso alijibu, "Mimi si mama Katumbo. Alimkosoa mumuwe na kuendelea, "Ndiyo. Niliichukua usiku na ndiyo nimenunulia hili dongo ambalo nalo limekwisha na ukipata pesa uninunulie jingine mume wangu."

Maneno ya Mateso yalifungulia kivumbi cha maneno.

"Hivi mwanamke wewe una akili timamu? Yaani, kwenje mia mbili nzima yote umeenda kuchezea kwenye udongo! Ama kweli jambo usilolijua ni sawa na usiku wa kiza, tena kinene." Matatizo alifoka kwa hasira.

'Kila siku nakwambia. Hivi unadhani mimi najifanya kula udongo kama mdudu? Mbona hunielewe. Hivi ulitaka nikaibe?" Mateso alimuuliza.

Jibu hili lilimchafua Matatizo ambaye bila kujali hali ya mkewe alijibu kwa hasira, "Sasa utakula utumbo wako. Maana hiyo ndiyo pesa niliyokuwa nayo kwa hadhari. Sasa, kwa vile umechagua udongo, achana na sahau utumbo."

Mateso hakujibu. Aliendelea na kuchochoea jiko lake.

Kuona kuwa mkewe hakujibu,Matatizo alisema, "Yaani, mke wangu kubali umekosea. Maana umeazima jamvi matangani. Japo hali hii si ya kujifanya ilibidi utumie lau akili."

Majibu haya yalimchefua Mateso. Alisema, "Yaani, unaendelea kunitukana kuwa sina akili! Ningekuwa sina akili ungenioa na kunikabidhi huu mzigo?"

Matatizo aliendelea kuwa kimya. Mateso aliongezea, "Mume wangu badala ya kushikilia kulaumu na kujisemea, uwe unachagua maneno ya kusema na jinsi ya kuwajibu wenzio." Alisogeza ukuni kwenye meko vizuri na kuendelea, "Hivi unaona najifanya kuguguna udongo kama mbuzi?"

Matatizo alikuwa amebanwa. Hakujibu.

Mateso alimchokoza tena, "Wanaume mnapendwa kuitwa baba fulani na kuwapangia hata maisha watoto wenu. Laiti siku moja mngebeba mimba japo kwa siku moja, idadi ya watu Githakwa ingeporomoka. Leo nimekuwa mtu wa kutotumia akili na kujifanya." Alianza kulia.

"Mke wangu huna haja ya kulia. Ni hasira tu na huu umaskini wetu. Basi nyamaza, nitaenda pale kwa Kupata nifanye hata kibarua hata kama ni cha kudhalilika kuliko kukutesa. Niamini nitafanya chochote mradi nisikutese mpenzi wangu." Alimbembeleza Mateso.
Mateso aliacha kulia na kusema, "Kama utaendelea na maneno yako

ya masimango nitamwambia mama mkwe maana anajua maana ya kula udongo. Kwani naye aliyapitia haya yanayonikumba, anaelewa vizuri. Japo unanicheka nawe ulitoka huko."

Matatizo hakuwa na la kusema bali kupuuzia huku kichwani akipiga hesabu jinsi ya kupata pesa ya udongo na utumbo au mapupu.

Moyoni alijisemea, "Lakini, kweli maana mama alinisimulia alivyotaka kuniita Udongo kutokana na kuubukanya udongo."

Akiwa kwenye lindi la mawazo na suto, alishtuliwa na sauti ya Mateso.

"Mume wangu naomba ukaazime shoka unipasulie kuni maana naona hizi ndiyo zimekwisha."

12

Matatizo hakupinga. Badala yake aliondoka haraka kwenda kuazima shoka kwa jirani yao Kilimwengu.

Kwake hii ilikuwa ni nafasi ya kukwepa maneno ya mkewe na kutafakari jinsi ya kumkabili Kupata ili amkopesha japo Kwenje mia tano.

Kwa vile alikuwa amepata sababu ya kumwepusha na hasira za mjamzito, alitimka harakaharaka.

Baada ya kupita mkungu alisimama na kuanza kuongea peke yake, "Yaani, nakwenda kujidhalilisha kwa yule habithi msaliti!" Alikwenda pembeni ya njia kujisaidia haja ndogo. Wavutaji tumbaku ni watu wa ajabu. Haiendi haja hadi avute. Alichomoa msokoto wake na kuuwasha huku akifungua zipu ya suruali yake.

Mara ghafla nyoka wa kijani alikurupuka kiasi cha kumstua. Aliruka huku matone ya mkojo yakimchuruzika asijali. Alijipa moyo. "Uhai muhimu kaka hunipati." Alimwambia yule nyoka aliyekuwa katimua mbio kumwepa.

Matatizo ana tabia ya kuongea na miti, mawe hata wanyama. Tabia hii aliirithi kwa babu yake marehemu mzee Molowo. Naye alikuwa na tabia ya kuuhisha kila kitu hata maiti.

Kuna kipindi aliwaacha hoi watoto wa marehemu Ngofiro. Kwani alipokwenda kulipa deni lake alilokuwa kachukua kwa baba yao akiwa hai alisema, "Leo nimekuja kumalizana na baba yenu Ngofiro."

Watoto walishangaa wakadhani amepagawa. Baadaye alipofafanua ndipo kiroho kikaacha kuwadunda. Maana waliishaanza kumdhania mwanga.

Alimaliza shughuli yake kwenye mitunguja na kutimka kuelekea kwa Kilimwengu huku akipiga miluzi.

Ghafla alikutana na mijusikaka walioonekana kama mke na mume walikuwa na ugomvi wao. Alisema nao, "Hamna aibu! Fanyeni mambo yenu kwa kificho. Hivi nanyi mna wabakaji kama sisi? Alizidi kusema,"Hivi na nyinyi mnahongana kama sisi? Je, nanyi mna rushwa ya ngono kama Mizengwe?"

Kwa vile hakuhitaji jibu, aliendelea na safari yake baada ya kujifurahisha kwa kuongea na visivyoongea.

Ilisemekana kuwa utamaduni huu wa kuongea na vitu visivyoongea uligunduliwa na mtu mmoja mtengeneza mvua. Alipokuwa ameletwa kwa mfalme Nkuzi kuuawa kwa kuzuia mvua isinyeshe, aliamua kuongea na mawingu na bahati yake mvua ilinyesha sana.

Alipoulizwa ilikuwaje akaamrisha mawingu alisema kuwa mtu yeyote akiongea na chochote kinamwelewa. Tofauti ni kwamba watu walikuwa hawajui hilo. Tangu siku hiyo ulijengeka utamaduni huu ingawa kuna kipindi mfalme Nkuzi alikuwa akiujaribu na kukwama mwisho wake akawa anaharamisha baadhi ya vitu.

Alizidi kupiga miluzi na kuendelea na safari yake huku akiwa amefurahia kuwashauri wale mijusi ambao walipomwona waliacha kibarua chao na kutimkia vichakani utadhani walikuwa wameuelewa na kuukubali ushauri wake. Watu wa Githakwa hupenda kuongea na kila kitu!

Njiani alikutana na jirani yake Kilimwengu aliyekuwa anaelekea kwake. Kilimwengu aliyetoka kuagana na mkewe anakwenda kwa Matatizo ili kujadili safari yao usiku kwenda msituni kukata magogo.

Wawili hawa waliamkiana na kuanza kuongea. Kili hakumkawiza, aliangusha bomu lililokuwa likimsumbua moyoni mwake, "Matatizo, umepata habari kuwa tunapaswa kuhama kupisha upanuzi wa machimbo ya vito?"

Habari hii ilimtia Matatizo mshtuko si kawaida. Kwani kabla hata ya kujua majaliwa ya tumbo la mkewe na banda lake sasa na ujio wa mama mkwe wake, linaingia tatizo jingine!

Huku akitweta alishusha pumzi na kuuliza kama vile hakuwa ameelewa alichoambiwa. "Unasemaje?"

Kilimwengu alijibu, "Nakuuliza kama umepata taarifa ya kutakiwa kuhama eneo hili ili kupisha upanuzi wa machimbo ya GRGW."

GRGW kirefu chake ni Get Rich in Goons' World ambayo ni kampuni tanzu ya kampuni moja ya kigeni inayoitwa Richman Hoax and Co ambayo inasemekana kuwa na uhusiano na waziri mmoja mwandamizi wa Mizengwe,

"Tuhamie wapi na vipi?" Aliuliza Matatizo.

Swali hili lilikuwa gumu kwa Kilimwengu. Kwani naye pamoja na kupokea taarifa hiyo ya amri, hakuambiwa mpango mzima wa kuhamishwa zaidi ya kupanga kugomea mpango huo.

"Hata nami najiuliza swali hilohilo. Linanichanganya na kunitisha. Sasa ni saa ya kufa na mtu. Heri kufa tukipambana kuliko kulialia. Maana adui yetu sasa yuko kwenye miliki yetu. Hatuwezi kuwa wapumbavu kufa tunajiona." Alijibu Kilimwengu kwa sura na sauti ya huzuni.

"Kaka, sasa hawa watu wanataka kutuua. Hivi serikali yetu ina akili kweli! Yaani, kosa letu ni kuwachagua?Alilalamika Matatizo.

Kilimwengu alidakia," Kaka, watuue mara ngapi? Sisi ni wafu wanaotembea. Hujui hili! Tunahitaji ukombozi na saa yake ni sasa."

Matatizo hakujibu hili swali bali aliendelea kulalamika, "Wameuza viwanda na mabenki yetu, tena kwa bei kichaa; hatukusema kitu. Wameuza kila kitu. Sasa wanataka kutuuza nasi kwa mafisi na simba! Hawa watu tusipowatolea uvivu hakika watatumaliza na vizazi vyetu."

Alikohoa na kuendelea, "Nao kwa jeuri na upumbavu wao wameridhika! Alichomoa tumbaku yake na kuanza kusokota na kuendelea, "Wameingia mikataba ya madini yenye kila sura na harufu ya rushwa na wizi, hatusemi kitu. Wameuza mashirika ya umma moja baada ya jingine, hatujasema tu."

Kili alimuunga mkono na kusema, "Huenda walipoona tumekaa kimya wamedhani tumeridhika na utawala wao. Hawajui penye kimya kingi!"

Matatizo aliwasha msokoto wake na kupulizia moshi baada ya kupiga kama mikupuo minne hivi na kuendelea, " Wameonja asali, wanataka kuchonga mzinga. Sasa hawajaridhika, wanataka kutuuza sisi na makaburi ya mababu zetu! Kweli hapa lazima tuwaonyeshe kuwa nasi ni watu, tena watu kwelikweli hata kama hatuna pesa wala madaraka. Serikali ina lipi angalau la kujitoa lawama?"

Kili hakulijibu swali hili. Hivyo Matatizo aliendelea, "Kama tutategemea serikali itusaidie tutakuwa tunakosea, tena sana. Hapa hakuna serikali. Mimi huwa sioni tofauti ya mkoloni na hawa. Hawa wameishatugeuza ng'ombe wao, tena hata ng'ombe ana nafuu maana hulishwa na kujengewa angalau zizi ili atoe nyama na maziwa."

Alisita kidogo kufikiria la kusema. Aliendelea, "Usimalize tumbaku hiyo. Maana unavyoikupua utadhani uko peke yako!" Kili alimtahadharisha. Alimkabidhi tumbaku Kili na kuendelea, "Sisi kazi yetu ni kujenga taifa wao kulibomoa. Eti wanatuhimiza sisi wenye moyo tujenge wao wenye meno watafune! Lakini, ipo siku hata ng'ombe atashtuka na kutembeza mateke na siku naona ni kama leo."

Alipiga chafya na kuendelea, "Wao wanatwambia tujenge taifa. Sasa hii lugha ya kujenga taifa wakati wengine wakilibomoa tuikatae, vinginevyo matatizo yataendelea kuongezeka ilhali wao wanaendelea kutukoga na kutunyonya."

Alikohoa tena na kuendelea, "Yaani, wametugeuza hata wezi! Kwani huu ukataji wa magogo tunaofanya kwa mashindano huoni tunaibia vizazi vijavyo? Lakini, ukishikilia hilo wao wanazidi kutoa leseni za ukataji! Matokeo yake tumeanza kujiibia wenyewe! Tukatae hii jinai na aibu. Tuamke tusimame na kukataa katakata."

Aliendelea baada ya kuruhusu mwenzie atafakari maneno yake, "Kuna kipindi unajiuliza kama kweli hata wasomi wetu wana maana. Maana

ukiangalia wahusika wengi ni madaktari na maprofesa lakini bure kabisa. Huu ni udaktari wa mazingaombwe."

"Kaka tatizo si elimu. Tatizo ni uzalendo na ubinadamu. Nasi pia ni tatizo. Maana kujikomboa hakuhitaji hiyo elimu bali kujitambua na kutambua tatizo na kuwa tayari kulikabili katika hali yoyote. Maana mimi nijuavyo elimu haiondoi upumbavu na roho mbaya ya mtu.

Ingekuwa hivyo wazungu wasingetutawala na kuendelea kutunyonya. Pia, mimi nilipozamia meli nilijionea mwenyewe wazungu tena wanaume wakigeuzana wanawake. Unadhani nakudanganya kaka?" Alinyamaza na kuendelea, "Pia, uelewe hata hao unaowaita madaktari na maprofesa, wengi wao wamepata vyote hivyo kwa wazungu na ndiyo maana inakuwa rahisi wazungu kuwatumia. Maana wanawajua vizuri. Wamewasomesha na wengine hata kuwaozesha. Wanawajua vizuri, tambua hilo." Aling'oa unyasi akaanza kutoa uchafu kwenye meno yake na kuendelea. "Kaka usomi si karatasi na maneno bali matendo. Tungekuwa na wasomi tusingefika hapa."

Alikohoa kidogo na kuendelea, "Halafu wakati fulani nilipokuwa mjini nilimsikia jamaa mmoja akisema kwamba wanaojiita wasomi nchini Mizengwe,wala si wasomi chochote. Yeye aliwaita 'Minyoo ya vitabu' yaani, wanasoma vitabu vilivyoandikwa na mzungu na kufanya mitihani na kufaulu kwa vigezo vya kizungu. Lakini, hawawezi kutumia elimu hiyo kulikwamua taifa bali kulizamisha. Huoni wanavyotuangamiza kwa faida ya mzungu anayewatumia?"

" Nakubaliana nawe" Alisema Kili na kuendelea, "Kweli tangu lini mbwa akamng'ata bwana wake? Hajitaki? Kumbe ndiyo maana wanafanya ziara nyingi Ulaya kuliko vijijini. Kumbe ndiyo maana mzungu akikohoa wanatetemeka utadhani ndiye huwapigia kura!" Alipuliza moshi na kuendelea, "Hujasikia wabunge walioghushi karatasi ili waonekane wasomi? Ajabu hawakuchukuliwa hata hatua! Sasa hapa sheria ni ya nini na nani kama inabagua?" Alilalamika Kilimwengu kwa kumalizia na swali akiwa amekasirika kabisa.

"Uchaguzi kaka mtego. Matatizo alijibu tangu lini binadamu akawa na urafiki na mapenzi na panya kiasi cha kumwekea karanga? Hawa watu wanatumia takrima zao kama chambo. Samaki akiishakimeza wanavuta na kumhesabu mbavu wakicheka na kushushia na bia. Mara hii umesahau mtalii wetu anavyokuwa karibu nasi wakati wa mwaka wa uchaguzi?" Alimalizia Matatizo huku akitikisa kichwa.

"Kumbe ukaribu wote wakati wa kampeni ilikuwa ni janja ya kutuelekeza kuzimu! Ama kweli usilolijua ni usiku wa kiza!" Alisema Kilimwengu aliyeonekana kuudhika na kuchanganyikiwa.

"Unauliza jibu? Hujui kuwa huyu ni mtalii? Kuna haja ya kuwahamasisha wananchi wetu wajue umuhimu wa kura yao na kuwapigia wenye sera za kutuinua badala ya kuridhika na hongo ndogondogo kama kanga,vibandiko na fulana na kila aina ya ukarimu wa mara moja kwa muhula." Kilimwengu alisema.

"Je, mbunge wetu naye anasemaje?" Aliuliza Matatizo.

"Kaka unaulizia huyo msaliti mtalii! Huyu ndiye chanzo cha matatizo. Tangu tumchague uliwahi kumsikia akiongelea haki zetu au kutupa taarifa ya uamuzi wao bungeni?"

Alikohoa na kuendelea, "Tangu atulangue kura zetu hajawahi kukanyaga kwenye jimbo. Yuko mjini na wakubwa wenzake wakijadili biashara hii ya kulangua nyoyo zetu. Wako kwenye maisha yao na vikao vyao vya kuvutia wawekezaji ambao wametugeuza wakimbizi ndani ya tunachokiita nchi yetu." Aliwasha tumbaku tena na kuvuta kidogo na kuendelea, "Hata mbunge mwenyewe akija utamkaribia au kumuona? Utamwona wapi yupo kwenye gari la viyoyozi na vioo vyeusi! Umwone umtie nuksi. Mbunge si yule rafiki uliyekuwa ukisalimiana naye tena kwa kukumbatiana wakati wa kampeni." Alimalizia Kilimwengu.

Alikupua moshi wa tumbaku na kuendelea, "Mbunge sasa ni mheshimiwa. Si yule tuliyekuwa tunakunywa naye gongo wakati wa kampeni na kusalimiana kwa kukumbatiana. Wakati ule ulikuwa ni wakati wa kutafuta

cha mvunguni. Sasa kaishakipata kuinama kwa nini tena?"

Alimpa msokoto mwenzie na kuendelea, "Ni wakati wa kutandaza mitego na kuwavutia kware. Ukishampata kware mwituni utafuata nini ndugu yangu?" "Halafu wewe kwa lugha za mafumbo na vijembe!" Alitania Matatizo.

"Si mafumbo. Ni uchungu kaka. Sisi ni watu wazima wenye elimu ya vitendo kutoka kwenye darasa la maisha ingawa wasomi wa kizungu hawatutambui. Wasomi wa kizungu wanataka karatasi zinazoitwa vyeti kaka. Ndiyo maana wajanja siku hizi wanayafyatua kwa wingi na kuwaibia hawa wajinga wanaotuibia sisi." Alijibu Kilimwengu.

Baada ya kupokea tumbaku na kubugia mafunda kama manne ya moshi, Matatizo alikubaliana na mawazo ya Kilimwengu. Alisema, "Nakubaliana nawe asilimia mia. Hukumbuki mwaka juzi alivyotuchangisha pesa ya kuchimba barabara ya kwenda kwake? Ajabu hata mtu ukiuguliwa anakukodisha gari lake ambalo asingelipata kama si kura yako. Mwaka juzi Kazibwe ilibidi auze mbuzi watatu ili kumlipa mbunge baada ya kumpeleka mkewe hospitalini Githakwa."

"Tuliibiwa na kutumiwa. Hakuna kitu kinachoniumiza kama watu walivyokuwa wakijipendekeza kusukuma gari lilipokuwa likikwama kwenye tope kabla hajatuibia pesa yetu kumtengenezea barabara binafsi, utadhani nasi tuna magari!"

Alivuta tumbaku yake tena na kuendelea, "Wakati wa zamani mbunge alikuwa kama baba wa wapiga kura wake. Kwanza alikuwa haendi bungeni bila kupata mawazo yao ya kwenda kusema bungeni. Alikuwa akiishi jimboni kwake. Siku hizi wabunge wetu ni watalii. Kikao kilichopita nilimsikia mbunge akiulizia juu ya kupinduliwa kwa dikteta mmoja Uarabuni akitaka eti na Mizengwe ilaani kitendo hicho! Ni mbwa gani amng'ate bwana wake?"

Waliangua kicheko na kuendelea, "Ule utamaduni wa kukutana na mbunge kumwambia matatizo yako umekwisha. Ataongeaje nawe wakati kuna wawekezaji wenye pesa wanamngoja? Wewe kwake huna shida zaidi ya

kukununulia pombe na kukupa vikofia wakati wa kampeni."

"Ukikumbushia enzi hizo unaambiwa umepitwa na wakati. Sasa ni chuma ushibe hata kwa kuuza damu ya nduguzo." Alijikuna kidogo kichwani na kuendelea, "Hukumbuki kipindi kile mpambe wake mmoja alivyotwambia kuwa kura zenyewe alinunua kwa pilau, gongo, kanga na kofia sasa watu walichokuwa wanadai kwake nini?" Alisema Kili.

Matatizo alijibu, "Achia hapo. Yaani, tumeuza uhuru na mali zetu kwa zawadi za pombe, kioo, shanga, shuka na kofia! Kweli kile kisa cha chifu Mangungo wa Tanzania tulichofundishwa shuleni kinatimia tena bila kupungua wala kukosewa!"

Alinyamaza kidogo na kuendelea, "Heri ya hata ya Mangungo hakujua kusoma na kuandika wala hakuwa na digrii na isitoshe hakuingia hiyo mikataba kwa nia mbaya wala tamaa zaidi ya kudhania ungekuwa ukombozi wa watu wake. Unakumbuka kile kisa cha mwaka juzi ilipogundulika kuwa Waziri wa Mifugo alikuwa amehongewa pete ya dhahabu kuruhusu dawa feki ya sotoka iuzwe Zuga?" Matatizo alilaumu na kuendelea, "Nakumbuka sana. Yaani hawa watu ni wapumbavu. Kwa mfano leo nani amhonge Mzengwe zengwerald wakati inachimbwa hapa? Huu ni ukuku. Mkaangie kuku mayai yake hata nyama ya mwenzie ataifakamia. Lakini, huwezi kumlaumu kuku maana ubongo wake haujai hata kijiko cha chai." Alikumbushia Matatizo.

Kilimwengu alidakia, "Ehee, una habari kuwa kisa hicho ndiyo kilifanya Redio Fikira iache kusikika kijijini? Wakubwa waliona inasababisha wananchi kujua madhambi yao. Hivyo walianzisha redio za miziki usiku na mchana ili kuwavutia watu wasikilize upuuzi badala ya habari muhimu. Pia, nasikia hata huu umaskini wetu unawasaidia kututawala. Maana hatupati habari. Nani ataleta magazeti huku ambapo hatuna pesa ya kuyanunua?"

'Hilo mbona linajulikana. Nilipokuwa mjini yalishamiri magazeti ya ngono na miziki tena ya matusi. Lakini, serikali haikuhangaika nayo kwa kujua kuwa watu wakiyapenda yatawapotosha na hawatajua haki zao."

Alijibu Matatizo.

Aliendelea, "Una habari kuwa katika nchi ya Mizengwe ni rahisi kupata kibali cha kucheza ngoma lakini si kuandamana? Una habari ni rahisi kupata mkopo wa kuanzisha baa au ukumbi wa muziki lakini si wa kujenga shule? Wenzetu wanajua wanachofanya."

Kilimwengu alimuunga mkono, "Zamani ilikuwa ni kosa la jinai kwa mtoto kukimbia shule na kwenda kuuza karanga mjini. Lakini, nakumbuka juzi pale wilayani nimeona watoto wengi wanaopaswa kuwa madarasani wakiwa wanauza karanga tena mbele ya polisi!"

"Wewe unasema hilo! Mie nilipokuwa Fikira nilikuwa karibu kila siku nikishuhudia wanafunzi, tena wakiwa na sare za shule, wakiingia Nyumba ya Kulala Wageni. Walipokuwa wakitoka wanaenda hoteli kula. Tena mara nyingine unakuta na polisi yumo humohumo." Matatizo alitikisa kichwa.

"Hivyo ndivyo wanavyotaka. Maana hao si watoto wao. Ni watoto wetu. Wao wanatutawala na watoto wao watatawala watoto wetu hivyohivyo hadi kiama tusipozinduka." Alijibu Kili aliyekuwa amesogea pembeni kidogo akijisaidia haja ndogo huku akiendelea na maongezi.

Wakati maongezi yakiwa ndiyo yananoga, kelele za Mateso ziliyavuruga. Kwani baada ya kungoja mtu aliyeendea shoka asimwone aliamua kumfuata.

13

Akiwa ameghadhibika, Mateso alitoa salamu na kumuuliza Kilimwengu,"Shemeji huyo bwana mbona kakugandisha hapo ilhali aliaga anakuja kwako kuazima shoka, kulikoni?"

"Samahani sana shemeji. Kuna msiba. Ndiyo nilikuwa nampa taarifa zake. Hivyo bila hata kujuliana hali tulijikuta tukizama kwenye jinsi ya kujikomboa na balaa hili."

'Msiba wa nani tena?" aliuliza Mateso kwa mstuko huku akijilaumu moyoni kwa kumlaumu bure mumewe.

"Hakufa mtu bali matatizo ya kimaisha." Kilimwengu alijibu kwa ufupi.

Baada ya kupita kitambo na Mateso kujulishwa kulikoni kwa utuo, walikubaliana mumewe na Kilimwengu, waandamane kwenda kwa Mjumbe wa Nyumba Kumi kujua nini hatima yao. Hivyo, Mateso aliamua kuendea shoka mwenyewe. Maana kutokana na hali yake na majukumu ya mama hawakuona umuhimu wa kumwingiza kwenye sakata hili.

Aliwaaga Matatizo na Kilimwengu na kuanza safari ya kuelekea kwa Kilimwengu.

Kwa vile tumbo lilikuwa limesogea sana, baada ya kukata kona tu aliamua kujipunzisha chini ya shina la mti huku akitafakari aliyosikia.

Mara alijesemea, "Hivi babu yangu aliyepigania uhuru wa nchi hii akirudi leo na kunikuta kwenye hali hii si atazimia. Maana nakumbuka alifungwa miaka saba kwa kukataa kulipa kodi kwa serikali ya kikoloni. Aliamini kuwa alikuwa akipigania uhuru ili sisi tuishi maisha yenye maana badala ya hiki kitendawili." Alijikuta akisonya kwa hasira na kutikisa kichwa chake.

Alizidi kuongea peke yake, "Akina Kupata waliokuwa wanapinga kupatikana kwa uhuru ndiyo hao leo wako mstari wa mbele kuzaa wabunge, matajiri na kila aina ya watoto waliofanikiwa wakati babu zetu wameambulia kuacha watu wasio na mwelekeo hata wa siku moja!"

Alijisogeza kidogo na kuegamia mti na kuendelea, "Dunia hii haina maana. Imetawaliwa na wasaliti na waovu wanaowaangamiza, kuwanyonya na kuwakandamiza watu wasio na hatia. Hivi huyu Mungu kweli kazi yake ni ipi iwapo dini zake nazo zimekumbatia mafisi waliovaa ngozi ya kondoo?" Anaamua kujijibu, "Lakini, Mungu haishi hapa na isitoshe hata hao wanaomtumia kila uchao wanaumbuka. Juzi padri alipokamatwa ugoni na mke wa muumini wake ndipo niliona mwisho wao unakaribia." Alivuta upande wake wa kanga chakavu na kujifuta kijasho kilichosababishwa na hasira na uchovu na kuendelea, "Mungu nisamehe kwa kuhoji huu wizi. Sina ubaya na wewe na isitoshe japo siamini kwenye dini hizi za wizi, naamini upo unaniona."

Baada ya kuongea peke yake na kupumzika vya kutosha aliamua kujizoazoa na kuendelea na safari yake huku akivinjari anga za Githakwa aliyoipenda sana japo utawala mchovu ulikuwa ukiupora uzuri ule.

Alipofika kwa Kiliwengu, kutokana na hali yake kuwa ya uchovu, mke wa Kilimwengu, Bi.Tunasota, alimuonea huruma kutokana na hali yake, hivyo aliamua kurudi naye kwake ili amsaidie kupasua kuni.

14

Huko nyuma baada ya Mateso kukata kona kiasi cha kutoonekana, Kilimwengu na Matatizo walisahau ulimwengu na matatizo yao kama majina yao juu ya kuhama.

Walianza kumsengenya Mateso. Kumbe hata wanaume wanakuwa wambeya! Binadamu wote ni sawa. Wana tabia na mahitaji yanayofanana ingawa wapo wanaowagawa kijinsi.

Tabia zao huanika kila kitu, ingawa silka ya ukandamizaji na unyonyaji huchomoza na kujenga matabaka.

Kilimwengu alisema, "Mzee naona umeishashinda bao. Maana huo mtungo si haba. Huenda likatoka dume humo."

"Bwanawe, hiyo mimba mbona imegeuka kifungo kwangu! Kwanza, mwanamke anavyojishindilia midongo sijui kama haitamwathiri mtoto tumboni. Yaani, ni mateso na matatizo kama majina yetu. Utadhani wazee walijua kuwa Matatizo atamwoa Mateso ili amtese na kumwongezea matatizo!"
Kabla ya kuendelea, Kilimwengu alimtoa wasiwasi, "Hii ni kawaida hata mama zetu walibwia madongo. Kwa vile ni mtoto wenu wa kwanza lazima uwe na mshawasha hata jokomoyo. Nasi tulipitia huko."

"Hiyo tisa kaka. Kumi mama anakula utadhani wamo watu mia tumboni mwake!" Alilalamika Matatizo.

"Kwani kula vibaya?" Kili hakungoja jibu, alijibu na kuendelea, "Mbona mjamzito anayekula ndiye mzuri. Maana hata mtoto tumboni anapata virutubisho anavyohitaji na mama anakuwa na nguvu."

"Kaka, shida yangu si kula bali mfuko baba. Angekuwa anatamani vyakula vinavyonunulika, mara mapupu, utumbo, mara kile sijui akitamani figo na maini itakuwaje? Maana mimi nilikula figo mara ya mwisho nilipokuwa kwenye kampeni za uchaguzi mwaka jana, na yenyewe ni baada ya kujipendekeza kwa mbunge na kudokoa kwenye meza yake!"

Alicheka na kuendelea, "Unaamini kuwa mke wa Heri pamoja na utajiri wa mumewe anatamani maharage badala ya figo na samaki? Kweli Mungu ana jinsi ya kuwalinda na kuwalinganisha wanadamu."

Alivuta tumbaku na kumpa tena msokoto Kilimwengu na kuendelea, "Mama kageuka jini ghafla. Hadi nafikia kujuta kwanini nilifanya hivyo. Sasa hili la kuhamishwa kupisha wawekezaji ndilo linaniua kabisa."

"Huna haja ya kujuta na kumlaumu Mungu. Kwani ndoa maana yake hasa ni kuongeza kizazi. Hatukuanza sisi wala hatutakuwa wa mwisho."

Kili alinyamaza kidogo kukamua msokoto wake vizuri. Alitutumua moshi mwingi na kuendelea, "We mshukuru Mungu kuwa hana maradhi yanayomhangaisha." Alinyamaza kidogo na kuvuta tena tumbaku yake iliyokuwa inaanza kusinzia na kuendelea, "Hukumbuki kisa cha waliouza mbuzi kulipa gharama ya kusafirishiwa mke na gari la mbunge?"
Alivuta tumbaku na kusema, "Hii tumbaku vipi ilikuwa na unyevuunyevu nini, mbona inasinzia haraka hivi!"

Alikohoa kutokana na ukali wa tumbaku na kuendelea, "Sisi maskini Mungu anayo njia ya kutulinda na kutunusuru na majanga mengine yanayowakumba matajiri kama kukosa usingizi, woga, majuto, ugonjwa wa moyo na mengine kama hayo."

"Ila kaka, lazima mwaka huu kijulikane. Lazima bubu aseme ili iwe taarifa kwao kukaa chonjo saa mbaya. Mara hii umesahau msemo huu ambapo umdhaniaye ndiye huwa siye!" alichomekea Matatizo.

Alitema bonge la kohozi lililokuwa linamemng'ang'ania kooni na kuendelea, "Mimi sikubaliani na kumtwisha mzigo Mungu ambaye haishi nasi kwenye matatizo haya. Mungu alikwishatupatia macho, mikono na akili. Hatuna haja ya kuendelea kumbebesha mizigo. Lazima tuamke tupambane, vinginevyo tutakwisha. Hali hii si mchezo."

Maongezi juu ya maisha ya ujauzito yaliwasahaulisha kidogo makali ya taarifa ya kuhama.

Baada ya muda walikubaliana kwenda kwa mjumbe wao wa nyumba kumi ili kujua kilichokuwa kikifuatia.

15

Wakiwa njiani kuelekea kwa Mjumbe wa Nyumba Kumi, baada ya kuvuka Mto Chania, walikutana na msururu wa magari.

Kulikuwa na gari la kikosi cha kuzuia vurugu maarufu kama PPK au Pinga Pata Kipigo , Mkuu wa Wilaya, Mbunge wao waliyezoea kumwita msaliti mtalii, Heri Kutapa badala ya Kupata, Mkuu wa Mkoa Gibbons Dikupatile na maofisa wengine wenye nafasi wilayani na mkoani.

Ulikuwa ni msururu wa mashangingi na landrover kama saba hivi. Magari ya bei mbaya siku hiyo yaliingia Githakwa na kushangaliwa na wanakijiji, wengi wao waliokuwa wakiyasikia kwenye vijiwe vya kahawa. Maana kuna kipindi ulitokea ubishi baina ya Ndirangu na Matatizo. Ubishi wenyewe ulikuwa juu ya thamani ya shangingi moja.

Ndirangu alishikilia kuwa shangingi moja linaweza kununua mashamba yote ya Githakwa. Matatizo alipinga ingawa mwishoni hakuna aliyetoka na ushindi. Maongezi ya wanakijiji mara nyingi huwa juu ya mambo madogo yanayowasumbua.

Siku nyingine ulitokea ugomvi nusura ya Ndirangu kuzipiga na Matatizo. Ugomvi wenyewe ulizushwa na kitu kidogo. Ni pale Matatizo alipowakoga wenzake kuwa yeye hatishwi na shangingi. Maana aliishapanda ndege wakati Ndirangu licha ya kulipishwa kodi hajawahi na atakufa bila kupanda shangingi. Kejeli hii, japo ni ukweli, ilimuudhi sana Ndirangu.

Mara Kilimwengu na Matatizo waliupisha msafara ule ukiwa umewaachia vumbi kubwia na kukoga. Vumbi lilipotulia walianza kujadili ugeni huu ambao si wa kawaida.

Wao walikuwa wamezoea kuona magari mengi wakati wa kampeni au inapopitishwa Sanamu ya Njiwa wa Amani ambayo tangu ianze kukimbizwa ilipitishwa kijijini Githakwa mara moja.

"Kaka, sasa yamekuwa. Hata huyo mjumbe hatutamkuta. Inaonekana magari haya tena na ya polisi ni kutoa ujumbe kuwa kuhama si hiari tena." Alisema Kilimwengu.

"Kuna kipindi nilisikia ngoma na kwa vile kulikuwa na upepo na kiangazi ndiyo kinaanza, nilidhani kuna harusi au ngoma kule Ngeme," alijibu Matatizo.

Kili naye alishangaa, "Migari mizuri hiyo. Ila bei yake na uchafuzi wa mazingira usisikie kaka. Hata wale watu wafupi wanaoyatengeneza nasikia huwa wanaogopa kuyapanda ingawa nchi yao ni tajiri wa pili kwenye dunia hii ya Muumba."

Alinyamaza kidogo na kuendelea, "Je, umesikia habari kuwa Kupata kauza ardhi zake zote na nyumba zake kwa mgodi wa GRGW?" aliuliza.

"Sijasikia." Alijibu Matatizo.

"Basi, nilisikia kama mwezi mmoja uliopita kuwa kama ni pesa alilipwa magunia kwa magunia." Kili aliendelea kumjulisha rafiki yake Matatizo ambaye alikuwa kapigwa na mshangao juu ya habari ile ya kisalata.

"Basi, inaelekea wenzetu matajiri walijua mpango huu muda mrefu. Isitoshe mwanawe ni mbunge. Lazima atakuwa amemwibia baba yake hii siri ya serikali. Lakini, hawatafanikiwa. Maana wananchi itabidi, kama nilivyokwambia, tufe tukipambana badala ya kufa kama kondoo. Muda wa ukondoo na ukuku umekwisha." alisema Kilimwengu.

GRGW kama ilivyojulikana ni kampuni ya Glutton Sucker inayochimba aina ya madini yaitwayo *zengwerald* ambayo duniani yanapatikana nchini Mizengwe inahofiwa kuwa iliwahonga wakubwa kupata kupanua mradi wake.

Madini haya yaligunduliwa na wanakijiji wa Githakwa wakiongozwa na Mzee Machungi Sengaa. Serikali ilipojua kuwa kuna vito vya thamani, pamoja na kwamba haikuvigundua, iliwatimua wachimbaji wadogo

na kukodisha eneo hilo kwa kampuni ya GRGW ambayo watu wengi wanasema ni ya wakubwa na Sucker anatumika tu kuwaziba macho wananchi. Inasemekana wakubwa wengi wanawaleta maajenti wao kusimamia miradi yao kwa kisingizio cha uwekezaji huku wao wakiendelea kuiba kwenye maofisi ya umma.

Kuna maswali mengi ambayo tangu vito hivi vigunduliwe yamekuwa yakiwasumbua Wanagithakwa. Kama *zengwerald* inapatikana Mizengwe peke yake na ina thamani sana mbona hali zao za maisha haziinuki?

Kama hilo halitoshi sasa wakubwa wamenogewa na utajiri wa Zengwerald na wanataka kuwatimua wananchi!

Lakini, inavyosemekana huu si mpango wa wakubwa wote. Maana nao wanaibiana katika kutuibia sisi. Hili limewapa moyo baadhi ya wanakijiji kusimama kidete kwa lolote. Kama maneno ya Mzee Njema ni kweli, kuwa huu mpango ni wa watu wachache, basi wananchi wana kila sababu ya kushinda usaliti huu. Maana wahusika hawatataka bomu lilipuke hadi kwa wakubwa wao.

Wakati wakijadiliana, Kimbelembele, ambaye wanakijiji walizoea kufupisha jina lake wakimwita Kimbe, Mjumbe wao wa Nyumba Kumi, aliingia akitweta lakini akiwa ana tabasamu.

Aliwaamkua "Wazee salama? Hakungoja wajibu salamu yake. Aliendelea, "Bahati nimewakuta hapa. Ni kwamba kuna mkutano wa dharura pale shuleni. Nadhani mmepishana na ugeni wetu ambapo tunakwenda kujadili taarifa za kuhama ili kupisha mradi wa maendeleo ya uchimbaji wa vito."
Hakungoja wajibu, alisema, tena akitabasamu, asijue maneno yake yalikuwa ni sawa na kumwaga chumvi kwenye kidonda. "Hivyo lazima twende shuleni kuwasikiliza wakubwa zetu wanasemaje."

Kilimwengu aliyekuwa anaonyesha dhahiri kuudhika alimuuliza, "Lakini, mzee Kimbe, mbona habari hizi mlizificha na kutushtukiza, yaani, mmeamua kutuuza mchana kweupe ndugu yangu? Hivi mnadhani kuhama ni suala la harakaharaka hivi?"

Kimbe alijibu haraka, "Hata sisi viongozi tumezipata wiki jana. Lakini, kutokana na mihangaiko ya maisha ilibidi tungoje hadi keshokutwa tuwaite na kuwaambia. Lakini, hata hivyo Redio mbao zilishataarifiwa na kuanza kusambaza habari hizi. Si unajua kijiji chetu si kikubwa sana", alijitetea huku akitabasamu kwa tahayuri.

Matatizo naye aliamua kutoa dukuduku lake, "Sasa wakubwa wenyewe ndiyo hao wamekuja, hata hatujajadiliana kujua tutalipwa nini lini na kiasi gani na tutahamia wapi?"

Kili alimjibu Matatizo haraka, "Tujadili nini iwapo mpango wenyewe uliishapitishwa? Hii imekuwa kawaida ya hawa wakubwa kujifanyia uamuzi, halafu wanajifanya kuja na lugha ya kuwashirikisha wananchi! Unafiki. Kweli wananchi tutaendelea na ubwege huu? Thubutu!" Alimalizia kwa ghadhabu kidogo huku akiwakazia macho wenzake kana kwamba alikuwa akisoma mawazo yao.

"Mabwana mimi naona kuchelewa kwetu kuna heri. Kwani tutajadiliana nao tujue hapohapo tena leoleo, kitakachofuatia. Hivyo, kuchelewa kunaweza kuwa na neema. Maana hatutasikia kutoka wilayani tena bali tutasikia wenye," alipendekeza Kimbe.

Alitema mate na kupiga chafya na kuendelea, "Maana Mkuu wa Mkoa mwenyewe leo kaamua kuja kututembelea." Akiwa anajiandaa kuendelea na ngonjera zake alikatizwa na Matatizo.

Matatizo ambaye alionekana kukerwa na utetezi huu aliamua kumpa vipande vyake, "Mzee Kimbe usitufunge kamba. Hapa hakuna cha ugeni wala neema. Mimi naona ni kama kuburuzwa tu ni balaa. Mkuu huyu wa Mkoa unayemsifia ametutembelea hajatutembelea kitu. Ni mgeni gani anakuja bila taarifa?"

Alitupa kipande cha msokoto wa tumbaku kilichokuwa kimebakia kiasi cha kuanza kumuunguza vidole na kuendelea. "Hapa si ugeni bali wamekuja kututisha na kutuibia ardhi yetu. Wamekuja kuchuma. Si unaona na huyo mtalii anayejiita mbunge alivyong'atuka mjini kuja kuwauza watu anaowaita wake."

"Matatizo inatosha. Usiziite shida. Inaonekana maneno niliyoambiwa kuwa wewe ni mwanachama wa chama wa CCU ni kweli." Kimbe alijaribu kumtisha Matatizo kwa kumsingizia kuwa ni mfuasi wa chama cha upinzani.

Matatizo alitikisa kichwa kwa hasira na kuendelea, "Huu si wakati wa kujadiliana kuja kwa ugeni na kugeuzana mabwege bali kujadili hatima yetu. Hivyo tusitishane, badala yake tushikamane, maana tunateseka wote."

Kimbe aliingilia haraka, "Kaka, nani huyo ambaye kakudanganya kuwa unaweza kupinga agizo la serikali, amekupoteza ndugu yangu," alionya Kimbe.

Matatizo hakungoja amalize maneno yake. Aliamua naye kujihami, "Kwanza, usizidi kunitisha. Kuwa mwanachama wa chama chochote ni haki ya kikatiba."

Alijikakamua na kuendelea, "Mzee Kimbe, hapa tunachuuzana wenyewe. Inaonekana umeshakatiwa chako. Unataka kutugeuza sisi mabwege. Lakini, mmekosea sana. Wao wakubwa wemeishategea nyavu zao. Sasa tunasukumana sisi kwa sisi. Huku ni kuibiana. Ni usaliti na umalaya wa aina yake. Maana nakumbuka mbunge wetu kwenye uchaguzi alituahidi maendeleo. Haya ndiyo maendeleo?"

Kimbe alidakia, "Sasa umefika mwao. Kumbe sikuwa nimekuelewa!"

Alinyamaza kidogo, kama kukumbuka jambo na kuendelea, "Nani asiyejua kuwa kwa kupanua mradi wa uchimbaji wa vito serikali itakusanya kodi kubwa ambayo itatumika kwenye shughuli za maendeleo? Hujui kuwa sera ya nchi ni utandawazi na ubinafsishaji?"

Matatizo hakukubali kudanganywa kama mtoto, tena mchana kweupe. Alijibu, "Huu ni utandawizi na haya si maendeleo yetu ni maendeleo ya matumbo yao na hawara zao. Haya ni maendeleo katika kuangamia, si kuendelea."

Alikohoa na kuendelea, "Maendeleo gani kama tunahamishwa kwenye ardhi ya mababu zetu kuwapisha wageni? Kama ni maendeleo basi haya ni maendeleo hatari."

Kilimwengu naye aliamua aongezee, "Kwanza, hapa hakuna maendeleo Kimbe, tusidanganyane. Mimi nilijua. Pale machimbo yalipoanza kuchuruzisha maji yenye zebaki kwenye Mto Chania nilijua huo ndiyo mwanzo. Baya zaidi hata nyinyi mnaojiita viongozi tulipowashtakia mlituona kama wachochezi na watu wasio na akili hadi walipokuwa wale wanasheria wa mazingira. Yaani, rushwa mbuzi imewaziba macho na kuchafua mioyo yenu kiasi kwamba hamuhisi hii dhambi mnayowatendea ndugu zenu wenyewe!"

Aliendelea bila kungoja mwingine aseme, "Unakumbuka ule ubao unaotuzuia kupita kwenye msitu wa Ngimu kwenda kuwinda wakati tunashuhudia wageni wengi wakija na kufyeka miti kupata magogo?" Alimkazia macho na kuendelea, "Yaani haya maendeleo gani yanayokuja kutuzibia njia na kutuchafulia vyanzo vya maji, kutumalizia miti na sasa kutuhamisha? Huu ni usaliti."

Alinyamaza kidogo, kumeza mate na kuendelea, "Zamani tulikuwa tukikatisha pale kwenda Lalago, Tetu, Mbarandwa hata Kasori, sasa wameweka ubao na sengenge. Pia, hata ile njia ya kwenda Kololo nako kumezibwa! Tunaanza kuzungushwa ndani ya nchi yetu, kisa pesa ambayo nayo hatuioni bali inaishia kwenye mifuko ya waroho wachache."

Aliendelea, "Halafu watu, nyie mnaonekana hamna hata shukurani. Madini tuyagundue wenyewe, wao wavamie kama simba anavyovamia windo la chui, wachukue na kuwaweka mawakala wao." Matatizo alimalizia kwa hasira.

"Hajatosheka na wizi wanaotufanyia! Kweli shukurani ya punda mateke. Lakini, ni bora wakajua kuwa wanachofanya ni sawa na kumuuza mama yako. Maana sisi ni ndugu zao na bado wageni wataendelea kutucheka kwa utaahira huu," alisema Kilimwengu.

Kimbe alimpinga, "Mbona taarifa tulizopewa zinaonyesha kampuni inalipa kodi kubwa kwa serikali na imechangia kuleta maendeleo, huoni watu wanavyohudumiwa kwenye hospitali ya mgodi kwa pesa kidogo?"

"Huko ni kutupaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Wewe umeshikilia inalipa kodi, inalipa kodi? Nani anaishi kwa kutegemea hiyo kodi zaidi ya wezi wachache? Kama hiyo kodi ina manufaa basi ni kwa wale waliomo kwenye genge la ujambazi linalojiita serikali. Angalia watu wetu walivyokonda na wanavyohangaika kuishi. Kodi tunazolipa na hawa wachimba madini zinaishia kwenye matumbo ya watawala. Hujasoma kashfa kila uchao juu ya wizi wa pesa ya umma? We kalia wanalipa kodi."

Anatoa leso mfukoni na kupenga kamasi na kuendelea, "Wewe umeona hospitali ambayo ukiilinganisha na pesa inayoibiwa si chochote si lolote. Kwanza, ile si hata kospitali. Ni zahanati ndogo tu." Alimzodoa na kuendelea, "Isitoshe ukilinganisha ile pesa tunayotozwa na kipato chetu na uduni wa huduma tunayopata ni mbingu na ardhi," Matatizo alizidi kumbana Kimbe.

Kilimwengu naye aliungana na Matatizo kumwonyesha Kimbe kuwa ule mradi licha ya kuwa wa wakubwa haukuwa na maana wala manufaa kwao. Kwao hizi sifa zilikuwa sawa na matusi na udhalilishaji usio wa kawaida.

Alisema, "Unayosema kaka ni kweli. Hiyo pesa wanayosema inatolewa kama kodi wanaikadiriaje iwapo nasikia kuna uwanja wa ndege mkoa wa jirani wa Zuga ambako umejengwa uwanja wa ndege na wenye kampuni ambapo ndege huja usiku na mchana na kuruka moja kwa moja kuelekea ulaya tena bila ya kukaguliwa?"

Swali hili lilikuwa zito kwa Kimbe. Alionekana kukubali kushindwa. Hakujibu.

"Mabwana, kung'oa mzizi wa fitina, twende mkatoe kilio chenu na dukuduku lenu kwa wakubwa." Aliwasihi Kimbe.

"Wakubwa au wezi wakubwa? Kama wakubwa, basi wakubwa, lakini ovyo." Alisema Kili kwa hasira.
"Mzee mwenzetu unatudanganya. Kwa nini wewe mjumbe wetu usitoe hicho kilio chetu na dukuduku letu, kwani uongozi wako ni upi na wa nini?" aliuliza Matatizo.
Kilimwengu anadakia, "Kaka uko mawazoni mwangu. Nami naona hii kazi aifanye mjumbe wetu. Maana naye kama kiongozi anawajibika kujua shida za wananchi wake." Alimkazia macho Kimbe na kuendelea, "Tena uzuri ni kwamba mwenzetu anafahamiana na hao wakubwa wenzake au siyo mzee."

Baada ya kuona kuwa aliitwa mkubwa, kama kejeli, naye Kimbe alijibu, "Kwani wewe kichanga. Sote tu wakubwa kama ni ukubwa na kama ni lawama sote tunapaswa kulaumiwa. Wewe unalaumu serikali kuiba. Mbona nawe usiku unaenda kukata magogo?"

Kili hakumkawiza. Alimjibu, "Nani amewahi kuiba shambani mwake. Huu msitu ni urithi wetu kutoka kwa mababu zetu waliopewa na Mungu. Lakini, si urithi wa wezi wachache wanaosingizia serikali. Hivyo, futa kauli yako na uniombe msamaha."

Kimbe alijikuta kabanwa asijue la kusema. Hivyo wanakijiji hawa, pamoja na kutokuwa wamejiandaa kuhudhuria mkutano huu wa dharura, waliandamana kuelekea kwenye mkutano.

Kimbe, baada ya kugundua maji haya hayawezi, bila hata kuaga, alikaza mwendo akiwapa kichogo na kutangulia shuleni kwa ajili ya mkutano huo wa dharura.
Matatizo alisema huku akitingisha kichwa kwa masikitiko. "Maskini mzee Kimbe, kapewa kipande cha ukubwa ili atumiwe kuwanadi ndugu zake. Unaona asivyojua kitu. Yeye amefundishwa kukariri urongo wa watawala. Hana tofauti na kinyago. Yeye ni bendera tena chakavu. Anafuata upepo asijue utokako wala uendako maskini!"

"Kaka hujakosea. Hawa mbumbumbu wetu wanatuhujumu kwa kudanganywa na uanachama. Wanapoambiwa kuwa chama ni chao wanadhani kweli ni chao wakati wao ndio waliwao. Ama kweli ujinga ni mzigo tena mzito." Alisema Kili.

16

Huko nyuma Mateso aliandamana na mke wa Kilimwengu. Tunasota aliamua kuandamana na Mateso ili akamsaidie kupasua kuni kutokana na kumwonea huruma. Maana tumbo lake lilikuwa limesogea sana.

Kama mwanamke anayejua masahibu ya hali hiyo, ingekuwa ni ukosefu wa heshima na upendo kumwacha mwenzake kwenda kupasua kuni.

Isitoshe hali hii ni leo kwangu kesho kwako. Hivyo naye ingefika zamu yake, alikuwa na pa kwenda kusaidiwa katika hali hiyo.

Baada ya kuwa ameegesha mlango wa banda lao,kulitokea ubishi kati ya Mateso na Tunasota. Ulikuwa ni nani atangulie na nani afuatie.

"Bosi, mbona umesimama, unangoja nini wakati unajua kwa mwendo wako huwezi kuniacha?" Alitania Tunasota.

"Hata nawe unanitania! Ama kweli mwenye shibe hamjui mwenye njaa. Wewe tangulia kwa sababu una nguvu na sitaki ukae nyuma yangu unichore." Alisema Mateso huku akijifuta jasho.

"We tangu uote hicho kitambi unawahangaisha wenzio utadhani walikula nawe! Lakini, usijali sana, hali hii huwa inasababisha mambo kama haya. Si kosa lako, ni maumbile. Twende zetu, acha nitangulie." Tunasota aliongoza njia baada ya kuridhika kuwa ilibidi afanye hivyo.

Aliamua kuchapa mwendo kwelikweli ili aone mwenzake angesemaje. Ulikuwa ni utani wenye furaha ya aina yake.

"Hee, punguza mwendo, maana naona unataka kunitembeza utadhani sisi wanajeshi!" Alilalamika Mateso.

Tunasota alitikisa kichwa na kucheka na kusema, "Namwonea huruma mumeo. Maana ulivyo na visa kama vya kuku sijui huyo mnayelala naye

kitanda kimoja anapambana na misukosuko kiasi gani?" Alimkata jicho Mateso na kuendelea kumtania, "Miye nilipokuwa mjamzito nilimchukia mume wangu sina mfano. Ile kunusa harufu yake ilikuwa ni ugomvi mtupu."

"Basi mie mwenzio ndiyo nampenda kuliko hata kabla hajanioa. Mwenye bahati mbaya ni shemeji yangu Tujaribu. Sitaki hata kumwona mtu wa watu, utadhani ndiye alinisababishia yote haya!" Alisema Mateso.

"Basi, utazaa mtoto wa kiume atakayefanana naye. Hata hivyo, yote si kazi ya kaka yake." Alijibu Tunasota.

Wakiwa wanaongozana kwa maongezi na mwendo wao wa taratibu, wakipiga umbeya juu ya hili na lile, walikutana na Mama Maendeleo. Huyu ni mama aliyestaafu kazi ya ualimu ambaye huhamasisha wanawake wenzake kushiriki kwenye siasa.

Aliwaamkua na kusema, "Afadhali. Yaani, hata wajawazito leo wameamua kwenda kwenye mkutano!" Alisema kwa furaha akidhani wawili wale walikuwa wanaelekea kwenye mkutano wa dharura wa wakubwa.

"Mkutano. Mbona sikusikia ngoma wala mbiu ya mkutano!" Aliuliza Tunasota kwa mstuko.

"Mwaya huna habari!"Alijibu mama maendeleo.

"Kwani kuna uchaguzi tena mara hii?" Aliuliza tena Tunasota.

Mateso alidakia, "Mwaya hujasikia kuwa tunahaamishwa kupisha upanuzi wa mradi wa machimbo ya vito?"

"Makubwa haya, madogo yana wenyewe!"Alijisemea Tunasota.

Wakati Mama Maendeleo akijiandaa kujibu, Mateso aliwataka radhi wenzie, akaenda kichakani kujisaidia haja ndogo.

Mama maendeleo alianza kumweleza Tunasota kisa kizima, "Baada ya machimbo kutoa kodi kubwa na kugundulika kuwa kuna vito vingine vingi zaidi kwenye eneo hili la Githakwa,serikali iliamua wananchi wahame kupisha mradi huu wa maendeleo."

Kabla ya kumaliza Tunasota alidakia, "Wamejadiliana na nani. Mbona hii ndoa ya wawekezaji na serikali yetu inatisha. Kuna haja ya kufikiria kuivunja ili nasi wajawazito tujue hatima ya watoto wetu".

"Serikali ijadiliane na nani? Bunge lilikaa likajadili na kuidhinisha mradi huu upanuliwe hivyo wajibu wetu ni kutekeleza. Hujui kuwa ardhi yote ni mali ya serikali, sisi tunakodisha?" Alijibu mama maendeleo tena kwa kujiamini huku akitabasamu!

"Haiwezekani. Maana wakati wa uchaguzi tuliahidiwa na mbunge wetu kuwa angetuletea maendeleo. Nakumbuka maneno yake vizuri. Alitufundisha somo moja kuwa hii nchi ni yetu na sisi ndio waamuzi wa kila kitu. Sasa haya ndiyo maendeleo ya kututaka tuhame. Wapi uamuzi wetu kama wenye nchi?" Alilalamika Tunasota na kufunga vizuri upande wake wa kanga na kuendelea, "Yaani unataka kusema na mbunge wetu aliridhia mradi huu hata bila ya kutupa taarifa! Basi, atakuwa si mzima kiakili kama atakuwa amesahau au kupuuzia somo alilofundisha mwenyewe na tukamchagua."

"Mimi naona tusiandikie mate ilhali wino tunao. Wakubwa wako shuleni. Wameitisha mkutano kujadili hili. Hivyo twende mkawasikie wenyewe." Alishauri mama maendeleo.

"Tujadili nini iwapo uamuzi uliishapitishwa. Unatufanya kama hatuijui nchi yetu? Mama, wewe nenda, lakini, kipindi hiki siamini kama watu watakubali kuendelea kutumiwa kama daraja la Mto Shara." Alitahadhalisha Tunasota aliyekuwa anaonyesha wazi kuchukia na kujiamini.

Baadaye Mateso aliungana na wanawake wenzake kuendelea na safari.

Baada ya mama maendeleo kugundua kuwa somo lake halikueleweka, alijifanya ana haraka, hivyo, aliamua kukaza mwendo na kuwaacha

wenzie akiwaaga wakutane kwenye mkutano asijue wenzake hawakuwa na mpango wa kwenda kwenye mkutano!

"He, umemfanya nini huyu mama, mbona ametimka kiainaaina?" Aliuliza Mateso aliyekuwa ndiyo karejea kutoka kichakani.

"Mnafiki yule. Anataka kutufanya hatuoni na wala hatuna akili ya kujua mbivu na mbichi. Ukikiona hivyo ujue kimeishakatiwa chake. Si unajua wanasiasa wanavyojua kututumia wanawake kwa kutupa nafasi za uani" Alisema Tunasota.

"Usinikumbushe yale maazimio ya mkutano wetu kina mama. Una habari kuwa swali la kwa nini wanawake wanapewa viti vya upendeleo halikujibiwa? Baya zaidi utakuwa hata hivyo viti vinachukuliwa na watoto au wake wa wakubwa. Hukumbuki mwaya!" Alikumbushia Mateso.

Tangu utokee mtafaruku juu ya mwenzao, Riziki, kunyimwa nafasi ya kugombea Vitu Maalumu kwa ajili ya mama iliyochukuliwa na ndugu wa mke wa balozi, huwa hawana hamu na mikutano. Maana kwao, imani ni kwamba mikutano na uchaguzi wa Viti Maalumu ni danganya toto. Kwani wa kuwawakilisha anakuwa ameishachaguliwa na wakubwa kutoka miongoni mwa watu wao.

Baya zaidi hata huyo aliyepewa nafasi hiyo ya wanawake anaishi ughaibuni na mumewe ambaye ni balozi huko. Hivyo, hawana hata huyo mwakilishi katika hiyo serikali.

Kwao, mikutano ilishageuka kama kichekesho na kejeli. Maana hawajawahi kuona faida yake zaidi ya kuwapotezea muda na kuwafanya mateka wa wanasiasa. Maana kila mkutano ukifanyika, wanakijiji hujikuta wamepoteza muda wao kusikiliza na kulishwa uongo na upuuzi wa wanasiasa ambao ni hodari kusema mengi na kutotenda lolote kabisa.

Bado wanakumbuka kwenye uchaguzi wa Rais walivyoahidiwa mabati na mifuko ya sementi wasione hata kuti wala dongo!

17

Baada ya Mama Maendeleo kuachana nao Mateso na Tunasota wanaendelea na safari yao ya kuelekea kwa Matatizo.

Wanaendelea na maongezi yao juu ya hali ya maisha ya kijiji chao kinachokabiliwa na tishio la kubinafsishwa kwa mwekezaji kisirisiri.

"Mwaya, sina hamu na mambo haya. Yaani, kumbe serikali imeishajadiliana na kuamua kumuuzia mwekezaji ardhi na mali zetu kwa kisingizio cha maendeleo! Maendeleo gani yanahamisha watu kupisha vitu badala ya vitu kupisha watu. Yaani, tunaanza kutumikia vitu badala ya watu!" Alilalamika Tunasota huku akionyesha kukereka waziwazi na kushangaa.

"Mwenzio nilivyochoka naona haya yananichanganya kusema ule ukweli." Mateso alisema huku akichomoa dongo lake na kuanza kulimung'unya.

"Mwaya, hebu nipe dongo lau nikusaidie." Alisema Tunasota.

"Subiri wakati wako, acha kunichulia." Alijibu Mateso.

"Sitanii umenitamanisha udongo. Natamani nami niwe kama wewe, lakini mh! Maisha yenyewe yanavyozidi kuwa magumu, wenzio bado tunajiuliza". Alijibu Tunasota ambaye mtoto wake wa mwisho alikuwa amekuwa mkubwa kiasi cha kuhitaji mdogo wake, lakini, kutokana na ugumu wa maisha, bado walikuwa wanajadiliana kutafuta mwingine au la.

Hali hii ilimletea usumbufu sana. Maana licha ya mtoto kuwa mkubwa na mtukutu, bibi yake naye alishikilia waongeze, maana kila mtoto huja na riziki yake. Lakini, wao walikataa. Maana enzi za kila mtoto na riziki yake zilishapita kitambo kirefu.

"Sasa kama tunatakiwa kwenye mkutano ina maana mume wangu hatarudi haraka? Maana alikuwa na safari ya kwenda kwa mjumbe kujua kulikoni

halafu akabangaize pesa ya kuninunulia utumbo." Alisema Mateso huku akijivutavuta kupumzika kidogo ili baadaye waendelee na safari.

"Yaani, unakaa wakati matatizo ndiyo yanaanza!" Alishangaa Tunasota.

"Yaani, wewe nawe! Unajifanya hujui yanayonisibu! Unakuwa kama hujawahi kubeba mimba!" Alijitetea Mateso huku akitabasamu.

"Mwaya, najua, lakini, lazima ujikaze hivyohivyo. Maana kama hawa wakubwa hakuna anayejali watu kama sisi, sijui na huyo mbunge wa viti maalumu yuko wapi?" Alishauri Tunasota.

"Kama ni kujikaza ninajikaza sana. Una habari ninapika na kuchota maji! Vyakula vyote vya bwana namwandalia si usiku si mchana." Alizidi kujihami Mateso.

"Unataka kuniambia pamoja na hali hii bado mna....." Alikatiza alichotaka kusema. Akaangua kicheko.

Alipokuwa akijianda kuendelea na utani wake, alisikia mngurumo wa magari kuelekea upande wao. Alisogea pembeni ya barabara kupisha yale magari aliyosikia mngurumo wake. Watu wa vijijini kwa kuheshimu sheria za barabarani ni mahiri kuliko washamba wa mjini.

Msururu wa magari ulipita na wanawake wale wawili waliendelea na soga lao.

"Yaani, mkutano tu waje na PPK! Kuna kitu si bure" Alisema Tunasota ambaye wasiwasi wake haukumwingia Mateso ambaye alimrudisha kwenye soga yao juu ya kula.

Ila Mateso alicheka na kusema, " We mwendawazimu kweli. Muda si tatizo na pia kula ni muhimu, si unajua, tena kuzoesha tumbo. Unataka kuniambia kuwa wewe wakati ukiwa katika hali yangu ulikuwa huli?"

"Mwenzenu siwawezi. Yaani na shibe yote hii hujatosheka!" Alijibu Tunasota kwa kicheko.

Mateso alijibu kwa ufupi, "Ama kweli nyani haoni kundule! Nani atakataa vitamu hivyo? Lazima kula ili kuongeza virutubisho mwaya."

"Hujatosheka na virutubisho ulivyo navyo?" Alitania Tunasota.

Baada ya kuwa Mateso amepumzika vya kutosha, walianza safari kuelekea nyumbani.

Kutokana na Matatizo kutoonekana, Tunasota alimsaidia Mateso kumnunulia utumbo kutoka kwenye akiba yake ya vijisenti ambavyo hujidhiki kwenye bajeti yake ya chakula.

Wanawake ndiyo maana husemekana kuwa ni viongozi bora. Kwani huwa hawali kumaliza. Kwao kesho ina thamani kuliko leo tofauti na wanaume walio wengi ambao kesho yao ni baa.

Alipasua kuni na kumsaidia Mateso kupika huku wakiwa wanapiga soga kama kawaida wakijadili mambo mbalimbali kuanzia kilimo hadi siasa na umbeya mwingine.

Kwa Mateso pamoja na tishio la kuhamishwa, siku hiyo ilikwisha vizuri.

18

Baada ya Matatizo na Kilimwengu kufika shuleni ambako wanafunzi walikuwa wamekatishwa masomo kupisha mkutano, baada ya ngoma ya kuita kwenye mkutano wananchi kupigwa, walikuta baadhi ya wanakijiji wakiwa kwenye vikundi vidogovidogo.

Nyuso zao zilisema yote. Kwani zilipambwa na simanzi na mfadhaiko si kawaida.

Wakati wananchi wakijiuguza kuikubali hali ile, wakubwa waliokuwa wameishakaa kwenye meza za mbele, walikuwa wanaongea kwa tabasamu masuala yao ya kikubwa kana kwamba hakuna kilichokuwa kimetokea!

Kweli, kitanda usicholala huwezi kujua kunguni wake. Wangejua wanakijiji walivyokuwa wamechanganyikiwa angalau wangejifanya nao kuwa na simanzi.

Lakini, simanzi zingetoka wapi iwapo bwana Glutton Sucker, mwenye mgodi wa vito alikuwa naye kajiunga nao akiongea nao?

Wangechelea nini iwapo mradi wao ulikuwa ndiyo unazidi kupata mafanikio huku wakipitishiwa mabunda yao ya noti?

Bwana Glutton Sucker alikuwa amekaa karibu na Mkuu wa Mkoa, Gibbons Dikupatile, ambaye Mzee Njema alizoea kumwita Nyang'au, yaani, maana ya Gibbons kwa Kigithakwa. Pembeni alikuwa amejaa Mwenyekiti wa Chama cha MCC wa Mkoa na Katibu wake. Hawa kilikuwa hakiwezi kufanyika kitu bila wao kuwapo. Maana chama katika Mizengwe kilikuwa na nguvu kuliko hata hiyo serikali. Ungemuuliza mwananchi wa Mizengwe chama kipi na serikali ni ipi kama angekupa jibu basi huyo ni Rais au Katibu Mkuu wa Chama. Wengine walikuwa hawajui tofauti.

Alikuwa akiongea kwa furaha na Sucker huku wakiangusha vicheko. Inaonekana walikuwa wakiongelea jambo nyeti, kwani vichwa vyao

vilivyokuwa vimeungana na tabasamu zikipamba nyuso zao si haba. Maendeleo yalikuwa yamefika mwao.

Wakati Mkuu wa Mkoa na mwekezaji wakiongea kwa furaha, kwa upande mwingine Mzee Njema Waithaka alikuwa amechukia nusu ya kupasuka. Alikuwa kichwani akipanga jinsi ya kutibua ule mkutano bila kuchelea lolote ambalo lingemkuta. Maana angekuwa ametimiza wajibu wake.

Mkutano huo ulileta kituko kimoja. Kwani Mkuu wa Wilaya alivyokuwa akihamanika utadhani Mjumbe wa Nyumba Kumi. Alikuwa akikimbia huku na huku kama kiranja wa shule wakati wa ujio wa mkuu wa shule.

Hakika alidhalilishwa na kudhalilika vilivyo. Maana huwezi kuamini kuwa alikuwa ni yule bosi aliyewahi kuja kijijini akiwa anapanguswa hata vumbi!

Vikundi vidogo vya wananchi vilikuwa vikiangaliana kama kumwonea huruma, wengine kumshangaa. Ndirangu alimnong'oneza Chikwakwa aliyekuwa amekaa naye, "Huyu siku zote anajifanya bosi leo naye anatumwa kama mpagazi!"

Kutokana na kungoja mkutano uanze, maongezi haya yalikuwa mafupi. Chikwakwa alijibu, "Kuna ubosi pale au kujikomba na kudhalilishana. Lakini, naye acha alipe, maana huwa akija Ofisa Tarafa naye hutumikishwa."

Kutokana na mikikimikiki iliyokuwapo, walikatiza maongezi yao na kwenda kwenye mambo mengine kichinichini. Maana wangeonekana wanapiga kelele wangeshughulikiwa na dola. Vijijini Mizengwe watawala ni kama miungu hata wawe wadogo.

Mkuu wa Wilaya, Kapteni Mstaafu wa Jeshi, Mrongo Kumbakumba, mzee mwenye kipara, akiwa kwenye umri kama wa miaka hamsini, baada ya kuongea na Wajumbe wa Nyumba Kumi alionekana akiwa na Mama Maendeleo na Ofisa Mtendaji wa Kijiji wakiwa nao na kikao chao kisicho rasmi.

Tofauti na Mkuu wa Mkoa na Bwana Sucker, wao walionekana kama walikuwa wanapanga mikakati fulani. Isitoshe wao ni mabosi wangehangaishwa na nani wakati watumishi wao walikuwa wapo kazini wakionyesha utii wao.

Uongozi wa Mizengwe ni kama wa kuku. Maana jogoo mkubwa huwaamrisha kuku wote wa chini yake. Hivyohivyo hadi kifaranga ambacho katika hali hii alikuwa ni mwanakijiji wa kawaida.

Wanakijiji, kwa upande wao, licha ya kujadiliana kwa sauti za chinichini, walikuwa kama watazamaji. Maana wakati wakubwa wanatabasamu na kuongea kwa furaha, wanakijiji kila mmoja kwa wakati wake na namna yake, alikuwa akiongea na moyo wake nini hatima yake.

Wangefurahia nini iwapo ndiyo walikuwa wanauzwa kwa mzungu na kusalitiwa na Waafrika wenzao, tena waliokuwa wakidai ni viongozi wao, kumbe wakoloni weusi?

Kati ya watu wote, Matatizo alikuwa akitia huruma. Kwani mkewe Mateso alikuwa na majuma machache tu kujifungua kifungua mimba wao. Ndiyo hili pigo la kupisha mradi wa mgodi limeingia, alikuwa akiugua moyoni. Lakini, alikuwa imara akiwa tayari kwa lolote, hata kama angepaswa kupambana peke yake.

Mbunge, Harry ambaye watu wa Githakwa walizoea kumwita jina lake la utoto, Heri, ambalo hakulipenda, naye hakujivunga. Yeye alikuwa amekaa karibu na mhasibu wa Bwana Sucker, naye alikuwa Mzungu mwenzie aitwaye Selfishson Coloniere.

Nao kama mabosi wao, walikuwa na maongezi yaliyoonekana kuwa mazito, lakini, yenye neema. Maana meno yao yalionekana wakikenua kwa vicheko na kukubaliana katika hoja zao. Kweli, mwenye shibe hamjui mwenye njaa.

Pamoja na Bwana Sucker kukaa, usoni alionekana kama mtu aliyekuwa akizunguka kuangalia nyuso za wanakijiji waliokuwa na kila alama ya huzuni, chuki na kisasi ukiachia mbali kihoro na mshtuko.

Sucker, kwa kujua unyama aliokuwa ameufanya, alijikuta katikati. Kuna kipindi aliwaonea huruma wanakijiji kwa kuwa na viongozi mafisi na kuna wakati aliwalaumu kwa kuwa mabwege kiasi cha kutopigania haki zao.

Mwisho wa yote tamaa yake ya kupata utajiri na kuuvusha kwao ilikuwa ndiyo dira ya mawazo na matendo yake. Kuna kipindi alijisemea, "Nikiwahurumia mimi wengine hawatawahurumia."
Kupata naye hakujivunga. Pamoja na kuwa yeye si kiongozi, alikuwa amekaa meza za mbele. Angeshindwaje kukaa meza za mbele iwapo viti vizuri na meza zake zilizokuwa zimepangwa mbele viliazimwa kwake na isitoshe mbunge ni mwanawe.

Baada ya Mkuu wa Wilaya, Kumbakumba na Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Leopord Kuburuzwa na wajumbe wa nyumba kumi kujiridhisha kuwa watu waliokuwa wamekusanyika walikidhi idadi waliyoitaka, walitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa ili kuanza kwa mkutano.

Mzee Njema alizoea kumtukana Kuburuzwa kuwa yeye ni mpumbavu kwa kuitwa chui akakubali wakati hajui sababu zake.

Wananchi waliamrishwa kukaribia eneo la mkutano ili mkutano uanze.

Baada ya kuwa wamejikusanya, Ofisa Mtendaji wa Kijiji alisimama mbele ya meza kuu kumkaribisha Ofisa wa Tarafa, Tumikia Nauwale, amkaribishe Mkuu wa Wilaya ambaye angemalizia kwa kumkaribisha Mkuu wa Mkoa ambaye alikuwa ndiye mgeni rasmi na msemaji mkuu.

Alikohoa na kuanza kusema, "Mheshimwa Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa, Katibu wa Chama wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mbunge wa Mazonge, mwekezaji Mheshimiwa Sucker, Mkuu wa polisi, Ofisa Ardhi, wakubwa wengine, Ofisa Tarafa na ndugu wananchi."

Alikohoa kidogo ili kuiweka vizuri sauti yake na kuendelea, "Ninayo furaha, heshima na taadhima kuwakaribisheni Githakwa na kwenye

mkutano wetu wa leo ili kujadili masuala ya maendeleo na neema kwa taifa letu tukufu."

Aliendelea, "Mimi, leo si msemaji. Hivyo, sitachukua muda mwingi. Napenda kumkaribisha Ofisa Tarafa naye amkaribishe Mkuu wa Wilaya ambaye naye atamkaribisha mgeni wetu rasmi, mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kuweza kuhutubia mkutano wetu. Hivyo, Ofisa Tarafa, tafadhali karibu uchuke kipazasauti na kutimiza azma yako adhimu." Alimaliza huku Ofisa Tarafa aliyekuwa anatabasamu akijongea alipokuwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji.

Kitu kimoja kilitokea ambacho kilifanya hata meza kuu ishtuke kidogo. Kwani baada ya kumaliza hotuba yake fupi, Ofisa Mtendaji wa Kijiji alitegemea watu wangelipuka kwa makofi.

Ukiachia makofi ya mama maendeleo na baadhi ya walimu, wanakijiji hakuna hata mmoja aliyepiga makofi. Hivyo, wakati Ofisa Tarafa akishika kipazasauti alijikuta akiongezewa kibarua. Hawakupiga makofi utadhani walikuwa wameambiana wasifanye hivyo!

Alisema, "Jamani mpigieni kofi Ofisa Mtendaji wa Kijiji, lau nami nipate motisha ya kutimiza azma yangu adhimu." Alimaliza akiwa anatabasamu, akingoja kupigiwa kofi Ofisa Mtendaji wa Kijiji.

Utadhani wananchi walikuwa wameambizana. Hakuna aliyetii amri yake ya kupiga kofi. Mkutano ulikuwa na kila dalili za kutumbukia nyongo.

Tabasamu lililokuwa limeshamiri usoni lilitoweka haraka. Wasiwasi na hasira vilianza kuchukua mahali pake. Maana kitumbua chake kilikuwa ndiyo kinaanza kuingia mchanga.

Kuokoa jahazi, Ofisa Tarafa alianza kwa kuongopa, "Naona wazee mmechoka kutafakari kiasi cha kuwa mbali. Inaonekana mko hapa kimwili lakini si kiroho." Alimalizia.

Pamoja na kuyasema aliyosema kwa tabasamu la uongo, moyoni alikuwa na hasira na aibu kwa yaliyokuwa yametokea. Maana aibu hii ilikuwa ni kwa uongozi wote wa kijiji, wilaya hata mkoa.

Wakati haya yakiendelea vikundi vya wakubwa waliokuwa wakitabasamu vilionekana wazi kustuka na kutopenda hali ile. Kila mmoja alikuwa ametafsiri kitendo hiki kwa jinsi/namna yake.

Tafsiri moja ilikuwa sahihi kuwa mambo yasingekwenda yalivyokuwa yamepangwa au kutegemewa. Maana dalili za mvua ni mawingu na siku njema huonekana asubuhi.

Ghafla Mkuu wa Polisi aliamka na kwenda alipokuwa Ofisa Tarafa. Alimnong'oneza jambo Ofisa Tarafa. Ilikuwa ni kama kutoa onyo kuwa utovu wa nidhamu uliokuwa unaanza kuonyeshwa na wanakijiji ungeweza kushughulikiwa kipolisi.

Wakiwa wananong'onezana, wananchi nao waliangaliana kama kuambiana kuwa hakuna kupiga makofi.

Mzee Njema alionekana akiwa kahamasika kuwaonyesha wananchi ishara ya kukataa kupiga kofi. Lugha ya ishara ilitembezwa harakaharaka.

Mbunge naye hakubaki kwenye kiti chake. Aliamka ghafla na kuja kwenye kikundi cha walimu na kuongea nao. Baada ya hapo walimu walitawanyika kwenda kujichanganya na watu wengine. Inaonekana lengo lilikuwa ni kuwahimiza wanakijiji kichinichini wasionyeshe utovu wa nidhamu.

Pamoja na walimu kutii amri ya mbunge, wasingefanya lolote. Kwa vile wanawajua watu wa Githakwa kwa kulipiza visasi. Nani angepingana nao ili wageni watakapoondoka achomewe nyumba yake?

Mwalimu Msimamo alisikika akinong'ona chini kwa chini kuwaambia watu wa karibu yake. Alisema, "Liwalo na liwe, tusikubali kutumiwa au kusalitiana maana tumeishasalitiwa, lazima tupambane."

Ndirangu alisikika akijibu, "Huu ndio usomi na uzalendo kaka. Lazima tujikwamue kwenye tope hili la wezi hawa."

19

Baada ya kutawanywa kwa walimu kwenda kwenye sehemu walipokuwa wananchi, hakuna kilichobadilika.

Ofisa Tarafa ilibidi aanze tena salamu zake akitegemea kuwa mambo yangebadilika.

Alianza, "Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa, mheshimiwa Katibu wa Chama wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mbunge, mwekezaji mheshimiwa Bwana Sucker, Mkuu wa polisi, Ofisa Ardhi wa Wilaya, maofisa wengine na ndugu wananchi."

Naye, kama mdogo wake Ofisa Mtendaji wa Kijiji, utadhani ilikuwa sheria. Alikohoa kidogo na kuendelea huku mikono yake ikiwa inaanza kuloa kwa jasho.

Kwa sauti ya kukwaruza na kutetemeka aliendelea, "Napenda kwa furaha, heshima, utii, taadhima na matumaini kushukuru kwa kupata fursa hii kumkaribisha mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ili afanye kazi adhimu iliyotuleta hapa ya kumkaribisha mheshimiwa Mkuu wa Mkoa atuhutubie." Mara ghafla karatasi aliyokuwa akisoma ilidondoka!

Akiwa anatetemeka na kuhamanika, aliinama haraka na kuichukua ile karatasi na kuendelea, "Aaa, kama nilivyosema, kazi yangu si kuhutubia bali kumkaribisha Mkuu wa Wilaya amkaribishe mgeni rasmi. Lakini, kabla ya kumkaribisha Mkuu wa Wilaya naomba kutoa hadhari. Ndugu wananchi,tuepushe kuonyesha picha mbaya kwa wageni wetu. Maana tutaonekana kama si waungwana na wakarimu kwa wageni. Kwanza tushukuru kupata ugeni huu. Maana wapo wanaoulilia."

Alikohoa huku akitabasamu kwa kulazimisha na kuendelea, "Hivyo sitegemei kusikia kimya kama vile tuko kwenye msiba." Alisita kidogo kuruhusu amri yake na onyo alivyovitoa kama pendekezo kuzama kwenye bongo za wanakijji.

Aliendelea, "Kwanza akina mama pigeni vigelegele kuchangamsha wazee wanakijiji."

Kwa mstuko mwingine, kilisikika kigelegele kutoka kwa Mama Maendeleo tu! Hali hii iliwachanganya wakubwa kiasi cha kubaki vinywa wazi wasijue kuwa wale waliodhani ni kondoo walikuwa wameanza kutoka usingizini.

"Mwanakijiji mmoja alijisemea, "Tupige kofi kwa usaliti na uchafu huu? Kamwambie mkeo na wageni wako wakupigie kofi. Tutapigaje kofi wakati tunapigwa makofi?" Alisema kichinichini kiasi cha watu waliokuwa wamekaa karibu naye kutabasamu kwa uchungu.

Kwa fedheha na fadhaa Ofisa Tarafa aliendelea, "Kama hivyo ndivyo mmeamua kuwakaribisha wageni, tusilaumiane tutakapopewa jina baya." Alijifanya kutabasamu na kuendelea, "Naomba hivyohivyo nimkaribishe mheshimiwa Mkuu wa Wilaya atukaribishie mgeni wetu tayari kutupa mawili matatu yenye manufaa kwetu na taifa letu tukufu."

Aligeukia meza ya wakubwa na kuinama kuashiria utii na kumpa uwanja Mkuu wa Wilaya ambaye alikuwa anaonekana wazi kuchukia na kutahayari. Lakini, angefanyaje iwapo kupiga kofi au kutopiga ilikuwa ni haki ya wanakijiji?

20

Mkuu wa Wilaya akiwa amepooza kwa kiasi fulani alisimama na kuanza, "Githakwa hoyee!"
Kimya!
"Githakwa mpooooo!"
Kimya! Mara hii tena walisikika Mama Maendeleo na baadhi ya walimu. "Tupoooo na hatuhami!" Sauti za watu kama sita zilisikika akiwamo Mzee Njema aliyesema, "hatuhami."

Kiasi fulani Mkuu wa Wilaya alipata moyo kuwa kumbe watu wanaweza kuona aibu na kumtoa aibu. Ila neno "hatuhami" alilosikia kutoka kwa mtu mmoja aliyeitikia lilimtia shaka. Lakini, hakulipa uzito. Alidhani ni wahuni wa kijijini. Maana kila sehemu watu wa namna hii hawakosekani. Alijipa moyo.

Aliendelea, "Angalau mpo na nimewasikia." Alikohoa naye na kuendelea, "Sina shaka kuwa mna kila sababu ya kuwa kimya ili kuweza kutafakari tutakayopata kutoka kwa mgeni wetu. Watu wa Githakwa nawajua". Alisema.

Aliamua kudanganya, "Ni watu wa manjonjo. Nakumbuka kabla hamjanifahamu nilipokuja kutambulishwa hapa,mlikaa kimya bila kunishangilia hadi nilipowahutubia."

Aliamua kwa makusudi kuhami kitumbua chake na kuendelea, "Nchi yetu yenye mamia ya makabila ina utamaduni na mila tofauti."

Kukohoa ilikuwa kama fasheni. Naye alikohoa na kuendelea, " Aaa, nchini Kameruni kuna kabila moja. Ukiwatembelea badala ya kucheka hulia!" Meza kuu japo wanajua kuwa wanadanganywa na kubwagizwa na siasa hawana mbavu.

Haijulikani walikuwa wakichekeshwa na uongo au kituko cha Mkuu wa Wilaya ambaye aliamua kuondoa aibu na kuhami kitumbua chake baada

ya kuona wananchi wameamua kufanya mgomo baridi. Pia, haijulikani kama vile vicheko vilikuwa vya kweli au kejeli.

Aliendelea huku akionyesha tabasamu la kulazimisha, "Siishii hapa. Katika nchi yetu ya Mizengwe, kuna eneo linaitwa Githakwa. Wanagithakwa wakikupenda wakikukaribisha hununa kama mnavyoona."

Watu hawana mbavu. Zamu hii hata wanakijiji walionuna wanacheka si kwa furaha bali kebehi kwa uongo wa mchana, tena ukitolewa na mtu mzima anayeitwa mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Ofisa wa Jeshi, mwakilishi wa Rais wa Jamhuri na makandokando mengine ya kisiasa!

Kinyume na welewa wake, zilisikika mbinja, miguno na vicheko vya kebehi ambavyo japo alijua, alivitafsiri kama kuchangamsha wanakijiji asijue wameamua kucheka na kupiga miluzi ili kupinga kauli yake kuwa wakikupenda hukupokea kwa kununa. Ni furaha gani huonyeshwa kwa kununa? Ni uzuri gani huonyeshwa kwa ubaya?

Sasa wamecheka. Mkuu wa wilaya atalitafsirije hili? Mtu angeweza kujiuliza. Kwa vile ni mwanasiasa, hakuna cha aibu bali kuhami kitumbua.

Aliendelea, "Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kama ada, kazi yangu leo si kuhutubia bali kwa taadhima na heshima kukukaribisha uongee na umati wako wa wakazi wa Githakwa."

Kuepusha kuendelea kuumbuka aligeukia meza ya mbele alipokuwa amekaa Mkuu wa Mkoa kuashiria kumkaribisha aongee.

Hakutaka kuendelea na kuongea ili kuepuka kuzidi kuumbuka. Isitoshe kulikuwa na kila dalili kuwa kibarua cha siku ile kilikuwa kizito kuliko wote walivyotarajia.

Hivyo, kwa kukwepa aibu zaidi, alimpa kipazasauti Mkuu wa Mkoa na kutimkia kitini kwake kushuhudia kitakachotokea.

Mkuu wa Mkoa, naye mtu mzima, aliyeshiba akiwa amevaa suti yake ya bei mbaya, alianza, " Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa, Mheshimiwa Katibu wa Chama wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Mwekezaji, waheshimiwa wengine wa meza kuu na wanakijiji, nina furaha kuwa nanyi leo katika siku hii adhimu na ya kihistoria kwa uchumi na maendeleo kwa taifa letu."
Aligeukia wananchi na kusema, "Githakwa motoooo!"
"Motooo na utawakaaaa!" Aliitikia mzee Njema.
Wengine Kimya na mshangao!
"Githakwa na maendeleoooo!"
Kimya!
Githakwa na maendeleooooooooo!
Mzee Njema peke yake alijibu, "Hakuna maendeleo kuna usaliti."

Mzee Njema yumo kwenye umri wa miaka kama hamsini na ushei hivi. Ni mzee anayeichukia serikali baada ya kustaafu asilipwe mafao yake.

Ni mzee aliyeanzia uasi wake wakati akisoma kwenye shule za wakoloni. Inasemekana hakumaliza masomo yake baada ya kummwagia wino mwalimu wa kizungu aliyetaka kumwadhibu alipoulizwa swali kuwa Malkia wa Uzungu ni nani? Alijibu kuwa ni mama mmoja mnyonyaji na changudoa na mvivu anayewatumikisha wanaume wajinga wanaojiona wajanja kiasi cha kukalia nchi za wenzao.

Bado huwa anasimulia alivyombadilisha rangi mzungu. Maana inasemekana baada ya kumtukania malkia wake, mwalimu wa kizungu alichukia hadi akaiva.

Baadaye mzee Njema alizoea kusema kuwa alimkaanga mzungu hivyo wazungu weusi walikuwa hawamtishi hata kidogo.

Pia, inasemekana kuwa wakati akifanya kazi alianzisha chama cha wafanyakazi na kuwashawishi kugoma ili kupewa heshima na haki zao.

Ni kati ya wale wazalendo wa kwanza kusoma kuanzia wakati wa ukoloni na kumalizia baada ya uhuru.

Huwa hanyoi ndevu zake, hata mara nyingine huwa hata hachani nywele zake. Hii kwake ni ishara ya uasi kutoa taarifa kuwa bado yuko utumwani.

Ni mzee asiyebabaika wala kubabaishwa linapokuja suala zima la kupigania ukombozi wa wanakijiji waliosahauliwa na serikali inayojiita yao.

Ni mkimya. Lakini, akipata mwanya ni msemaji mahiri na mwenye msimamo wa kihafidhina.

Baada ya mzee Njema kutibua salamu za Mkuu wa Mkoa kila mtu alipigwa na butwaa asijue nini kingefuatia.

Hata mama maendeleo aliyekuwa akijipendekeza aliona aibu na kuamua kunyamaza. Huenda aliogopa macho ya ukali kutoka kwa wananchi.

Maana alijua kuwa angeendelea kupingana na msimamo usio wa makubaliano ya wananchi si ajabu usiku angepewa majibu ya usaliti wake. Hivyo, naye pamoja na wale wachache walioitikia waliamua kunyamaza ili waone kitakachotokea. Maana kifo cha wengi ni harusi.

Mkuu wa Mkoa aliendelea kana kwamba hakuna kilichotokea, "Sitasema mengi. Kilicholeta ugeni huu mkubwa kwenu nadhani mlikwisha kutaarifiwa."

Kabla hajaendelea alisikia sauti ikihanikiza, "Kutuchuuza, kutuuza na kutusaliti kwa vipande thelathini vya fedha." Alijibu tena mzee Njema bila kujali uzito wa Mkuu wa Mkoa ambaye kwa watu wa kijijini hana tofauti na Rais!

Watu wote waligeukia ilipotoka sauti ile. Kumbe ni Njema! Mmoja alisikika akisema kana kwamba alitegemea hili.

Njema aliyestaafu baada ya kutumikia Jumuia ya Ushirikiano wa Kuunganisha Pesa za Ukanda wa Mashariki, miaka thelathini iliyopita. Hakulipwa hata senti tano ya mafao yake. Ana hasira na serikali kiasi cha kuwa mwenyeji wa kila chama cha upinzani katika Kijiji cha Githakwa.

Pamoja na Wanagithakwa kupenda vyama vya upinzani, wanaogopa chama tawala kitawasumbua. Kwa Njema hakuna kitu kama hicho. Bendera ya CCU inapepea nyumbani kwake usiku na mchana. Mwenyekiti wa kijiji aliwahi kutaka kumtisha aiondoe bendera. Mzee Njema alimtolea katiba ya nchi iliyoandikwa kwa kizungu, mwenyekiti alinywea.

Badala ya kumsumbua alikwenda kutangaza kijiji kizima kuwa Njema ni mwanasheria!

Mzee Njema pamoja na kisomo chake cha mkoloni ni mjuzi wa mambo. Anaijua historia ya nchi kuliko hata hao wanaojiita waheshimiwa.

Pia, akichukia huongea kizungu utadhani ni mzungu! Kwa Wanagithakwa kusoma ni kujua kuzungumza kizungu hata kama ni cha uongo na ukweli.

Ana hasira na serikali na yuko tayari kwa lolote mradi haki itendeke.

Wakati akijibu kuwa ni usaliti na uchuuzi wa watu wa Githakwa ananyanyua bendera ya chama chake cha CCU, yaani, Chama Cha UKOMBOZI! Duniani wawiliwawili. Kwani wapenzi na vibaraka wa chama tawala cha MCC, nao japo kwa uchache, walikuwapo. Hakuna aliyeamsha bendera wala aliyekuwa amekuja nayo. Pamoja na kukipenda chama chao, mradi wa upanuzi wa uchimbaji wa vito ulikuwa haukubaliki kwao. Maana haukuwa ukiwanufaisha. Ukiondoa viongozi waliokuwa wakineemeka na mchezo mchafu wa chama tawala, wanachama walikuwa wanafuata mkumbo tu.

Mzee Njema hangoji Mkuu wa Mkoa aendelee. Anaanza kupayuka, "Nyinyi si waheshimiwa wala hamstahili hata kuitwa robo ya waheshimiwa, bali majangili na wasaliti mnaochuuza roho na miili yetu, huku kwa unafiki, mkijidai ni ndugu zetu na wenzetu. Mzee Njema hana kituo.
Anaendelea kuporomosha makombora yake kabla hajatiwa nguvuni.

Anasema bila kumung'unya maneno, "Huu wizi mnaoupaka mafuta na kuuita utandawazi na uwekezaji si chochote bali ujambazi hata kama

unatendwa na wanaojiita wakubwa wakati ni wadogo kuliko hata nzi. Nyinyi ni watumwa wa wazungu wanaowakilishwa na mjakazi wao mnayemnyenyekea na kumwita Bwana Sucker ambaye kimsingi ni mwizi Sucker. Mlaaniwe na hila zenu na unafiki wenu. Mmegeuza matumbo kuwa vichwa! Na njaa zimekuwa ndiyo bongo zenu."

Mzee Njema alipoona polisi wanamwijia aliamua kusogea katikakati ya watu na kuendelea kuporomosha shutuma, "Tunajua kuwa hata vito vinavyochimbwa hapa ni mali ya wakubwa ambayo hutoroshwa kupita Zuga ambako mmejenga uwanja wa ndege kwa ajili hiyo. Tunajua kuwa mlimdhulumu Mzee Machungi aliyegundua vito hivi."

Anazidi kujichanganya kwenye watu na kuendelea, " Kwa nini kila kitu muwategemee wazungu? Yaani wazungu mmewageuza Mungu! Aibu, aibu. Tena wewe Mtalii unayeitwa Mbunge hupaswi hata kuja hapa. Wewe ndiye umekuwa kuwadi badala ya mwakilishi. Ulaaniwe na umetapakaa rushwa! Rushwa! Rushwa! Rushwa." Ili kufikisha ujumbe haraka alikuwa akibwabwaja kama mvua za masika.

Mbunge alipokuwa alikuwa ameduwaa na kufedheheka asiinue hata mdomo kusema. Maana yaliyosemwa na Mzee Njema yalikuwa ni ukweli mtupu ambaye hata kuku pale kijijini alikuwa akiujua.

Kabla hajamaliza risala yake isiyo rasmi na ya kushtukiza, PPK wameisha mtia mikononi. Anakokotwa kama kiwete. Maana anajaribu kughairi kukamatwa bila kosa kama anavyoamini.

Aliondolewa umatini akiwa amehanikiza akisema, "Haya yule si ana bunduki. Mwambie anipige risasi. Siogopi watu wapumbavu na woga kama nyinyi. Nipige risasi kama kweli wewe askari."

Aliendelea, "Mnawaogopa nini wananchi kama nyie si wezi? Nanyi askari hamna akili. Mbona na nyinyi ni maskini kuliko hata mimi, lakini, bado mnatumiwa kunikandamiza? Mimi sina mtindio wa ubongo kama nyinyi ambao kama mbwa mnalinda watesi wenu, wakizidi kutuibia na kutajirika, nyinyi mkizidi kuwa maskini na wala rushwa ndiyo muishi.

Acheni huo utaahira. Mnawalinda mbwa wanaowararua ndugu zenu na mama zenu. Mbwa hulinda mali nyingi lakini siku zote yu maskini!" Alighahamu kwenda akijibwaga chini huku akizidi kuhanikiza, "Sasa ni **Saa ya Ukombozi**. Wananchi tushikamane dhidi ya huyo Nyang'au na wenzake. Tushikamane na kusimama dhidi ya vibaka hawa wenye masuti. Huu ndio wakati wa ukombozi halisi kwa kila mtu hata wadudu! Badala ya kuniwinda mimi kila mmoja awinde roho na nafasi yake. Ajiulize anafaidi au kukosa nini? Ajihoji kwa nini anabangaiza badala ya kuishi. Tuuu..."

Mwishowe askari wa PPK walifanikiwa kumziba mdomo. Maana maneno yake yalikuwa makali sana. Hata hivyo, walikuwa wamechelewa sana. Maana maneno ya kejeli na ukali yalishasikika kwa waheshimiwa. Kama ni silaha basi ilikuwa ni nyuklia. Maana aliwaacha wakubwa wakiwa wameloa kwa aibu. Uzuri ni kwamba wananchi walikuwa wakiyasikia na kuzidi kupata nguvu na kuuona ukombozi ukiwadia kama mwizi bila hata kutarajiwa.

Maneno na vitendo vya mzee Njema, licha ya kuchafua hali ya hewa,viliashiria mengi. Lakini, kubwa kila mtu kwa nafasi yake alitekwa na kitendo cha ushujaa wa kuamua kusema bila kumung'unya wala kuchagua maneno.

Ndirangu alimwambia Chikwakwa, "Shujaa ametangulia. Je, zamu ya nani kutuongoza au nichukue usukani kidume?"

Chikwakwa alicheka na kunyamaza. Maana hakuwa tayari kujitokeza kuubeba msalaba wake, pia, alijua Ndirangu alikuwa anatania. Yeye ni kiongozi wa mitungi tayari. Ila kama si ulevi jamaa alijaliwa akili si mchezo.

Kwa Wanagithakwa waliohiniwa na tangazo waliloona kama tangazo la mauti, mzee Njema ni shujaa. Kwa Mkuu wa Mkoa Njema ama ni kichaa au anatumiwa na maadui wa amani na utulivu wa taifa lake!

Mzee Njema amefanikiwa kumshushua Mkuu wa Mkoa na kuonekana kama kituko mbele ya wanakijiji wenzake ambao wamepigwa na butwaa, lakini,

wakiunga mkono ujasiri wake ambaye siku zote walikuwa wanamchukulia kama aliyekuwa amechanganyikiwa. Kitendo hiki kilifanya wabadili mawazo yao juu yake. Maana kwa Wanagithakwa, msimamo huabudiwa hata kama hekima hutukuzwa.

"Hakika hili ni pigo kubwa na la kwanza dhidi ya wezi hawa wanaoitwa waheshimiwa. Je, hali itakuwaje huko mbele?" Hili ndilo swali lililokuwa likimsumbua kila shuhuda wa mapinduzi haya ya kifikira na vitendo. Wengine waliogopa Mzee Njema angenyongwa kwa kuvuruga amani na mshikamano wa kinafiki wa Mizengwe. Wengine, kama Mzee Njema, walipiga moyo konde na kusema liwalo na liwe. Maana Mzee Njema alizoea kuwaambia kuwa ni heri kufa umesimama kuliko kufa umepiga magoti. Heri kuwa mbwamwitu kuliko mbwa, tena koko.

Mbunge Heri alinyanyuka kitini kwake kuelekea jukwaani alipokuwa Mkuu wa Mkoa. Pamoja na kujikaza kisabuni, sura yake ilionyesha wazi mtikisiko na butwaa kwani yaliyokuwa yakijiri si haba.

Huku akiweka vizuri suti yake ya bei mbaya, aliinama na kumnong'oneza Mkuu wa Mkoa aliyekuwa naye kapigwa na butwaa kwa dafrao lililokuwa likiwafumkia.

Alisema, "Mheshimiwa huyu anasumbuliwa na njaa na ngoa ya kuachwa nyuma. Anahitaji msaada wa kuwekwa ndani na kushughulikiwa ili liwe somo kwa watu wanaoota mchana kuwa wanaweza kutuchezea wasijue hii ni serikali tena isiyolala. Lazima afundishwe kuwa serikali hii ni ya wananchi na hawezi kuwachezea wananchi."

" Huyu Mzee anatia aibu na ni adui wa maendeleo, mshikamano na amani ya taifa hili tukufu. Ni mbegu isiyofaa shambani." Alisema Mkuu wa Mkoa asijue paka alikuwa ameishatoka kwenye gunia!

Mbunge alimjibu, "Huyu Mzee ana matatizo. Ana ugomvi hata na kanisa la Mungu. Eti analishutumu kwa kutomuunga mkono kwenye uzushi wake wa uchafuzi wa mazingira. Amefikia kusema serikali na dini zinalala kitanda kimoja! Hajui hii ni serikali ya wananchi kwa ajili ya wananchi?"

Maneno ya mbunge yalisababisha watu kuguna huku Ndirangu akisema kichinichini, "Yenu ni serikali ya mbwamwitu vinyamkera, mbweha na mafisi."

Mara Mkuu wa Mkoa alimkaripia Mzee Njema kwa ukali asijue alikuwa anakwaa kisiki tena cha mpingo. Alisema, "Mzee, naheshimu sana umri wako. Lakini, ukitaka kucheza na serikali sitaangalia umri wako. Hujui hii ni serikali ya umma na sisi ni wawakilishi wa umma!"

Mzee Njema hakumkawiza wala kumkopesha. Alimpa kavukavu. Alisema, "Hii si serikali, ni kundi la manyang'au. Wala usiwasingizie wananchi. Kama ni wananchi nami ni mwananchi. Nami nawakilisha serikali ya wananchi hawahawa japo haiko rasmi. Hivyo, ndugu yangu usinitishe. Tukubaliane kuwa zenu zimekwisha. Hii ni arubaini yenu. Sina haja ya kukuficha wala siogopi kitu." Alichanganya na Kiingereza huku akiwaacha wananchi wakiwa hawana mbavu na mshangao.

Chikwakwa hakuwa na mbavu zaidi ya kucheka na kusahau masahibu yake maskini. Kweli, kicheko ni dawa. Maana ungemwona usoni ungedhani hakuwa mnadani akiuzwa kwa vipande thelathini na ndugu zake mwenyewe aliowachagua kwa kura yake mwenyewe!

Alijisemea huku akicheka, akimgeukia Ndirangu, "Ama kweli wajanja wamekutana. Leo lazima kieleweke kama ni kusuka au kunyoa. Lakini, wadudu hawa wamezidi kutudharau na kutugeuza majuha."

Maongezi ya Mkuu wa Mkoa juu ya tabia ya Mzee Njema hayakuwa marefu. Kwani kila mmoja alikuwa anafikiri jinsi ya kuokoa jahazi lililokuwa limekumbwa na dhoruba kali iliyosababishwa na mtu mdogo mwenye moyo mkubwa aitwaye Njema Waithaka.

Wakati Mkuu wa Mkoa na walaji wenzake wakitafuta jinsi ya kuliokoa jahazi lao lililokuwa likionekana wazi kuwa linazama, wananchi walikuwa wakibishana kichinichini juu ya nani msomi. Wote hata kama hawakuonyesha waziwazi, walikuwa nyuma ya Mzee Njema ambaye aliibuka kuwa shujaa aliyekuwa akidhaniwa kichaa na yeyote ambaye

hakuwa akimfahamu vilivyo wala hoja zake nzito na zenye mantiki na maudhui ya kutosha kumshawishi na kumwelimisha kila aliyemsikiliza kwa makini. Wanakijiji walihitaji ukombozi na **saa ya ukombozi** wenyewe ilikuwa inaingia kama mwizi.

Kitendo hiki cha kuwatolea uvivu wakubwa, tena mbele za wananchi, bila woga wala kujali, ambacho kingefuatia kilimfanya Mzee Njema aheshimike sana.

Kimsingi, mkutano ulikuwa unaanza kuvurugika. Maana maneno ya mzee Njema yalikuwa kama nyuki waliovamia msafara wa mazishi. Sura na maneno ya Mzee Njema vilikuwa kama ulimbo kwa wananchi waliokuwa wamechoshwa na kunyonywa na kudhalilishwa na watawala wasio na aibu wala huruma. Waliwachukia vilivyo. Lakini, nani angejitoa mhanga kufikisha ujumbe wao.

Kwa vile **saa ya ukombozi** na mkombozi vilikuwa machoni mwao, wanakijiji hawakutaka kupoteza nafasi hii adimu na adhimu. Kimoyomoyo kila mtu aliiomba mizimu yake iwasimamie waondokane na utawala huu mchovu na mchafu uliokuwa umegeuka kinyaa na kero kubwa kwao na mstakabali wao.

Mzee Christian Muumini alionekana akifanya alama ya msalaba huku akinong'ona maneno fulani ambayo hayakusikika. Alikuwa akimwomba Bwana Yesu amzidishie Mzee Njema ithibati awaokoe hata kama alikuwa haamini kwenye imani za kikoloni na kimapokeo.

Mzee Njema alifurahi na kufarijika pamoja na kutiwa mbaroni, moyoni alikuwa hajutii kitendo kile. Kwake kumwaga nyongo ya maovu iliyokuwa moyoni mwake lilikuwa ni jambo bora kuliko hata kuishi. Alizoea kusema, "Ipo siku isiyo na jina nitawatolea uvivu majambazi hawa bila kuchelea lolote." Kumbe siku aliyokuwa akisema ilikuwa imetimia. Hivyo asingehuzunika wakati alijiandaa muda mrefu kuipokea siku hii ya ukombozi.

Wanakijiji wote walipigwa na butwaa iliyochanganyikana na furaha.

Hakuna aliyetegemea hili wala hakuna anayeamini kuwa ujumbe tena mkali na kwa walengwa wenyewe ungefikishwa wakati mwafaka namna hii na mahali mwafaka na kwa mtu mwafaka.

Njema kajiandaa lini na vipi bila hata mtu mmoja kujua, hakuna anayejua! Hatua aliyochukua ilikuwa ikijulikana kwa watoto wake Ititu na Ithaka na saa nyingine mama yao Wacera binti Nkwapatira. Kama ni utume, basi, mkewe na wanawe walikuwa manabii na wafuasi wake wasioyumba wala kutishika. Walimwamini kwa kila nukta na hatua. Walikuwa ni kama wanafunzi watiifu ambao wangefanya lolote aliloamrisha mwalimu wao. Alizoea kuwaambia habari za mwanafalsafa Plato, akisisitiza kuwa gwiji huyu aliufia ukweli, lakini akafa akiwa huru. Mwanzoni walimchukulia kama aliyepagawa. Lakini, kadiri siku zilivyokwenda wakawa wakishuhudia ukweli wa mambo, walijikuta wakizama kwenye fikira na mtafaruko wa kutafuta jibu la masahibu yao na kuna kipindi Itutu na Ithaka walikuwa wakimtania baba yao kwa kumwita Plato wakati mama yao akiwakataza kumwita baba yao Pilato. Kwani mumewe hakuwa msaliti. Waliozea kumcheka mama yao kwa kuchanganya Plato na Pilato.

"Kawapiga bao la kisigino. Kafunika kuliko hata hao wanaoitwa waheshimiwa. Hawa si waheshimiwa bali ni wezi wa miwa tu hata waishiwa!" Alijisemea mwanakijiji mmoja.

Pia, kitendo cha watu kuanza kumshangilia, kiliongeza uzito wa pigo alilotoa Njema. Kwani watu walisikika wakisema, "Njema shujaa wetu. Njema shujaa wetu. Tuko nawe popote, tumechoka kuonewa, kunyanyaswa na kunyonywa."

Kweli, wananchi walikuwa sasa wameamua kusema, "Sasa basi." Japo hawakutamka kwa ndimi zao, sura zao zilisema kila kitu, tena kwa uwazi na usahihi uliojaa ithibati ya hali ya juu. Maana ule woga wa wanakijiji ghafla ulitoweka na kwenye nafasi ya woga ukakaa ushujaa na ithibati ya hali ya juu. Mzee Njema alizoea kusema kuwa kondoo akijitambua anaweza kumuua mbwamwitu, tena kirahisi na haraka. Mambo yalivyokuwa yakienda, wakati wa kondoo kuwaua mbwamwitu ulikuwa ndiyo umetimu, tena bila taarifa!

Wakati askari wa PPK wakimchukua Mzee Njema, akina Kili walikuwa wakianza kunong'ona wakipanga kumuunga mkono. Walifanya hivyo ili kuwashtukiza wakubwa ili kuwafanya washindwe kutawala matukio.

Matatizo alimnong'oneza Kili, "Mzee Njema kaisha uwasha moto, lazima tuuchochee usizimike. Hapa leo si mahali pa kudanganyana, kugeukana wala kuogopana, bali kutoleana uvivu. Kwanini tuwe mashahidi wa mnada wa kutuuza sisi wenyewe utadhani tu hayawani? **Saa ya ukombozi ni sasa.** Tuwaonyeshe wezi hawa kuwa tu dhaifu, lakini wenye mioyo mikubwa na yenye nguvu kuliko wanavyotuchukulia juujuu. Tuwaonyeshe kuwa sisi si kuku bali kunguru. Kwa vile mkeo ni mjamzito, mimi nitajitoa mhanga nawe huko nyuma ikibidi kutoa sadaka zaidi usisite. Kwani ni suala la muda tu". Alimaliza Kili.
Matatizo alijibu, "Kaka, nakuamini. Niamini niko tayari kwa lolote kuhakikisha kuwa saa ya ukombozi haiahirishwi wala kusalitiwa, iwe kwa lolote. Niko tayari kuliko awali."

Ujumbe huu, licha ya kumvutia na kumtia moyo Matatizo, ulimwacha hoi. Alipata hamasa na mori ya kusimama kidete bila kuchelea lolote kwa namna yoyote!

Alisema, "Liwalo na liwe. Saa ya ukombozi ni sasa. Sasa hivi na sisi hawa hapahapa."

Kili alitikisa kichwa kwa furaha kama alama ya kukubaliana na msimamo na hakikisho la rafiki na mpiganaji mwenzake. Mambo yalianza kuchukua sura mpya ya ufanisi usiokuwa wa kawaida. Ama kweli mja akiamua hakuna limshindalo.

Pamoja na kuchanganywa na mambo jinsi yalivyojifunua, Matatizo alielewa haraka mwelekeo wa upepo. Alichofanya ni kugonganisha mikono na Kili kuonyesha kuwa amemwelewa na kumuunga mkono. Wote utadhani walikuwa wameambizana, waliinua mikono ya kulia ikionyesha alama ya V ambayo ilitafsiriwa kama alama ya ushindi na ithibati katika mapambano.

Wahenga walisema kuwa ujiti mmoja wa kibiriti huteketeza msitu mzima hata uwe na ukubwa sawa na nchi.

Baada ya PPK na polisi kumweka ndani Mzee Njema walidhani kitendo hicho kingekuwa somo na onyo kwa wanakijiji waliokuwa wamebakia.

Hivyo, baada ya sakata na vumbi la mzee Njema kutua, Mkuu wa Mkoa aliendelea na hotuba yake akiwa amejiridhisha kuwa onyo limepokelewa. Bila kujua kuwa alikuwa amegonga mwamba!

Hivyo, kwa hadhari ya hali ya juu aliamua kwenda moja kwa moja kuelezea kilichokuwa kimemleta Githakwa. Hata hivyo, moyoni alikuwa anajilaumu kwa kutumia njia ya kushtukiza kama njia rahisi ya kuzuia wananchi kujadiliana kiasi cha kupinga mradi mzima. Hata hivyo, hakuwa na jinsi ikizingatiwa kuwa yeye na wenzake walijitahidi kuwa na idadi ndogo ya wahusika ili wapate migao mikubwa kuliko kuwa na watu wengi ambapo migao ingepungua.

Baya zaidi, hata majigambo kuwa bunge lilikuwa limepitisha mradi huo ni uongo. Kwani "bunge" lililokuwa likiongelewa ni yeye, Bwana Sucker, Mbunge, Mkuu wa Wilaya, Maofisa Ardhi wa Mkoa na Wilaya na wenzao wa madini, viwanda, uwekezaji na serikali za wilaya walioamua kwa tamaa, hila na uovu kuidhinisha dhuluma hii. Maskini, hata Rais na Waziri Mkuu hawakuwa na habari, ingawa lawama zote zilielekezwa kwao! Wangekuwaje na habari wakati nao kwa namna yao walikuwa wakihangaika kujiingizia pesa kwa njia haramu na haraka kwenye nafasi zao? Kwa Mizengwe, kila kitu kilikuwa ni kama mchezo wa vurugu ambapo huwa hakuna kanuni wala refa. Kila mtu huupiga mpira ajuavyo, awezavyo na atakavyo. Serikali iligeuka kuwa sirikali iliyokuwa imeficha vurugu zisizo za kawaida za kuuhujumu umma ambao haukuwa na habari wala hatia! Hali ilikuwa inatisha sana. Maana wale waliokuwa wameaminiwa na umma kuujenga ndio walikuwa wamekazana kuubomoa!

Rais au Waziri Mkuu wangejuaje wakati udhaifu wa Rais ulikuwa unajulikana kuwa ni kupelekewa taarifa za uongo na wapambe na wachumiatumbo na kuziamini bila kufanya utafiti?" Walijua jinsi ya

kuutumia udhaifu huu. Walikuwa wanamvizia ima alipokuwa na ugeni mkubwa au ziara ya nje na kumpelekea masuala mazito yaliyohitaji uamuzi mzito. Yeye alimwaga wino asijue anamwaga damu ya watu wasio na hatia! Mzee Njema alizoea kumwita ajali ya kihistoria na kisiasa. Maana ukiangalia alivyokuwa akitengeneza historia chafu na kusababisha ajali kimaisha kwa wananchi, hakika Mzee Njema alikuwa amepatia kwa kuchagua sifa mwafaka.

Baadhi ya wachumiatumbo na wapambe wengine si chochote wala lolote. Ni vijikundi vya vijiweni na wacheza bao ambao kutwa nzima hujadili umbeya usiokuwa na msingi wowote. Ili kumpiga chenga Rais, vikao kama hivi vya Githakwa vilikuwa vikifanyika wakati Rais akiwa nje ya nchi.

Viongozi wa Mizengwe baada ya kuvuruga uchumi na huduma zote za jamii, hawakuwa wakitibiwa nchini mle. Hata mafua walienda kutibiwa ugenini pamoja na wake zao na watoto wao. Hata watoto na wajukuu wao hawakusoma Mizengwe. Walisoma ughaibuni kwenye elimu ya maana. Maana walihakikisha wanaivuruga elimu ili wawe na wajinga wengi wa kutawala na kunyonya wakiwatumia kipunda na kimbwa kama walivyotaka.

Ughaibuni ilikuwa kama ndiyo kwao. Maana walitumia muda mwingi huko kuliko nchini Mizengwe. Licha ya kutibiwa kule, watoto walikuwa wakienda kuwatembelea watoto wenzao waliokuwa wakisoma kule. Wakati ule kusomesha watoto nje ilikuwa kama mashindano kwa kila mwenye nafasi. Maana hata wale watoto waliokuwa hawajiwezi kiakili walipelekwa nje na kurudi na shahada tena za kuheshimika. Wapo waliokuwa wakishuku kuwa shahada hizi ama zilikuwa za kughushi au zilitokana na vyuo vilivyojali kuchuma pesa kutoka kwa mabwege matajiri.

Hivyo, wezi hawa walijua jinsi ya kuutumia udhaifu huu. Walijua jinsi upashanaji habari vijijini ulivyokuwa wa taabu ukiachia mbali utambuzi na elimu juu ya uraia na haki za raia.

Hakika, wahujumu hawa waliwekeza kwenye hali hii ili kujichumia pesa kwa kuwatesa wananchi wasijue akina Njema na sasa Kilimwengu nao walikuwa na namna yao ya kuwafichua waovu hawa.

21

Mkuu wa Mkoa alianza hotuba yake kwa vitisho. Alisema, "Ndugu wananchi, kwanza kwa dhati kabisa na huruma ya aina yake nawashauri mmpuuzie huyo mzee. Ana matatizo yake na hajitakii mema wala hawatakii mema. Ametumwa huyo na maadui wa mshikamano na maendeleo ya taifa letu tukufu. Tunajua mabwana zake ni nani."

Licha ya kupigwa na butwaa, wanakijiji hawakuamini kama uchafu huu ulikuwa ukitoka kinywani kwa mtu aliyeitwa mheshimiwa na kiongozi.

Ndirangu alisikika akisema, "Lo! Huyu alifaa awe kuli, si Mkuu wa Mkoa. Hii ndiyo hasara ya kubambikiwa watawala." Naye Mzee Njema alisema, "Mimi nimetumwa na mabwana zangu, nanyi mmetumwa na matumbo yenu na roho mbaya na ulafi kama wa fisi."

Mkuu wa Mkoa alijifanya kama hakusikia alichosema Mzee Njema. Aliangalia upande alikokuwa akipelekwa Mzee Njema na kusema, "Nina hakika yeye na mabwana zake waliomtuma aje kupiga kelele hapa hawatafanikiwa. Maana wananchi wa Mizengwe tumeshikamana na tuko tayari kwa lolote kulinda uhuru na mafanikio ya taifa hili tukufu. Nina imani kubwa na wananchi wa Githakwa. Githakwa hoyeeee!"

Hapakuwa na mwitikio zaidi ya watu kucheka kwa kejeli huku wengine wakitikisa vichwa kwa masikitiko na dharau.

Ndirangu aliguna kichinichini na kumtazama Mwalimu Msimamo aliyekuwa naye kaudhiwa na uongo ule. Msimamo alimwambia Ndirangu, "Kumbe siku hizi tunatawaliwa na wahuni na wanaotumia midomo kufikiria badala ya ubongo. Huyu kazidi. Maana huwezi kutofautisha maneno yake na ushuzi tena wa maharage yaliyogaga. Hakika kama mambo ni haya tumekula hasara, tena sana. Nakwambia."

Mkuu wa Mkoa alicheka na kuendelea, "Ndugu wananchi, nataka nieleweke vizuri na vilivyo kuwa sikuja hapa kufundishwa kufanya kazi ambayo licha ya kuisomea nimeifanya kwa zaidi ya miaka ishirini. Pia, sikuja kushuhudia watu wakicheza na serikali. Tena serikali, wendawazimu hawa wanayotaka kuichezea, ni hii yenye kutaka kuwaletea maendeleo haraka na kwa kila gharama."

Wanakijiji waliguna kuonyesha kutoukubali uongo huu wa mchana kweupe.

Alisita kidogo kupima mwitikio wa wasikilizaji wake huku polisi wakiwa wameishajichimbia katikati ya wasikilizaji ili kuzuia aibu nyingine isitokee.

Aliendelea, "Kumbuka mimi na mkubwa kwenye serikali yenu ni wanajeshi tena wenye nishani. Mimi ni mwakilishi wa Mtukufu Rais kwenu. Hivyo nisingetaka mtulazimishe kutoa makucha."

Alitabasamu na kuwaangalia watu ambao pamoja na kutoa vitisho vyake walikuwa wametulia, utadhani hawakuwa wakimsikiliza zaidi ya kunong'ona kwenye makundi yao walipokuwa wamekaa.

Baada ya kuridhika kuwa wanakijiji wanamfuatilia kwa makini, aliendelea, "Lengo la kuja hapa, nasisitiza si kufundishwa kazi na wajibu wa kila mmoja wetu ambao hauna mjadala, ni kusikiliza na kupokea uamuzi. Kama mlivyotaarifiwa ni kwamba kutokana na siasa yetu ya ubinafsishaji, uwekezaji na ujenzi wa uchumi wa kimataifa wa kisasa, serikali yenu imeamua mradi wa uchimbaji wa vito upanuliwe. Nasisitiza, hili halina mjadala. Kinachotakiwa ni utekelezaji tena haraka. Huu ndiyo uzalendo."

Aliendelea, " Kwani licha ya kuonyesha dalili za kukwamua uchumi wa nchi yetu,umezalisha kodi kubwa ambayo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu. Hivyo, kuhama kama mlivyotaarifiwa si suala la hiari, bali ni amri halali ya serikali."

Alikohoa na kuendelea, "Inasikitisha kuona kuwa kuna watu, tena wendawazimu hawa, miongoni mwenu hawataki maendeleo! Hawa ni maadui wa taifa na ni tishio kwa mshikamano wetu. Narudia, hawa wanatumiwa na maadui wa taifa hili tukufu. Tusiwavumilie wala kuwapa nafasi kujaribu upumbavu wao."

Akiwa anajiandaa, Kilimwengu aliamua kumtolea uvivu, kumwonyesha kuwa hila zake hazitafanikiwa. Alipaza sauti na kusema, "Hata aje Rais mwenyewe hahamishwi mtu. Mtahama nyinyi na wezi wenzenu, lakini si sisi wenye ardhi hii kihalali tuliyorithishwa na Mizimu na mababu zetu walioteseka hata kufa kupigania uhuru mnaoufaidi na sasa kuzidi kiasi cha kuturejesha utumwani."

Utadhani yeye na Mzee Njema walikuwa wameambizana. Kilimwengu aliropoka harakaharaka ili polisi watakapomtia nguvuni awe ameishafikisha kilio chake na ujumbe wake kwa walengwa.

Aliendelea kupayuka, "Mwaka jana tulikichagua chama chenu kwa ahadi kuwa matatuletea maendeleo. Haya maangamizi ndiyo tafsiri yenu ya maendeleo? "Wananchi msikubali kuuzwa nyinyi na hata ardhi yenu. Heri kufa tukipambana kuliko kuishi tukinyenyekea. Kama tulivyoonyesha mshikamano tangu mwanzo, tusiogope na kukubali kugawanywa. Hawa mnaowaona mbele yetu ni watumwa wa matumbo yao yaliyowapeleka kwa wazungu kutuchuuza roho zetu. Hawana lolote la maana. Kataeni uongo na unafiki wao. Ni chui kwenye ngozi ya kondoo hawa. Wanataka kututia pingu na kutuswaga kutupeleka kutuchinja, si watu hawa."

Wakati akiendelea kubwabwaja aliona polisi wakielekea alipokuwa. Alianza kukimbilia katikati ya watu ambao kwa sura ya nyuso zao walionekana kukubaliana na maneno yake. Maana alipita kirahisi bila kuzuiliwa. Moto aliouwasha Mzee Njema sasa ndiyo ulikuwa unasambaa. Maana kwa kumkamata Njema walidhani wameuzima. Kumbe ni kata mti panda mti.

Kilimwengu aliendelea, "Tuna taarifa kuwa huu ni mpango wenu unaotoka kwenye matumbo yenu ambayo yamegeuka serikali. Hata

serikali yenyewe haipo. Maana kama ingekuwapo ingetulinda badala ya kuwaruhusu mfanye mnavyotaka kwa kisingizio chake. Katu msiendelee na ndoto za mchana kuwa mtafanikiwa kuiuza Githakwa. Leo tumeamua. Saa ya Ukombozi ni leo na sasa hivi. Lazima..."

Hakupata tena muda wa kusema, kwani polisi waliishamzunguka na kumkamata huku wakimziba mdomo.

Kilimwengu mtu aliyejaliwa mwili miraba minne hakukamatwa kirahisi. Purukushani na mshikemshike ulitokea hadi mwishowe polisi walipomzidi nguvu na kumwondoa kwenye mkutano.

Mkuu wa Mkoa aliendelea kana kwamba hakuna lililokuwa limetokea. Ingawa alionyesha kujiamini moyoni, kiroho kilikuwa kikimdunda. Rafiki yake, Bwana Sucker alikuwa kanywea kama mbwa aliyenyeshewa na mvua. Lile tabasamu aliloingia nalo kwenye meza kuu lilishakimbia na nafasi yake kuchukuliwa na sura ya kuchoka na kukata tamaa. Mkuu wa Wilaya na Mbunge na maofisa wengine ndio usiseme. Walionekana kabisa kuchaganyikiwa na kuogopa. Kwani dalili za mvua ni mawingu. Hawakutegemea kuwa wanakijiji, tena wa mabondeni Githakwa, wangalikuwa na msimamo na welewa kiasi hiki. Kitumbua, taratibu kilianza kuingia mchanga. Hili lilikuwa wazi kwao na kwa wanakijiji. Hivyo, kila upande ulianza kuvuta kamba kuelekea kwake.

Mkuu wa Mkoa aliendelea na hotuba yake, "Waheshimiwa wananchi, msijali sana hawa ni wapinga maendeleo wachache wanaotaka kuvuruga maendeleo yetu ya kijiji, wilaya, mkoa na taifa. Lakini, nawahakikishia serikali ipo na hailali. Hawatafanikiwa. Wanaota, tena mchana kweupe. Aliyewadanganya kakosea sana."

Aliiweka vizuri suti yake na kuendelea, "Hivyo, nisipoteze muda. Nimekuja rasmi kutoa taarifa kuwa mtasaini mkataba wa kuhama kwa kuweka saini na vidole gumba ili kudhihirisha kuwa mmekuwa wananchi wa kwanza kuonyesha uzalendo kwa kuunga mkono mipango ya maendeleo ya serikali na mtafanya hivyo katika kipindi cha siku tisini yaani miezi mitatu." Asanteni.

Hapakuwa na cha kofi. Alirejea kwenye kiti chake na kungoja kusikia maoni ya wananchi kuhusiana na ujumbe wake.

Sura za wananchi zilikuwa zikionyesha kila alama ya shari na kutaka kupambana. Kulikuwa na kila dalili kuwa wananchi wangezinduka kwenye woga na kupinga dhuluma hii iliyokuwa imo mbele yao bila kujali chochote.

22

Kabla hata ya kukaa kitini vizuri na kutoa nafasi ya kupokea maoni, mikono kama sita ilikuwa imenyooshwa.

Mkuu wa Wilaya alimteua Kamanda wa Polisi wa Wilaya kupokea maswali akidhani kuwa kutokana na magwanda yake angewatisha wananchi kutoa dukuduku zao asijue kuwa walikuwa wameishakamia kujikomboa na kulikomboa taifa lao kutoka kwenye makucha ya waliowaona kama wakoloni weusi. Hakujua kuwa walikuwa wanaichukia serikali waliyoiona kama zigo la kawaida. Serikali waliyohisi ikiwanyonya damu na kuwadhalilisha sana.

Kamanda huyo alinyanyuka kwenye kiti chake na kwenda mbele kupokea hoja za wananchi.

Mpaka leo Matatizo hajui alikopata ujasiri siku ile. Kwani alikuwa amenyoosha mkono na bahati nzuri kamanda alianzia kwake.

Matatizo aliamka kwa hamasa na kujiamini na kuanza, " Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kabla ya kupokea maoni yetu lazima tukubaliane jambo moja. Hatuwezi kutoa maoni yoyote bila ya wenzetu wawili waliokamatwa kwa kutoa maoni yao. Je, mnataka tutoe maoni gani iwapo tukitoa maoni tunatishwa na kukamatwa? Bila hawa kurejeshwa mimi naona wanakijiji hawatakuwa na sababu ya kutoa maoni. Hivyo, basi, tukubaliane kuwa kwanza waletwe na mtusikilize, si mtuamrishe kama wanyama. Nyinyi mna maoni na sisi tuna maoni. Lazima tujadiliane, kukubaliana au kutokubaliana na maoni yetu yaheshimike. Kwani hii ardhi ni mali yetu si ya serikali wala mtu yeyote isipokuwa sisi na Mungu. Nisingependa ionekane kama mnatulazimisha kuhama." Kabla ya kuendelea alisikia sauti kutoka kwa wanakijiji wakisema, "Warejeshwe kwanza! Warejeshwe kwanza na hatuhami! Hatuhami."

Ujanja wa kupamba sumu yake kiasi fulani ulimlainisha Mkuu wa Mkoa na kukubaliana na mawazo ya Matatizo asijue ndiyo alikuwa anajikaanga yeye na wenzake.

Mwamko na mshikamano huu ulianza kuwatia shakani wakubwa. Mbunge alikuwa kinywa wazi asiamini kuwa yaliyokuwa yakitokea yalikuwa kweli zaidi ya ndoto! Isitoshe anamfahamu Matatizo kama mtu aliyejaribu kuzamia meli na kushindwa, ukiachia mbali kujua kuwa mdogo wake alikwenda sekondari kwa jina lake. Wale watu aliokuwa akizoea kujisifia kuwa wanaweza kula hata mawe kwa ajili ya kununua mafuta yake ghafla walikuwa wamegeuka. Wale aliodhania ni misukule walikuwa sasa wamejitambua na kuamua kujikomboa kwa dhati na namna ya ajabu!

Wakati mwingine akiwa bungeni alizoea kujisifu mbele ya wenzake kuwa ni bingwa wa siasa ambaye hata angewambia watu wake kula majani hata mawe kwa ajili ya mafuta ya gari lake wangefanya hivyo bila kuuliza tena kwa kunyenyekea na kuona kama wameheshimiwa. Kwake wapiga kura wake walikuwa kama shamba la kuchumia kura kwa ajili ya kula tena kwa mrija ilhali wao walikuwa wakifa njaa wakati nchi yao ilikuwa na ardhi yenye rutuba. Walizoea kuletewa vyakula vibovu vilivyokuwa vikiagizwa nje, wakiuziwa kwa bei ya kulanguliwa. Mzee Njema alizoea kuwaita kuku ambaye hula asichozalisha na kuzalisha asichokila. Yeye hutaga mayai yenye protini. Huishia kulishwa minafaka mikavu na ya daraja la chini kabisa.

Mzee Njema alikuwa akiilinganisha serikali ya Mizengwe na mbwa anayekula vitoto vyake kutokana na uroho wa nyama. Alizoea kusema kuwa mbwa wa namna hii dawa yake ni kumpiga rungu na kumtokomezea mbali. Alizoea kusema kuwa serikali yenye tabia hii haifai kuwapo popote duniani.

Wakati fulani shemeji wa Mbunge aliwaambia kuwa hata kama ni kula majani, wananchi wayale, lakini punda wa mfalme angenunuliwa. Wakati ule bunge lilikuwa kwenye majadiliano makali ya kununua punda wa Rais kwa ajili ya kupanda akipokea wageni mashuhuri waliomtembelea kwenye Ikulu yake ya kifalme iliyokuwa ikikarabatiwa kila mwaka kwa

mabilioni ya kwenje. Wakati akimpa hakikisho shemeji yake ambaye ni Waziri wa Fedha alitumia mfano huu. Wanasiasa wa Mizengwe walikuwa ni watu wa kukufuru. Kuna mmoja aliwatukana wananchi wa jimbo lake kuwa wanaishi kwenye vijumba ambavyo hata teke la kuku linaweza kuviangusha! Mzee Njema alizoea kuwaita misukule isiyojitambua wala kuwatambua waliokuwa wamewaroga.

Kutokana na hoja ya kuungana na akina mzee Njema na Kilimwengu ilimkata maini hata Kamanda wa Polisi wa Wilaya aliyejikuta amemtumbulia macho Mkuu wa Mkoa aliyekuwa anaonekana kuchoka kabisa huku akichanganyikiwa.

Maana alijua wazi kuwa kama hali hii haitazuiliwa kulipuka na kufika ngazi ya taifa, basi licha ya kupoteza kazi atakuwa amepoteza uhuru na ulaji wake. Alihofia kuozea kifungoni, ila alijipa moyo kuwa, kwa vile kila kiongozi alikuwa mwizi kwa namna yake, basi, angeonewa huruma. Maana binadamu ameumbika na aibu.

Kwa hali ilivyokuwa ikionekana, ni kwamba hata wakubwa wenzake waliishaanza kumsukumizia yeye mzigo. Hata bwana Sucker alianza kuonekana mwenye shaka, uchovu hata majuto. Kwani, katika muda huu mfupi alikuwa ameishasindikizwa msalani si chini ya mara tatu. Simu yake ilikuwa ndiyo usiseme. Alikuwa akipiga simu muda wote hadi Mkuu wa Mkoa kushtuka. Maana hakuwaamini wawekezaji. Wanapopatwa na tatizo wanaweza kumpigia simu hata Rais, aliwaza moyoni. Lakini angefanyaje iwapo hakuwa na uwezo wa kumwamuru Sucker azime simu yake?

Kugunduliwa kwa teknolojia ya simu za mikononi kuna faida na hasara zake. Wakati malumbano yakiendelea, mtoto mwingine wa mzee Njema, Ititu alikuwa kwenye choo ya wanafunzi akichungulia kilichokuwa kikiendelea. Alikuwa ameishapiga simu kwa waandishi wa habari mkoani ambao nao waliwasiliana na wenzao wa Fikira ili kuja kupata ripoti za kilichokuwa kikijiri.

Pia, kuruhusiwa kuanzishwa vyombo vya habari vya binafsi nako kuna uzuri wake. Kwani mhariri wa gazeti la upinzani, *The Politicos,* aliamua kukodisha helikopta kuwawahisha waandishi ili kuliripoti tukio hili.

Kwa vile mwekezaji mwingine kutoka India, mmilki wa helikopta, alikuwa rafiki wa chama tawala, waandishi wa habari walichelea angegoma kuwakodisha helikopta yake. Hivyo, walivalia kama madaktari waliokuwa wamekodisha ndege kama shirika lisilo la kiserikali kwenda kuokoa maisha ya watu waliokuwa wameungua moto kwenye kijiji kimoja mkoani Zuga.

Hivyo, hapakuwa na pingamizi juu ya kutoa kibali cha kukodishwa kwa ndege yake, asijue alikuwa ameipiga mshale serikali yake mwenyewe ingawa haikuwa ikihusika moja kwa moja ukiachia kuachia madaraka na sifa ya serikali kutumiwa vibaya na maofisa wake wabadhilifu kama huyu Mkuu wa Mkoa ambaye arubaini yake ilikuwa ikimnyemelea kwa kasi.

Hapa ndipo upande wa pili wa kuruhusu baadhi ya taasisi na vyombo kumilkiwa na watu binafsi kulipoonyesha faida zake.

Maana wakati wa zamani hakuna mtu ambaye angeruhusiwa kumiliki vyombo hivyo.

Pamoja na serikali kupata pesa nyingi kupitia kodi kutoka kwa mashirika ya ndege binafsi, kwa upande wa pili sasa helkopta hii inatumika kama nyenzo ya kurahisishia wapinzani wa serikali kuipiga mishale huku ikiwanufaisha wapinzani wa sera hii kufikia lengo lao.

Yaani, siasa za siku hizi ni kama puto. Kuna wakati zinatumia mazingira yaliyopo kujipanua na wakati mwingine matokeo yake yanazihujumu zenyewe kama ilivyo katika kisa hiki cha upanuzi wa mradi wa vito wa Githakwa.

Ukiachia mbali waandishi wa habari wa gazeti la upinzani, pia wanaharakati wa haki za binadamu kutoka taasisi inayojitegemea ya haki za binadamu na wanasheria wanaopambana na uchafuzi wa mazingira iliyoitwa Kamati

ya Kupigania Haki za Binadamu na Mazingira, nao waliandamana na msafara huu wakijifanya madaktari.

Kila kundi lilikuwa na ajenda yake ingawa viliunganishwa na kitu kimoja, yaani kutoridhika na serikali ilivyokuwa ikifanya mambo na ubadhirifu uliokuwa umekithiri. Waandishi wa habari walitaka kutimiza wajibu wao kuwa sauti ya wasio na sauti na wanyonge waliokuwa wakinyanyaswa na wanaotumia madaraka vibaya.

Pia, walitaka kuizindua serikali kutoka kwenye mazoea na usingizi wa kuwaachia watu madaraka wasiyojua kuyatumia. Walitaka serikali ijue kuwa kupeana vyeo kama njugu kulipa fadhila au kuwatafutia ndugu na marafiki ulaji ilikuwa vibaya.

Pia, kwa kufichua uchafu huu, licha ya kuifanya serikali iwaamini, ingesaidia kuonyesha umma kuwa vyeo vilikuwa vikitolewa ama kwa ukereketwa wa chama tawala au kwa kujuana na mambo mengine kama hayo.

Kwa upande wa wanaharakati wa haki za binadamu na mazingira, lengo lao lilikuwa ni kuweka bayana kilio cha wanyonge na jinsi wanavyoathiriwa na sera zinazotungwa na mataifa makubwa na kulazimisha mataifa maskini kuzitekeleza ili watu wake waweze kuishi.

Vyama vya upinzani, ingawa havikuwa na mwakilishi, vilikuwa vinategemea kutumia udhaifu huu kama turufu kwenye uchaguzi ambao ungefanikiwa. Pia, vingetumia mkasa huu kama suto kwa wananchi waliovinyima kura kutokana na kutokuwa na mfuko wa kuweza kuwahonga kama chama tawala kilivyofanya.

Pia, ujumbe huu ulilenga kuwafichua akina Bwana Sucker na Mkuu wa Mkoa waliokuwa wakitumiwa na kampuni za kigeni zenye pesa na ushawishi kuhujumu rasilimali na haki za wananchi.

Maana haikuwa tena siri kuwa karibu serikali nzima ilikuwa inaanza kuwa mikononi mwa wawekezaji, hasa matapeli walioidanganya na kuitumia vibaya kuibia watu maskini wa Mizengwe huku wakishirikiana na maofisa

wachache wa serikali waliokuwa hawana uadilifu wala uchungu na nchi yao.

Wakati kashfa hii ikitokea, kulikuwa na kashfa nyingine nchi jirani ambapo mmoja wa wakubwa wa nchi alikuwa ameingizwa mjini kwa kuridhia kuleta kampuni ya kuua magugu ambayo wala haikuwa na utaalamu wala kampuni ya kuua wadudu bali kuchonga vyuma.

Kampuni hiyo ilimhonga mkubwa mmoja na kujipatia mamilioni ya dola huku isifanye kitu chochote zaidi ya kuishia mitini, ikimwacha mhusika katikati. Maana alitaka kuwaonyesha wananchi alivyo kwenye madaraka kwa ajili yao huku akipaswa tena kuwatumikia wawekezaji ambao matakwa yao na ya wananchi yalikuwa sawa na panya na paka.

Hivyo, ujumbe huu pamoja na kulipa mamilioni ya pesa kukodi helikopta, ulikuwa na uhakika kuwa dunia nzima ingejua madhara ambayo nchi changa kama Mizengwe zilikuwa zikiyapata kutoka kwa nchi za kinyonyaji na koloni. Hili pia lingeisaidia serikali kuwabana nchi wafadhili kuhusu jinsi kampuni za nchi hizi zinavyotumia vibaya utandawazi na uwekezaji uliokuwa umegeuka utandawizi na uchukuaji vilivyoanzishwa kuwanyonya wananchi wa nchi changa.

Kwa vyama vya upinzani huu ulikuwa ni ushindi mkubwa. Kwani pamoja na udhaifu vilivyokuwa nao, vingepata hoja ya kuwapelekea wananchi kuhusu kufanya mageuzi ya kisiasa ambayo katika nchi ya Mizengwe yalikuwa midomoni na vitabuni tu.

Ili kuhakikisha zoezi hili linafanikiwa, mabingwa wa mikakati walishauri daraja la Mto Chania livunjwe ili kuzuia msafara wa Mkuu wa Mkoa kutoroka kutoka Githakwa kama ikitokea wakachelewa na wahalifu wakawa wamenusa harufu ya mpango wao.

Daraja lenyewe lilikuwa la mbao nne zilizoanza kuoza lililojengwa wakati wa mkoloni. Hivyo, spana ya kufungulia nati na mtu mwenye kujua kuitumia vilitosha kuimaliza kazi hiyo, tena kwa muda mfupi.
Kazi hii alipewa Ititu ambaye alifungua nati harakaharaka bila mushikeli. Ilikuwa rahisi sana kwake na wala haikuchukua muda.

Baada ya kufungua nati zote, Ithaka alizisomba mbao na kuzipeleka mbali chini ya mkondo wa mto uliomsaidia kuzifunika. Kwani zilizama majini. Aliamua kuzitunza ili baada ya vita kwisha zirejeshwe na daraja liendelee kuwahudumia wanakijiji ingawa wangeweza kuvuka hata bila ya kuwapo mbao hasa msimu huu wa kiangazi.

Japo Ititu siku zote alikuwa akilaumu serikali kuzisahau sehemu za vijijini, siku hiyo aliona madhara ya hali hii ambayo kwake ilikuwa nyenzo ya ushindi wa vita vyao.

Kuondolewa kwa daraja hilo kulisaidia waliokuwa ndani ya healikopta kumkuta Mkuu wa Mkoa na ujumbe wake na kuwahoji wananchi kuhusu matukio yaliyokuwa yametokea kwenye kijiji chao.

Mambo yalipangwa na kupangika ukiachia mbali kuwa yalifanyika kwa muda mfupi kutokana na kuzidiwa kete na Mkuu wa Mkoa ambaye licha ya kufanya ziara ya kushtukiza alikuwa amefanikiwa kuifanya siri.

Hata wasaidizi wake ofisini, ambao hakuwaamini, hawakujua mpango mzima wa kuhujumu wananchi wa Githakwa.

Maana si wote ofisini walikuwa wakiridhika na hujuma ambayo wananchi wa kawaida walikuwa wakifanyiwa na wale waliowaamini, tena kwa kura na imani zao.

Kwa bahati nzuri, hata Mkuu wa Mkoa hakujua kuwa wakati akijaribu kutimiza azma yake, walikuwapo watu angani wakikimbilia Githakwa kumvua nguo ili Rais amfukuze kazi na kumfunga vizuri. Maana Rais siku zote alikuwa akisisitiza kuwa wananchi wampelekee taarifa za watendaji wake wanaowatilia shaka tayari kuwashikisha adabu.

Hivyo, huu ungekuwa ni mtihani wa aina yake ambao ungepima ukweli wa maneno na matendo ya Rais ambaye alikuwa akilalamikiwa na wananchi kwa kuwalinda wahalifu, hata walipompelekea taarifa kwa siri. Hii sasa isingekuwa siri. Hivyo, angeona aibu na kuwajibika kuwajibisha wahusika.

23

Huko nyumbani kwa Matatizo mambo yalikuwa shwari kwa Mateso. Kwani baada ya kuutandika utumbo alionunuliwa na Tunasota, aliamua kujilaza.

Mara usingizi ulimwiba kiasi cha kuuchapa fofofo asijue mumewe alikuwa msambweni. Aliamshwa na kelele na vilio vya Tunasota aliyepokea habari za masahibu ya waume zao. Hivyo, kumtaka ajikongoje waelekee kujua kulikoni.

Pamoja na tumbo lake, alijizoazoa kuelekea shuleni kujua kuliko kutokujua atasaidiaje kutuliza zilizala lililokuwa limemnyang'anya mumewe bila kutarajia. Maana kwa wanakijiji kushtakiwa au kukamatwa na polisi hakuna tofauti na kuhukumiwa kifungo, tena cha muda usiojulikana.

Hali ilikuwa mbaya zaidi ukizingatia na uzito wa ugeni na suala lililouleta ugeni ule kijijini.

Ingawa hakuwa na taarifa kamili, habari alizozipata kuwa kulikuwa na mtafaruku zilimtosha kuhakikisha kuwa Matatizo alikuwa matatani. Maana alimfahamu mumewe kwa misimamo yake na hasira juu ya maisha waliyokuwa wakiishi kutokana na unyonyaji wa watu wachache.

Hivyo, alikaza mwendo akimfuata Tunasota kama mtoto amfuataye mzazi mwenye hatua za kikubwa ikilinganishwa na hatua za mtu mzima. Alijikaza kisabuni na kupiga moyo konde kuwa wangeushinda mtihani huu.

Pamoja na kuhamasika kwenda shuleni, wawili hawa hawakujua pa kuanzia na kumalizia. Ilimradi walikuwapo waume zao na wana wajibu wa kuwalinda na kuwaonyesha kuwa wapo kwa ajili yao, wawili hawa hawakuchelea lolote wala chochote. Maana rafiki wa kweli ni yule akufaaye wakati wa dhiki.

Wakiwa wanaelekea kwenye mkutano ambao hawakuwa na mpango wa kuhudhuria, walikutana na watu waliokuwa wametokea kule wakikimbia kuchelea ambayo yangetokea. Kilichowapa moyo ni kwamba watu wenyewe hawakuwa wengi. Wengi walikuwa wafuasi wa Chama cha Wote (CCW), kilichokuwa kikitawala taifa la Mizengwe wakati ule.

Kawaida katika maisha hasa ya vijijini, kuna wale watu wenye tabia kama za kware. Kware aliambiwa akafugwe na binadamu, akasema heri nile kidogo kuliko kingi cha kunitenganisha kiwiliwili na shingo.

Kwa akina kware kuonekana woga, lakini mwisho wa yote wakaishia kucheka, lilikuwa jambo la maana tofauti na akina Mateso ambao kufa na umpendaye ulikuwa ni wajibu.

Hata hivyo, akina kware ni kama walikuwa wakicheza mchezo wa mbuni kumwona adui akaficha kichwa chake kwenye ubawa wake. Maana suala zima la kuhamishwa lilikuwa linawachanganya ukiachia mbali kukimbia hatima ya mkutano.

Hivyo, nao kama tumbo walikuwa katikati. Maana ukiliuliza tumbo wewe rafiki yako ni yupi kati ya miguu na kichwa haliwezi kukujibu.

Wakati Mateso na Tunasota walikuwa wakijiwahi kujua hatima ya waume zao, Ithaka mtoto wa mzee Njema, alikuwa akifanya kazi mbili. Kuhakikisha polisi hawamfichui kwenye maficho yake, pia ujumbe wake unafika na pia baba yake haumizwi. Hata hivyo, hakuwa na wasiwasi na baba yake. Maana kama ni kuteseka alikwishamaliza mateso yote. Kukaa kwenye umaskini wa kutengenezewa kwa miaka zaidi ya thelathini kunataka moyo.

Kama ni shida, alishazizoea kiasi cha kuzifanya rafiki, ingawa shida hazizoeleki. Kwake mambo yalikuwa tofauti. Maana shida zilimfundisha kupata faida kutoka kwenye hasara. Shida zilimfundisha kuvumilia na kufikiria.

Shida zilimfukuza woga kutoka kwenye maisha ya mzee Njema na badala yake zilimkaribisha ithibati kuchukua mahali pake. Hii ndiyo siri ya

kujitoa mhanga kwa ajili ya wanakijiji na ardhi yao. Kwa mzee Njema, kufa na kuishi, tofauti yake hakuiona wala hakujua tofauti ya kufurahi na kuhuzunika.

Ukiachia kudhulumiwa kwa miaka thelathini na ushei, Mzee Njema, hata wakati akisoma kipindi cha ukoloni, alikuwa akichukia historia iliyokuwa ikifundishwa wakati ule. Maana ilikuwa ikimsifia malkia wa Uingereza na kumfanya mtu mweupe kuwa mkombozi wakati kwake alikuwa ni shetani mkubwa na mwangamizaji wa dunia.

Licha ya kumtukana malkia na kummwagia wino mwalimu wa kizungu, kulikuwa na habari kuwa mzee Njema alikataa hata kubadilishwa jina na kubatizwa huku akiaminishwa kuwa Malaika ni mweupe na shetani ni mweusi. Habari hii hadi leo inasimuliwa, tena kwa heshima kijijini Githakwa na pote alipofanya kazi.

Mzee Njema, pamoja na kusahaulika kwenye duru za kisiasa, ni mmojawapo wa vijana wachache wakati ule waliosaidia kueneza siasa za kudai uhuru katika Kijiji cha Githakwa. Bahati mbaya, kutokana na msimamo wake usioyumbishwa na kiu yake ya haki kwa wote hata baada ya kupata uhuru, wale aliowasaidia walimtelekeza kwa kuogopa angewawia kisiki.

Kitu kingine kilimponza Mzee Njema. Licha ya kuwa na msimamo usioyumbishwa alijaliwa ithibati na uwazi. Hii ndiyo ilimfanya asifanikiwe kwenye siasa baada ya uhuru. Kwani hakuwa tayari kutumika au kufanya jambo ambalo dhamira yake ilipingana nalo.

Zaidi ya hilo, kutokana na kujua na kujiamini kwake, hakuwa tayari kufuata jambo lolote kwa mkumbo. Mzee Njema hakuwa akiuamini utawala uliopokea uhuru kutokana na kutokuwa huru na kupuuzia mambo mengi aliyoona muhimu.
Jambo hili lilimfanya afarakane na siasa za baada ya uhuru, hasa pale alipotaka walowezi wote waliokuwa wameletwa na mkoloni kuhujumu harakati na uchumi wa nchi kuondoka na mkoloni aliyewaleta. Alipogundua kuwa hakueleweka kwa watawala wapya, wala kusikilizwa na walikuwa wameridhia kuwapa uraia, alianza kuwaambia watu wa karibu na wale

waliokuwa na mawazo kama yake, kuwa hapakuwa na uhuru bali kubadili wakoloni kutoka wakoloni weupe kuweka weusi.

Maana hadi Mizengwe inapata uhuru, mzee Njema hakuwa akishabikia upande wowote kati ya magharibi na mashariki. Yeye hadi atakapozikwa anaamini kuwa Waafrika walikuwa na mfumo wao wa utawala ambao kama usingehujumiwa na kutokomezwa ungewafikisha mbali kuliko hapa walipo.

Mzee Njema aliwaacha hoi Wanagithakwa alipokataa kulipa kodi ya maendeleo. Alimwambia mtoza kodi, tena kavukavu kuwa asingelipa kodi ya maendeleo ya matumbo ya wakubwa na hawara zao! Alizoea kuwaambia waziwazi kuwa yeye hakuwa msukule wala kondoo wa kuwanyenyekea mafisi na mbwamwitu waliokuwa wamevaa ukuu waliozoea kuuchafua. Kuna kipindi alimwambia Ofisa Mtendaji Kata kuwa vitendo vya serikali ya Mizengwe vilikuwa vinachukiza sawa na makaburi ya watakatifu kufagiliwa na wazinzi na wauaji!

Ithaka alizidi kuwasiliana na ujumbe aliokuwa anajua utamwokoa baba yake. Bahati mbaya mawasiliano yake yalitumbukia nyongo. Kwani baada ya kupaa hewani ili kutosumbua mawasiliano ya helikopta, simu zilizimwa. Hivyo, alipoteza mawasiliano kiasi cha kuanza kuwa na wasiwasi.

Kitu kilichompa faraja ni habari kutoka kwa kamanda mwenzake kama walivyozoeana kuitana, yeye na kaka yake Ititu, aliyemjulisha kuwa daraja lilikuwa mengele!

Habari hii ilimzidishia matumaini na ithibati ya kuwa wangeshinda mapambano na kuzizika dhuluma zilizokuwa zinawataabisha na kuwaaibisha. Kwani hata ujumbe kutoka Mji Mkuu wa Fikira ungechelewa hata baada ya wiki ungemkuta mheshimiwa mtegoni tayari kumhoji. Maana kama angefanikiwa kutoroka magari yangekutwa tu darajani.

Mara moja wazo lilimjia kuwa kama wageni kutoka Fikira wangechelewa basi usiku wangeyahujumu magari yale.

Ili kuhakikisha kuwa mbinu yake inafanikiwa, Ithaka alimshauri Ititu kuongeza na misumari kwenye sakafu ya daraja ili kama watajaribu kulazimisha magari kupita yatoboke magurudumu na kuishia kukwama katikati ya mto bila kuvuka ng'ambo yake. Ititu alitumia ujuzi wa medani aliokuwa ameupata kwenye mafunzo ya mgambo wakati wa vita vya kukomboa eneo moja la Mizengwe lililokuwa limevamiwa na nchi jirani ya Udanga miaka michache iliyokuwa imepita.

Wakati maji yakizidi unga kwa Mkuu wa Mkoa na ujumbe wake wakijikuta kwenye tafrani, polisi walijikuta, bila kujua, wakizidisha ushindi kwa akina mzee Njema. Kwani licha ya kutokuja na wataalamu wa makosa ya jinai na kuhoji, hawakuwa wamejiandaa kwa hali iliyotokea.

Baada ya kuwatia nguvuni mzee Njema na Kilimwengu, licha ya kuwafungia kwenye chumba cha nafaka cha shule, hawakuwatenganisha. Kosa kubwa. Hivyo kwa watu wenye msimamo, matatizo na mawazo yanayofanana, hali hii ilikuwa ni fursa nzuri ya kufahamiana na kupanga mikakati ya pamoja, jambo ambalo walilifanikisha kwa ufundi mkubwa.

Ukiachia mbali kufahamiana kama wanakijiji wa kijiji kimoja wenye kukutanishwa na koo zao, kwenye ndoa au asili, ni watu waliokuwa wamejaliwa ithibati na uwezo wa kuamua haraka kama ilivyotokea kwenye kukamatwa kwao. Maana hawakuwa wamewasiliana kabla, ukiachia mbali kukutanishwa na mkasa wa kutaka kuhamishwa na kuburuzwa.

Hivyo, kuwamo kwao chini ya paa moja kulikuwa ni fursa nyingine ya kuboresha mbinu ya mapambano yao dhidi ya watu wachache wasiojua thamani ya dhamana zao na nafasi zao.

Hivyo, basi, kama mateka wa vita, walipeana moyo na mikakati harakaharaka wakigawana majukumu.
Kwanza, walikubaliana kutotoa habari yoyote juu yao wala kutoa fursa ya mahojiano yoyote na polisi hata kama wangepelekwa wilayani au mkoani.
Pili, walikubaliana kugoma kula hata kunywa wakishinikiza waachiwe kwanza na madai yao kutambuliwa huku wakiombwa msamaha.

Walikubaliana kutokubali kuacha madai yao hadi mpango mzima ufutwe.

Hapa ndipo mara ya kwanza Kilimwengu alijua kuwa kumbe Mzee Njema alikuwa akijua kila kitu kuhusu usaliti huu. Kwani alimwelezea mpango mzima na wahusika wake na jinsi ambavyo serikali kuu haikuwa na habari na hujuma nzima. Hivyo, walijua kabisa kuwa ujumbe wa Mkuu wa Mkoa haukuwa na mamlaka kisheria hata kuwafungulia mashtaka.

Hili lilimwongezea Kilimwengu ari na ujasiri wa kusimama kidete. Maana alijua mwisho wa yote, ili kuepuka bomu kulipuka, mpango mzima ungefutwa na wanakijiji wangeamua kulifikisha suala zima kwenye ngazi ya kitaifa kutokana na viongozi wa upinzani kuwa na maslahi nao, ukiachia maslahi ya wanakijiji na wapiganiaji haki za binadamu na vyombo vya habari ambavyo kwa zaidi ya miaka kumi vilikuwa vikitahadharisha na kupinga zoezi zima la ubinafsishaji, uwekezaji, utandawazi na jinsi masuala haya yalivyokuwa yakitekelezwa kiwiziwizi.

Pia, kulikuwa na mgogoro wa katiba ya nchi kutokwenda na wakati. Watawala, kwa bahati mbaya hawakuwa tayari kuukubali ukweli na kuukabili. Hii kwa mzee Njema ilikuwa ni fursa pekee ya kurekebisha hali ya mambo mengi. Hivyo, kufumka kwa mgogoro na kukamatwa kwao ilikuwa ni sherehe na dalili ya msingi ya mafanikio ya ndoto zake.

Mzee Njema alisema, "Hii ni arubaini ya uzandiki, unyang'au na ubabaishaji unaofanywa na watu wachache kwa kusingizia serikali. Pia, litakuwa somo kwa serikali kuwa makini na watu wake."

Siku zote aliwazia na kutamani kuukosoa mfumo mzima wa siasa zilizoitwa za kisasa wakati zilikuwa na matokeo ya kizamani kwake, yaani, unyonyaji, ukoloni na utumwa, ukiachia mbali uchumiatumbo, ubadhirifu na wizi wa fedha ya umma wa watu maskini wa Mizengwe.

Kwa muda waliokaa korokoroni pamoja, mzee Njema na Kilimwengu walijikuta kama samaki wa aina moja kwenye bwawa moja. Walijilaumu kwa nini hawakukutana mapema kubadilishana vipaji, ubongo na misuli. Kwani walijikuta wakitofautishwa na umri, lakini waliunganishwa na

misimamo na dhamira.

Lilipokuja suala la kupigania haki, walikuwa ni pacha. Ama kweli duniani wawiliwawili. Kwao ilikuwa Githakwa wawiliwawili. Mzee Njema na Kilimwengu na Mateso na Tunasota!

Baada ya kuwa wamekubaliana kufanya mgomo wa kutoa habari na kula, Kilimwengu alijikuta anapata faraja zaidi kutokana na ushupavu na mipango ya Mzee Njema ambaye tangu siku ile alikuwa akimwita baba ili kuonyesha heshima na shukurani zake kwa kuwakomboa wanakijiji wenzake akitumia uzoefu wake wa mapambano kutafuta haki tangu wakati wa ukoloni.

Naye mzee Njema alimzawadia Kilimwengu jina la Dalibunga ambalo ni jina la ukoo la shujaa kama ishara ya kutambua mchango wake.

Pamoja na Kilimwengu kujulishwa juu ya serikali kutokuwa na habari ya mpango huu ukiachia mbali maofisa wake waroho, alijulishwa kuwa kulikuwa na ujumbe wa waandishi wa habari na watetezi wa haki za binadamu ambao ungeuvamia mkutano ule pale kijijini na kusambaza habari za mateso na hujuma ambazo Wanagithakwa walitaka kufanyiwa ili kutoa onyo kwa serikali iliyokuwa imelala.

Ili kumpa moyo zaidi Mzee Njema alisema, "Najua watu wengi wasiojua vizuri siasa wamekuwa wakinichukulia kama mwehu wakati wehu ni wao waliokuwa wamekubali kudhulumiwa na kutishwa na kikundi cha wezi wachache, tena wababaishaji na waoga wa kawaida."

Alitabasamu na kuendelea, "Saa chache zijazo Githakwa itajulikana dunia nzima kutokana na kafara hii tunayoitoa mimi na wewe."

Kilimwengu alijibu, "Ni kweli baba. Maana hata mtume Modimu wa Githakwa kuna kipindi aliambiwa alikuwa na mapepo."

Kumbe mpango mzima wa kuwahamisha Wanagithakwa ulikuwa umefikiwa baada ya kugundua kuwa sehemu ya Wamuyu walipokuwa

wakiishi wanakijiji haikuwa kwenye ramani ya kijiji iliyochorwa na serikali ya kikoloni.

Haikuwa sehemu huru kama kijiji bali kitongoji ndani ya Kijiji cha Githakwa kilichokuwa kimegawanyika katika maeneo matatu, yaani, Wamuyu, Shera na Githakwa yenyewe.

Hivyo, katika kupanga mpango mzima, wahusika walikuwa wakilijua hilo. Walichokuwa wakitarajia kufanya ni kuwahamisha Wanagithakwa kutoka kwenye eneo la Wamuyu na Githakwa kilimani huku wakimega msitu wa Kololo karibu na Githakwa kuu na Shera.

Hivyo, hawakuwa wajinga. Walijua kuwa utakuwa ni uhamisho wa ndani kwa ndani ambao serikali isingeujua zaidi ya kupelekewa taarifa ya upanuzi wa mradi. Hii, ikichangiwa na tabia ya viongozi wa serikali kuangalia upande mmoja wa mapato, kama ingefanikiwa, akina Gibbons wangeishia hata kupandishwa vyeo.

Hii ndiyo ilisababisha hata wasipoteze muda kushirikisha serikali kuu wala kuhangaika na masuala ya kulipa fidia ya maana.

Wezi hawa walikuwa wamepanga kuwapa pesa kidogo wananchi kwa ajili ya kuanzia maisha ilhali walikuwa wamemkamua mamilioni Sucker ambaye kutokana na faida aliyokuwa akiipata kwa kutorosha madini, bado ilikuwa ni kama njugu tu.

Pia, walikuwa wamekubaliana kuwa kama wananchi wangeleta malalamiko juu ya udogo wa fidia, basi, Sucker angeongezea kiasi fulani cha pesa kutegemea ambavyo wangekubaliana. Hii ilikubaliwa na Sucker baada ya kudanganywa kuwa mgao wa Rais na mawaziri usingepunguzwa ili kuhofia kubadili mawazo juu ya jinai nzima.

24

Huko nyuma Mkuu wa Mkoa akiwa kwenye kitatange cha kupingwa na wananchi, tena wadogo, ambao hakuwategemea, alikuwa akijiandaa kujibu hoja za wananchi.

Imani yake ilikuwa ni kwamba wale waliowagomesha wananchi baada ya kuwa wamewekwa, wananchi wangerudisha utii kwa serikali. Hivyo, kujadili mpango mzima ambao kimsingi ilikuwa ni kuwalazimisha kuhamia eneo la pili kwenye kitongoji cha Shera, sehemu ya msitu wa Kololo jirani na Nthethe, kwa gharama ndogo kwenye kijiji hichohicho cha Githakwa, kuliko pesa ambayo walikuwa wamemkamua Bwana Sucker, ambaye naye alianza kutilia shaka mpango mzima.

Maana kila dalili zilionyesha kuwa mpango mzima ungeenda harijojo kama si kuishia hata kuwa historia chafu na doa kwa serikali kuu ambayo kosa lake ilikuwa ni kutoa madaraka makubwa kwa maofisa wachache wa kuteuliwa na Rais. Hawa, walikuwa wanaonekana kama wakoloni kwenye maeneo yao ya kazi. Maana hawakuwa wamepata ridhaa ya wananchi wala kutokana nao. Wao waliwajibika kwa Rais tu bila hata kujali wananchi wanatakaje.

Baada ya Matatizo kutoa sharti lake la kuwa kisifanyike kitu chochote bila ya Mzee Njema na rafiki yake Kilimwengu kurudishwa mkutanoni, meza kuu ilibidi ikae kikao ndani ya kikao kuamua hatima ya mkutano mzima ambao nao haukuwa mkutano wa haja, bali ulikuwa kama darasa ambapo mwalimu alitoa amri kwa wanafunzi, akijua watazitekeleza na somo litakuwa limeeleweka na kwisha.

Baada ya kujadiliana na kuanza kukubali kushindwa au kutikiswa, mawazo ya Matatizo yalikubaliwa.

Mkuu wa Wilaya alikuja mbele na kuwatangazia wanakijiji kuwa serikali haikuwa ya mabavu kama walivyokuwa wakidhania.

Alisema, "Hii serikali si yetu ni yenu. Hatuwezi kutunisha misuli dhidi ya watu wetu na wenye serikali yenyewe. Hivyo, tumewaamuru polisi wawarudishe wale watu wawili waliokamatwa. Hii haina maana kuwa tumeshindwa au tumewaogopa. Hapana. Ni kutaka kuwaonyesha wananchi tunavyojali maendeleo yao na ya taifa."

Alipomaliza kusema zilisikika sauti za miguno kuonyesha kuwa wananchi hawakukubaliana na maneno yake.

Matatizo ambaye alijizolea sifa lukuki siku hiyo kwa kitendo chake cha kusimama kidete, alitabasamu tu huku akifikiria hatua ya kuhakikisha kuwa haachii fursa hii ambayo ilikuwa imejitokeza.

Hivyo, hakusema lolote pamoja na wananchi kumtolea macho, wakitegemea angesema lolote. Yeye alingoja Mkuu wa Mkoa amalize kujikaanga ili ammalize palepale.

Baada ya Mkuu wa Wilaya kutoa onyo lake alimkabidhi kipazasauti Mkuu wa Mkoa na kurejea kwenye kiti chake.

Mkuu wa Mkoa aliendelea, "Kwanza, tukubaliane kuwa sisi kama binadamu tunaweza kukosea, kukosana na kukosoana. Lazima nishukuru pia kuwa wananchi mmeonyesha mfano mzuri kuishauri serikali yenu." Alikohoa na kuendelea, "Hili ni jambo bora sana. Nasi kama serikali hatukuona sababu ya kupingana na umma."

Maneno ya Mkuu wa Mkoa yalionekana kuwashangaza wananchi waliokuwa wamelipuka kwa vigelegele huku meza kuu ikizidi kuzama kwenye lindi la aibu, hasa mbunge ambaye alikuwa akijipangapanga kwenye kiti chake kilichoonekana kuanza kuwa kama kina miba.

Ukiachia mbali aibu, nyuso za waliokaa meza kuu zilionyesha kushangaa, kadhalika huku hisia za kusambaratishwa zikianza kujitokeza.

Sucker alikuwa ndiyo kaishiwa kabisa. Maana hakuamini masikio yake.

Wakati Mkuu wa Mkoa akitoa shukurani zake, moyoni alikuwa hajakubali kushindwa, bali kuwalainisha wananchi na kutafuta njia nyingine ya kufanikisha ulaji wake. Hivyo, alikatiza hotuba yake ambayo alitegemea kuwa ingekuwa amri.

Maana hali haikujitokeza kuwa kama alivyokuwa amepanga na kutegemea. Hivyo, alijikuta akiishiwa maneno.

Mara ghafla shinikizo la moyo lilimpanda na kuanguka. Wananchi hawakuamini masikio na macho yao pale aliposema "Waheshim.." Mara alidondoka chini puuu!

Utadhani siafu wamemwona nyoka, maana meza ya mbele yote ilimeguka haraka kwenda kujua kulikoni bosi wao ameanguka. Kila mtu alijitahidi kuonyesha anamjali Mkuu wa Mkoa.

Badala ya kumwonea huruma, wananchi walishangilia kwa nguvu huku wakinyanyua mikono juu wakiwa wamekunja alama ya ngumi wengine wakinyoosha vidole viwili kuonyesha alama ya ushindi.

Matatizo alizidi kupata nguvu, alisema. "Kubalini kushindwa. Huu ndiyo mwanzo wa ukombozi na kuuzika ubabaishaji unaoanza kuwa sheria na kanuni ya maisha ya taifa". Alisimama na kurusha ngumi hewani na kusema, "Sasa ni saa ya Ukombozi. Taifa zima lisikie. Ukombozi wake unaanzia Githakwa."

Mwingine alijibu, "Toboa baba, kunguni wamezidi."

Ile nidhamu ya woga ilitoweka ghafla na wananchi wakajikuta wamepumbaa, wasiaminii yote haya yamefanywa na watu wa kijijini, tena waliokuwa wamesahaulika.

Polisi na meza kuu walimzingira Mkuu wa Mkoa, huku wakimvua koti na kumpepea.

Mwanakijiji mmoja alisikika akisema, "Damu zetu na mizimu ya mababu mnayouziana kwenye soko lenu la sera zenu za kuazima zimeamua kugoma na usaliti wenu sasa unawatokea puani."

"Aaaa" Baadhi ya watu, hasa Mama Maendeleo na mzee Kimbe, walisikika wakishangaa. Haijulikani kama walikuwa wanashangaa kitendo cha watu kushangilia balaa la mwenzao au ushujaa wao.

Mzee Kimbe alisema, "Hata kama hamkubaliani na mpango wa maendeleo na wale walioubuni, hakuna haja ya kushabikia maafa ya wenzenu."

Matatizo hakumkopesha, "Mzee Kimbe nakuheshimu. Lakini kwa hili nimekudharau. Wewe hukuona walivyoingia kwa mbwembwe wakishangilia msiba waliokuwa wametuandalia ambao tutahakikisha utawarudia wao?"

Alicheka tetete na kuendelea,"Kumbe mkuki kwa nguruwe. Sasa kwa taarifa yako tukimalizana na hawa tutawageukia nyinyi viongozi wetu, hasa mbunge, ili liwe somo kwa wengine wanaodhani kuwa wananchi ni madaraja yao ya kuvukia au farasi wa kuwafanyia kazi zao chafu."

"Toboatoboa wamezidi." Zilisikika sauti za wanakijiji ambao walikuwa wameishachoshwa na uchafuzi wa mazingira uliokuwa ukisababishwa na zebaki, ukiachia mbali kukamatwa mara kwa mara na kupigwa na walinzi wa mgodi.

Pia, wananchi waliishaanza kuuchukia mgodi kutokana na kambi ya wafanyakazi wa mgodi kuwa chimbuko na zalio la mila chafu kama vile umalaya, ulevi, ugomvi hata ujambazi.

Mkuu wa Mkoa alikimbizwa haraka kupelekwa kwenye hospitali ya mgodi ili kupewa huduma ya kwanza. Kwa kiasi kikubwa, wakubwa walikuwa wanaanza kushindwa vita vyao. Kwani kitendo cha kuanguka kwa kamanda wao, licha ya kuwa pigo, ilikuwa ni ushahidi mkubwa kuwa kumbe wengi, hata kama ni wanyonge, wakiungana wanaweza kufanya lolote. Ama kweli umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Umoja wa wananchi na mshikamano na vyombo vya habari na mashirika ya haki za binadamu katika vita hivi ndio ulikuwa silaha pekee na ya msingi wa kuufikia ushindi dhidi ya dhuluma na unyanyasaji wenye madaraka waovu.

Kitendo cha kuanguka na kuzimia kwa Mkuu wa Mkoa kilileta faraja kwa Ititu na Ithaka ambao walikuwa wakiendelea kuwasiliana.

Ititu alimpigia simu Ithaka kumfahamisha ushindi huu. Alitania, "Usishangae watu wakasema mzee kampiga juju."
Simu yake ilikuwa na fedha kidogo. Hivyo, hawakuongea sana. Isitoshe hawakuwa wakijua vita vyao vitachukua muda gani.

Sala zao kuwa ugeni uchelewe na kufumaniwa zilikuwa zimepokelewa na mizimu ya mababu wa Githakwa.

Ithaka alijistukia akiita miungu ya mababu zake. Aliwashukuru akina Modimu, Inkanyezi, Inkosi na wengine wengi kwa pamoja.

Baada ya Mkuu wa Mkoa kukimbizwa kwenye hospitali ya mgodi, karibu wakubwa wenzake wote waliandamana naye. Nyuma walibakia Kamanda wa Polisi na Ofisa Tarafa na wanakijiji.

Hivyo, kwa mara nyingine mkutano ulikuwa unazidi kusambaratika, ukichukulia kuwa aliyekuwa amezimia ndiye alikuwa msemaji mkuu na mwenye shughuli nzima kwa ujumla.

Sasa lilizuka tatizo jingine. Je, wananchi watawekwaje shuleni pale kungoja Mkuu wa Mkoa arudi au wasiende kupanga mpango wa kuhujumu jitihada hizi?

Pia, wakati Mkuu wa Mkoa akianguka alikuwa ameishatoa amri Mzee Njema na Kilimwengu watolewe korokoroni kwenye stoo ya nafaka ya shule. Je, watakaporejeshwa hawataweza kuwagomesha zaidi wananchi?
Maswali haya mawili yalitaka majibu ya haraka sana.

Wakati kamanda wa polisi akitafakari la kufanya kuhusiana na maswali haya, hao akina Mzee Njema na Kilimwengu ndiyo wanarejeshwa wakiwa watu huru.

Walikuwa wamekunja ngumi na kupunga mikono juu kama alama ya umadhubuti na ushindi.

Walikuwa wakiimba:
"Tuna imani na Githakwa."Aliimba Mzee Njema.
"Hoyaa hoyaa hoyaa." Aliitikia Kilimwengu.
"Saa ya Ukombozi." Mzee Njema aliendelea.
"Hoyaa, hoyaa, hoyaa." Aliitikia Kilimwengu.

Mfuatano wa matukio haya ulizidi kumchanganya kamanda, maana kitendo cha kuingia kwa wapambanaji hawa, kiliamsha hamasa na shangwe si ya kawaida.

Kwani mbinja,vigelegele hasa vikiongozwa na Mateso na Tunasota, vilihanikiza kiasi cha kuziba masikio.

Nao akina Mzee Njema na Kili hawakujivunga. Badala ya kuelekea walipokuwa wanakijiji wenzao, walielekea moja kwa moja meza kuu ambako kulikuwa patupu baada ya wakubwa kuondoka.

Pigo jingine. Kwani PPK waliokuwa wamewasindikiza, waliamua kuwazuia wasiende kukaa pale. Mara Kilimwengu, pandikizi la mtu ambalo lilikuwa limeishaonja majeraha na ushindi hakukubaliana na kuzuiwa kwenda kukaa meza kuu.

PPK kama ada hawakuchelea kufanya kazi yao. Mara virungu na mitama vilianza kutembezwa. Bahati mbaya zaidi walikuwapo askari watatu waliokuwa wamewaendea mahabusu na mmoja aliyebaki kulinda meza kuu. Hivyo, hali ilivyokuwa ni kwamba idadi hii ya watatu isingeweza kufua dafu kama wananchi wangeamua kujihami kama ilivyokuja kutokea.

Katika purukushani, askari alinyang'anywa kirungu na Kili ambaye hakufanya ajizi, bali alimpasua kichwa huku akiwashambulia wengine wawili walioonekana kuwa wasingemuweza hasa ikizingatiwa kuwa licha ya maguvu yake, sasa alikuwa na kirungu huku wanakijiji nao, bila kujivunga, wakaingilia kumsaidia mkombozi wao, Kili.

Ilikuwa ni patashika nguo kuchanika. Matatizo alizidi kuwatia moyo, akihanikiza.

"Jamani huu ndio wakati. Tusiuache kupita na kifo cha wengi ni harusi hakuna haja ya kujivunga."
Maneno ya Matatizo yalizidi kuchochea kujiamini kwa wananchi.

Wapo waliopiga mbinja na kelele. Wengine walizomea, mradi kila mtu na lake. Kitu kimoja kilikuwa wazi, kuwa wananchi wa Githakwa walikuwa wameamka na wasingezuilika kwa chochote na lolote wala yeyote. Maana mambo yalivyokuwa yakienda ilikuwa ni kama yalikuwa yamepangwa kwa muda mrefu, tena kwa umahiri mkubwa!
Hii ilifanya wakubwa wasiamini kama kweli kile kilichokuwa kinatokea kilikuwa halisi au ndoto. Wale waliokuwa wakidhani ni ndoto, walikosea. Hawakujua kuwa mwanzo wa ngoma ni lele.

Kama kawaida yake, mzee Njema hakupenda mapambano ya vurugu. Hivyo, alimwendea Kili huku akisukwasukwa. Alimwamuru aache vita. Maana lengo la ukombozi halikuwa vita vya kuumizana bali kukomboana. Bahati nzuri Kili alimtii na kuacha kupigana.

Ndipo Mzee Njema alianza kuwaasa hata wale askari. Alisema, "Vijana, kimsingi hili si kosa lenu. Nyinyi kama sisi ni wavujajasho wanaotumiwa na manyang'au wachache."

Alimgeukia kamanda wa polisi na kusema, "Afande, hatuna ugomvi na nyinyi kama chombo cha dola. Hivyo, hakuna haja ya kuumizana wakati nanyi mnahitaji ukombozi kama ambavyo nasi tunauhitaji." Kamanda alitikisa kichwa kukubaliana na mzee Njema.
Aliendelea mzee Njema, " Huyo aliyeumia anatosha na ni alama ya aibu kwetu. Maana nia ya ukombozi ni kuhakikisha kila mtu anakombolewa hata akina Gibbons na Sucker na wengine wa aina hii." Alimalizia kwa kupeana mkono na Kamanda wa Polisi wa Wilaya.

Kamanda wa polisi alikubali ushauri wa Mzee Njema. Aliamrisha wale askari kumwacha Kili. Pia, alimwamuru Kili kumrejeshea askari kirungu chao.

Kutokana na kipigo cha Kili na wananchi, askari aliyepondwa kichwa naye ilibidi akimbizwe kwenye hospitali ya mgodi.

Hali ilivyokuwa ni kwamba hatima ya kila jambo ilikuwa mikononi mwa Wanagithakwa wenyewe. Nao kwa kujua hilo hawakuwa tayari kupoteza fursa hii adhimu na adimu.

Alichukuliwa harakaharaka na kupelekwa hospitali ya mgodi. Alipofikishwa tu hata wenzake walishangaa na kuishiwa nguvu. Kwani, hawakujua kuwa kilichokuwa kinaendelea ilikuwa ni kweli au ndoto. Maana kwa hali ilivyokuwa, wakubwa wote waliishaonyesha dalili zote za kusalimu amri kwa watu hawa wadogo na dhalili, lakini wenye moyo mkubwa waliokuwa wameweka msingi wa mambo makubwa.

Wakubwa hawakutaka maafa yoyote. Maana hawakushindwa kuamrisha PPK, kukichakaza kijiji kizima kuanzia watu hata mifugo. Lakini, walichelea kuwa maafa yangetokea kiasi cha kuishtua serikali ambayo, nayo pamoja na udhaifu wake, isingevumilia wala kupata pa kuuficha uovu huu.

Hivyo, kuletwa kwa askari majeruhi kuliongeza uzito wa pigo kwa mpango mzima. Isitoshe wilaya haikuwa na PPK wengi. Wengi hukaa Mji Mkuu wa Fikira kuwapiga waandamanaji wanapojitokeza.

Mkuu wa Mkoa alipatiwa huduma ya kwanza na kurejerewa na fahamu. Hata hivyo, kichwa kilikuwa kikipiga utadhani kulikuwa na karakana ndani yake. Alikuwa dhaifu na asiye na raha. Lakini, yote hii haikumzuia kufikiri juu ya majaliwa yake.

Wazo moja lilikuwa limetawala kichwani mwake. Nalo ni kuondoka haraka kurejea mkoani ili kupanga mkakati mwingine au kuachana na mpango huu ambao ni dhahiri uliishaingia mdudu.

Bwana Sucker naye alikuwa hoi. Alionekana mzee kuliko umri wake huku ngozi ya mwili wake ikiwa imepauka. Nywele zilimsimama, utadhani anaugua kwashakoo.

Siku chache baadaye Mzee Njema alimlinganisha Bw. Sucker na mwalimu wake aliyemmwagia wino miaka hamsini iliyokuwa imepita.

Mkuu wa wilaya na kamanda wa polisi, kama watoto wanaongoja mama yao aamke, walikuwa wamemzunguka Mkuu wa Mkoa kusikia ataamuru lipi.

Nao mioyoni mwao walikuwa wakitamani zoezi hili lisitishwe, lakini hawakuwa na ubavu wa kumkabili bosi wao kumfundisha kazi. Isitoshe kamanda alikuwa amefanikiwa kuongea na mzee Njema ambaye aligundua kuwa mawazo yake hayakuwa mabaya kama alivyodhani mwanzoni.

Mbunge Heri Kupata hakuwa tena heri wa siku zote, bali shari kupatikana. Maana ndiye aliyekuwa amesuka mpango mzima. Hivyo, naye alikuwa kalowa chapachapa kwa mawazo.

Alikuwa amezongwa na watu huku mlinzi wake na dereva wakijitahidi kumkinga kutoka kwenye mawe na vitu vingine alivyokuwa akirushiwa na maneno mengi ya kejeli.

Mtu mmoja alihanikiwa akiimba, "Kupata umepatikana, tamaa imekurudi! Kupata umepatikana tamaa imekulipa! Kupata umepatikana usaliti umekusaliti mwenyewe!"

Watu, waliitika "Kupata kapatikana! Kupata kapatikana! Kupata kapatikana!"

Mwingine aliingilia kati na kuongeza, "Kupata ang'olewe, Kupata ang'olewe!"

Wanakijiji walijibu,
" Ang'olewe! Ang'oke na aondoke leoleo."
"Kupata achomwe moto."
"Achomwe moto." Umma uliitikia.
Matatizo alipinga wazo la kumchoma moto mbunge. Alisema, "Wananchi, pamoja na kuwa tamaa na uroho wa akina Kupata umesababisha Wanamizengwe wengi kuchomwa moto kama vibaka, hatuwezi kufanya unyama huu. Tufanye mapinduzi na kuleta ukombozi na kuachana na maisha ya kinyama ya jicho kwa jicho. Tutatoboa mangapi?"

Wananchi walimtii na kumwelewa. Hiyo, ndiyo ilikuwa salama ya Mbunge Harry Livingstone Kupata.

Kwanza, licha ya kushtuka, Kupata alikuwa haamini kuwa watu wake wangekuwa mashujaa kiasi hiki. Lakini, lawama zote alizitupa kwa Mzee Njema, ambaye kijiji kizima, kutokana na kutoelewa misimamo yake, walikuwa wakidhania ni mwehu.

Heri alikuwa amenywea ghafla, akionyesha kila alama ya woga na kushindwa. Kwa mara ya kwanza, mapinduzi yalikuwa yamefanywa na watu wadogo wa kijijini, tofauti na ilivyokuwa imezoeleka.

Hakika kitendo hiki kingelifanyika mjini kwa jinsi kilivyofanikiwa, si haba visiki vingaling'oka.

Ni leo tu, kwa mara ya kwanza, Mzee Njema amerejesha heshima yake na kutoa tafsiri ya maisha yake ya upinzani na kujiamini huku akiwaona wanakijiji wenzake kama majuha wanaoburuzwa na wajinga wachache.

Mzee Njema alikuwa halipi hata kodi wala kushiriki shughuli za kujitolea za maendeleo.

Kuepuka kuwaumbua, hata watoza kodi ambao nao walikuwa hawalipi kodi ingawa walikuwa wakiwakamata wasiolipa kodi, walikuwa wakimwacha wakijifanya wanamchukulia kama mwehu.

Ni wanawe Ithaka na Ititu na mkewe Wacera na watu wachache waliokuwa wakimwelewa. Kwa waliobaki, alikuwa mwendawazimu wa kawaida aliyechanganywa na maisha.

Mara zote alipoambiwa kuhusu shughuli za maendeleo aliwatukana wananchi kuwa hawana macho wala ubongo kwani hapakuwa na hata dalili ya maendeleo.

Hata kashfa na mgogoro wa zebaki ndiye aliyeshupalia na kuwaleta wanaharakati wa mazingira na haki za binadamu.

Pamoja na kufanya yote hayo, wanakijiji wenzake walikuwa wanamwona kama mwendawazimu. Ni leo tu wamemtambua, kumwelewa na kumkubali kama Mzee anayeona mbali kuliko wao.

Ni kama kazaliwa upya. Kwake ni siku yenye kuwekwa kwenye kumbukumbu ya aina ya peke yake. Maana ametimiza ndoto yake ya kufichua na kuushinda uovu.

25

Safari ya kutoka Fikira kwenda Githakwa haikuwa ndefu sana kwa helikopta. Kwani ilichukua saa tatu na nusu hivi.

Ithaka aliposikia tuku-tuku-tuku ya helikopta, alitamani aruke akaipokee angani! Kwani kuja kwake kulikuwa ni mwanzo wa ukombozi na tafsiri ya falsafa ya baba yake aliyemwelewa sana na kutamani kuwa kama yeye maishani. Yaani, mpigania haki asiyekata tamaa, hata kama asingeeleweka kama ilivyokuwa kwa baba yake.

Alirusha ngumi hewani kuashiria ushindi. Alijipongeza ingawa hakuwa na wa kumpongeza.

Mara alijisemea, "Wamekwisha mbwa hawa." Moyo wake ulishangilia na kurukaruka kama ndama ndani yake. Mapigo ya moyo yaliongezeka, akatamani arukeruke na kuimba, kwani ukombozi aliongojea kwa muda mrefu umefika. Alisema,"Saa ya ukombozi wa kweli na halisi imetimia hatimaye."

Helikopta ilitua salama kwenye uwanja wa mpira wa shule. Nayo ilileta changamoto ya aina yake. Kwani Githakwa madongo poromoka ilikuwa haijawahi kuona helikopta.

Wanakijiji walizidi kufurika kuiona ndege. Kwao tofauti ya ndege na helikopta haikuwapo. Kwao kila kipaacho ni ndege hata kama ni tiara. Hao ndio wananchi katika nchi huru kwenye karne ya ishirini na moja. Jina la Mzee Njema na Kilimwengu viliimbwa kama alama ya ushindi na kufungua ulimwengu mpya. Maana ya jina la Kilimwengu yalitimia. Tunasota alijawa na furaha utadhani ile helikopta ilikuwa zawadi ya mumewe.

Mateso alianza kufikiria kumshauri mtoto atakayezaliwa aitwe Helikopta au Ukombozi. Kwani kwake alikuwa akiuona ukombozi ukikaribia.

Kila mtu alikuwa na lake.

Huku hayo yakiendelea kwa wanakijiji, wakubwa walikuwa wamechanganyikiwa kabisa. Maana kama walivyokuja bila kutoa taarifa, nao hawakuwa na taarifa za ujio wa helikopta kijijini pale.

Mkuu wa polisi mara alitikisa kichwa na kusema, "Simu za mkononi!Tulisahau hili!" Alimwambia mbunge ambaye alikuwa amesinyaa kama jani lililopigwa na jua la kiangazi, akitafakari jinsi ya kuepuka kikombe hiki ambacho kilikuwa wazi kuwa lazima kinywewe.

Mkuu wa polisi na Harry walipanda magari yao na kuondoka kuelekea mgodini huku nyuma wananchi wakiwazomea baada ya Harry kunusurika kuchomwa moto kama si busara ya Mzee Njema.

Ithaka na Ititu walitoka mafichoni kuja kushuhudia matunda ya juhudi zao katika kupambana na uhalifu uliokuwa unaanza kuhalalishwa.

Walikuwa ni wenye furaha sana. Licha ya kufurahia ukombozi wao kama wanakijiji, walifurahishwa na kutimia kwa yale aliyokuwa akiwambia baba yao kuwa siku moja angeibadili hali na historia ya Githakwa na Mizengwe.

Mwanzoni waliyachukulia kama kujiliwaza. Kadiri walivyozidi kuisoma hali ya maisha na kumwelewa baba yao, walijikuta wakiwa waumini na wafuasi wake wakuu walioishia kuwa wasaidizi wake hasa kwenye saa yenyewe ya ukombozi ambayo baba yao alikuwa akiomba ifike kabla hajafariki kama ilivyotokea.

Siku zote walikuwa wakiitana mitume wa mzee Njema ambaye kwao alikuwa kama Yesu wa Wakristo. Maana alikuwa tayari kumwaga damu yake kwa ajili ya nchi yake.

Mzee Njema, Kilimwengu na Matatizo waliongozana kwenda kuwalaki wanahabari na wanaharakati wa haki za binadamu uwanjani.

Walitembea vifua mbele wakijua mwisho wa mahangaiko yao umefika na kilio chao sasa ni habari, tena kubwa kwenye vyombo vya habari nchi nzima na dunia nzima. Bahati mbaya hawakuwa na televisheni. Wangejiona kwenye televisheni kwa mara ya kwanza katika maisha yao.

Walijisikia raha, kwani walikuwa wamefanikiwa kufikisha ujumbe kwa serikali waliyoichukia na kuidharau kutokana na kuwaachia watu wachache kuchezea madaraka.

Wanagithakwa walianza kuheshimiwa na vijiji vya jirani hata vile vilivyokuwa vikiwadharau na kuwaita madongo anguka.

Mara baada ya kushuka kutoka kwenye helikopta wapiga picha walianza kuwapiga picha wananchi. Vimulimuli vya kamera zao vilihanikiza kila sehemu.

Wanakijiji walijipanga kupiga picha utadhani walikuwa studio.

Waandishi walianza kazi mara moja. Walianza kudodosa kila aliyeonekana kuwafaa. Walianza kukusanya habari. Kila kitu kilifanyika kama vile mchezo wa kuigiza ulioigizwa kwa ustadi wa hali ya juu.

Mzee Kimbe hakungoja yamkute. Alitimka kama mbwakoko aliyeona fisi. Akifuatana na Ofisa Mtendaji wa Kijiji na yule wa Tarafa. Wananchi walimsindikiza kwa kelele za kumzomea, wengine wakipendekeza wamfukuze na kumkamata na kumtia moto.

Kama si Mzee Njema kuingilia kati kuwazuia, wangekuwa marehemu. Maana Mzee Njema aliwaonya wanakijiji kuwa wasidai haki kwa kuvunja sheria. Wawe watulivu na kuona mwisho wa yote. Alisisitiza wasivunje sheria ili wakubwa wasipate visingizio vya kuzima wimbi lao la ukombozi.

Alisisitiza kusema kuwa kuwachoma watu moto ni unyama. Alishangaa ni kwa vipi watu wanaweza kupata ujasiri wa kuwachoma moto vibaka wadogo wakati wakiwaabudia majambazi wakubwa waliowafikisha hapo.

Alisema, "Hao mnaowachoma moto kwa kudokoa, kimsingi wametengenezwa na hawa tunaowaheshimu na kuwanyenyekea. Tukomeshe jinai hii mara moja kwa kuonyesha mfano."

Aligeukia upande wa Ndirangu aliyekuwa kahanikiza akimmwagia sifa na kucheka na kuendelea, "Lazima Githakwa tutoe somo. Somo lenyewe ni kuongoza kwa kuwa mstari wa mbele kwa maneno na matendo. Tumeelewana?"
Wananchi walitii na kuitikia, "Tumekuelewa shujaa wetu."

Kufikisha ujumbe wake barabara aliwasimulia visa vya watu wawili mashuhuri, yaani, Nelson Mandela ambaye jina lake alikuwa amempa Kilimwengu kama ishara ya kuheshimu ushujaa na mchango wake.
Alitalii historia ya Mandela. Alimalizia na historia ya Gandhi mtu mdogo lakini mweye busara aliyewashinda Waingereza kwa utulivu wake lakini ukali wa kung'ang'ania kudai haki.

Wanakijiji waliwapenda mashujaa hawa. Hata hivyo, walisikitika walipoambiwa kuwa Gandhi alikuwa ameuawa kwa kupigwa risasi mwaka 1948.

Walisikitika sana. Lakini, walifurahishwa sana na kujua kuwa Mandela alikuwa bado hai.

Mama Maendeleo alikuwa ameishapotea kimyakimya baada ya kuona kuwa wanakijiji walikuwa wameamka dhidi ya ukandamizaji na unyonyaji na uongo wao.

Kwa mara ya kwanza tangu astaafu,Mzee Njema aliingia ulimwengu mpya aliouwaza na kuupigania kwa muda mrefu. Ndoto yake imetimia.

Alikumbatiana na kiongozi wa wanaharakati wa haki za binadamu aliyejulikana kama Mshindi Mapigo na baadaye mkuu wa waandishi wa habari, Jasiri Ndamu. Alikuwa mshindi na mwenye mapigo kweli. Maana, ukiangalia hicho kidevu chake na kipara, unakubali kuwa huyu amemaliza vitabu.

Ndirangu naye heshima yake ilipanda. Alisema, "Hawa ndio wasomi ambao huwa nawaambia. Wasomi ndio hawa wanaotumia usomi wao kuwakomboa wenzao. Nami ni msomi." Wananchi waliangusha vicheko aliposema kuwa naye ni msomi.

Wananchi walishangaa kuona mzee Njema alivyokuwa mashuhuri, lakini asiyejionyesha. Kiingereza yes, yes kilianza kutawala. Ajabu na mzee Njema hakuwa nyuma kwenye kutema cheche zake kwa ung'eng'e!

Mzee Njema aliongea na yule jamaa mwenye madevu kwa Kiingereza halafu akamshauri waongee Kigithakwa ili wananchi nao wapate kujua kilichokuwa kinaendelea. Maana tukio zima ni juu yao na maslahi yao.

Yeye hakujichukulia kama shujaa, bali wanakijiji waliokubali kusimamia mapambano tena ya siku moja kuuangusha ukandamizaji uliokuwa umeishi nao kwa miaka mingi.

Pendekezo hili liliwafurahisha wananchi sana na kumwona mzee Njema kuwa ni mkombozi wao kwelikweli. Kwani, kwa kupendekeza kitumike Kigithakwa alikuwa anawashirikisha wananchi. Hivyo alijijengea heshima na uzalendo wa hali ya juu kwa wananchi.

Baada ya kutoa pendekezo mwananchi mmoja alijisemea, "Kuanzia leo Heri Kupata kapata saizi yake. Lazima Mzee Njema tukupeleke bungeni." Alimalizia.

Mzee Njema alicheka na kuwatia hamasa wanakijiji. Alisema, "Hakuna haja ya kuogopa. Wanaweza kunifunga hata kuninyonga. Lakini, hawatafunga mawazo yangu wala ukombozi."

Alipandisha mori na kusema, "Saa ya ukombozi ni sasa na moto huu usizimike. Tunataka hata huko aliko Rais ajue kuwa Githakwa imeamua kuongoza njia kuelekea ukombozi wa nchi hii iliyogeuka chaka la majambazi na wezi. Hizi ni salamu zake."
Ndirangu alijibu, "Baba, toboa, tupo nyuma yako."

Mzee Njema aliendelea, "Tumenyanyaswa, tumenyonywa, tumepuuzwa na kudhulumiwa vya kutosha. Sasa ni saa ya kujikomboa kama watu na taifa. Hivyo, moto huu ndugu zangu usizimike. Mambo ndiyo yanaanza. Hatuhami, hatuhami tukihama tuwe maiti."

"Duh! Mzee Njema kumbe si bure kama mbunge wetu!" Alidokeza mwanakijiji mmoja.

Wakati yote haya yakiendelea waandishi wa habari na vyombo vyao walikuwa kazini.

Ushirikiano na mwitikio wa wananchi ulimtia moyo na kumpa faraja na hamasa ya kuendelea kupambana.

Swali lililowachanganya na kuwafungua macho ni pale waandishi na wanaharakati wa haki za binadamu walipouliza alipokuwa Mkuu wa Mkoa na ujumbe wake.

Kweli Waarabu wa Pemba hujuana kwa vilemba. Kumbe, wakati wananchi wakipambana kwa hisia za kuepuka mateso ya kuhama, miongoni mwao walikuwapo waliokuwa wanajua kila hatua ya mchezo mzima!

Mara mwanakijiji mwingine alijisemea, "Mzee Njema, kiboko, umesikia vipande vyake? Kumbe si mwehu wala mwenzetu kama tulivyokuwa tukidhania. Huyu ni kiumbe wa dunia nyingine!"

Harakaharaka Kilimwengu na Ithaka walifuatana kuwapeleka waandishi wa habari na wapiga picha kwenye hospitali ya mgodi.

Hospitali iko kama kilometa moja kutoka shuleni. Waandishi hawakuwa na gari. Lakini, kutokana na uzito wa tukio lenyewe waliamua baadhi wachape mguu na wengine waliendelea na kuwahoji wananchi.

Wakati kundi la akina Kilimwengu lilipokuwa limetembea kama meta ishirini hivi, mara gari la polisi lilitokeza likiwa limefuatana na gari la mbunge.

Magari mawili yalisimamishwa na kamanda wa polisi na mbunge walishuka kwenye magari yao.

"Enhe! Nyinyi ni nani na mnataka nini hapa?" Kamanda aliuliza kwa sauti ya ukali kidogo.

Badala ya waandishi wa habari na wanaharakati kujibu kwa mdomo walichomoa vitambulisho vyao huku mpiga picha akiwa anapiga picha.

"Wewe, nani kakuruhusu kutupiga picha?" Badala ya kuangalia vitambulisho vyao alimuuliza mpiga picha ambaye alikuwa kahamanika kupiga picha. Mianga ya kamera ilikuwa ikimemeta.

Alikuwa ameishapiga kama picha kumi hivi. Mpiga picha wala hakushughulika na kujibu wala kueleza.

Kamanda wa polisi alitoa tishio jingine, "Acha kupiga picha kwanza, vinginevyo nitaamrisha unyang'amywe hiyo kamera. Kwanza, nani kawaruhusu kuingia kwenye wilaya yangu bila kibali wala taarifa?"

Mwandishi mmoja aliyekuwa ameshikilia chombo cha kurekodia mazungumzo naye kama mpiga picha badala ya kujibu swali aliuliza swali, "Kamanda leo kuna nini mbona viongozi wote wa mkoa mko huku?"

Kabla ya swali lake kujibiwa mwandishi mwingine aliuliza swali jingine,"Je, ni kweli kuwa viongozi wa mkoa wa Chelewa mmekula njama na Glutton Sucker kuwafukuza wanakijiji ili Sucker apanue mradi wake?"

Swali hili lilimmaliza nguvu kamanda wa polisi ambaye kijasho chembamba kilikuwa kikichuruzika.

Baada ya mzee Njema kuona magari ya mbunge na kamanda wa polisi yamerudi, alihofia wangeanzisha fujo.

Hivyo, alimshauri Jasiri na wenzake waandamane kwenda kujua kulikoni

pale walipokuwa wakihojiana na waandishi wa habari na wanaharakati wa haki za binadamu na mazingira, waliokuwa wameamua kumfuata Mkuu wa Mkoa mgodini.

Harry na kamanda wa polisi waliokuwa wameishachanganywa na waandishi wa habari, walivyoona mzee Njema anaelekea upande wao, waliamua kuondoka. Badala ya kuendelea kukabiliana na sulubu za waandishi wa habari alipanda kwenye gari na kuamrisha dereva aondoe gari kuelekea hospitali.

Mbunge naye akiwa amechanganyikiwa alijikuta kavamiwa na waandishi wa habari na maswali yao!

Alisema, "Pamoja na kutuvamia mjue upinzani hauendeshwi hivi. Kwa nini waandishi wote ni wa magazeti ya upinzani?" Aliuliza kwa hasira.

Mwandishi mmoja alimjibu, "Hilo swali la wale ambao hawapo, ungengoja ukionana nao uwaulize."

Kabla ya kutafakari jibu hili mwandishi mwanamke aliuliza, "Eti mbunge, ni kweli njama ya kuwahujumu wananchi ilitokana na Sucker kuwapa kiasi kikubwa cha pesa? Je, ni kweli kuwa hata Rais wala Waziri Mkuu hawajui mpango huu?"

Mbunge alijibu kwa hasira, "Wewe ndiye wasema."

Mbunge naye kuogopa kujiingiza kwenye mtego, alidandia shangingi lake na kumwamuru dereva wake kukanyaga mafuta kurudi hospitali.

Baada ya waandishi kuona wamekimbiwa, walikubaliana kutowafuata bali kuwangoja. Maana hapakuwa na barabara nyingine ambayo wangetumia kuwakimbia.

Hivyo, walirejea kujiunga na wenzao waliokuwa wanaendelea kuwahoji wanakijiji wakiwa na nyuso za furaha kwani walikuwa wamepata picha za mwanzomwanzo.

26

Mbunge na kamanda wa polisi wa wilaya walipofikisha habari za kuja kwa waandishi wa habari na wanaharakati wa haki za binadamu kwa Mkuu wa Mkoa aliyekuwa ameishazinduka kwenye kuzimia, alizidi kuchanganyikiwa.

Aliiona hatari ya cheo chake inakaribia. Pamoja na kwamba alikuwa rafiki wa Rais, hili lilikuwa kubwa kiasi cha kumshtua na kumchanganya.

Mkuu wa Mkoa alijitahidi kuficha mshtuko wake huku akijiuguza.

Wakati Mkuu wa Mkoa akiendelea na masahibu yake,simu ya Sucker ilikuwa kazini akiwasiliana na balozi wa nchi yake ili kumtaka aingilie kati kuibana serikali iridhie mradi wake hata kwa kutishia kusitisha misaada kwa serikali ya Mizengwe iliyokuwa ikipata kutoka kwa nchi yake.

Kimsingi haikuwa misaada kitu bali kuibebesha mzigo nchi ili iendelee kutawaliwa na kunyonywa. Maana kilichoitwa misaada ilikuwa ni mikopo yenye masharti magumu na riba kubwa.
Haikuwafaa wananchi bali watawala wachache waliokuwa wakikatiwa chao na kuitumbukiza Mizengwe kwenye shimo la ufukara.

Sucker alijua nguvu ya balozi wake ambaye alikuwa na uwezo hata wa kuonana na Rais wakati wowote bila kipingamizi.

Pia, balozi alijua udhaifu wa Waziri wa Fedha ambaye alikuwa shemeji yake mbunge. Yeye alikuwa akijali asilimia kumi yake na kutelekeza maslahi ya taifa. Kwake taifa lilikuwa ni tumbo lake.

Balozi naye hakuchelewa. Alianza kuwasiliana na mabalozi wenzake wa nchi zenye ushawishi ili kuhakikisha maslahi yao yanashinda dhidi ya maslahi ya wananchi.

Mmojawapo aliyewasiliana naye alikuwa ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Anga ili kujua huyu mwenye helikopta ni nani na kwa nini alikodisha helikopta yake kwa watu waliokuwa na nia mbaya na mshikamano wa kitaifa.

Mkurugenzi naye hakuchelewa, aliwasiliana na kampuni iliyokodisha helikopta ile kwa watu ambao kimsingi walikuwa ni wapinzani wa serikali.

Alijitetea kuwa kampuni yake haikujua kabisa kuwa waliokodisha helikopta yao hawakuwa madaktari kama walivyojitambulisha, bali waandishi wa habari na watetezi wa mazingira na haki za binadamu.

Katika nchi ya Mizengwe karibu kila biashara au kitu chochote kinachohusiana na maisha ya wananchi, kina mkono wa serikali ambao siku zote unahakikisha hakuna shughuli inayovuruga maslahi yake hata yakiwa na madhara kwa wananchi.

Lilikuwa ni jambo la kawaida katika nchi hii, wakubwa,watoto wao au wake zao kuvunja sheria bila kushughulikiwa.

Kipindi hiki, hata sheria ilikuwa imepoteza maana. Kwani ilionekana kuwapo kuwadhibiti wadogo dhidi ya wakubwa na kuwahudumia wakubwa ikiwadhulumu wadogo.

Badala ya sheria kuwa nyenzo ya haki, iligeuzwa nyenzo ya dhuluma iliyofanya haki kununuliwa sokoni kama dagaa kwa walanguzi wenye pesa tena walioipata kwa kuibia umma huohuo uliokuwa unalanguliwa haki!

Ilikuwa jambo la kawaida kwa mtu wa kawaida kuombwa, hata kulazimishwa, atoe chai, mchango wa harusi, kutolewa upepo, kuzunguka mbuyu na majina mengine ya ajabuajabu, yote yakimaanisha rushwa iliyokuwa imehalalishwa na haki kuharamishwa.

Kulikuwa kumetokea jinai ya watoto wa wakubwa au matajiri kuua watu maskini na kuachiwa, utadhani walikuwa wameua mbwa au nyoka. Wengi

waliwaua watu hawa kwa kuwagonga na magari yaliyonunuliwa kwa kodi zao wakati wakienda au kurudi kutoka kwenye starehe zao. Katika jinai hii ya kulangua haki, wenye nafasi walishinda na kuondoka wakiwa watu huru!

Kwa upande mwingine kulikuwa na wawekezaji wageni. Hawa walikuwa wakinyonya haki za wananchi na kuwadhalilisha bila kuguswa. Waliwafanyia unyama wote wakijigamba kuwa serikali ilikuwa mifukoni mwao na hakuna ambaye angewagusa. Lakini, kwa mara ya kwanza wananchi wa kijiji kidogo cha Githakwa, chini ya Mzee mwenye mwili mdogo, Njema, walikuwa tayari kung'oa tabia hii.

Yalikuwa yanafanyika mambo mengi ya ajabu. Kuna kisa kimoja ambapo mpishi kutoka uhindini alikutwa akiwa anafanya kazi nchini Mizengwe kama mtaalamu wa viwanda vya nguo! Pia, iligundulika kuwa kumbe wageni wengi walikuwa ni wakimbizi wa kiuchumi na wauza dawa za kulevya waliokuwa wamepewa vibali na serikali baada ya kuhongwa ikiwa inajua walikuwa watu hatari!

Miaka kama saba iliyopita kuna gavana mmoja alimpiga mtu mateke na kufariki. Lakini, cha ajabu gavana yule hakufanywa kitu zaidi ya kuteuliwa kuwa balozi nchi za mbali alikokuwa akiendelea kutanua.

Hivyo, mabalozi wa nchi za kigeni walikuwa wanaujua udhaifu huu na walijua kuutumia. Kwani haohao waliokuwa wakisaidia kuvunjika haki za binadamu pia walikuwa ni haohao waliokuwa wakifadhili makundi ya haki za binadamu ili kuficha uovu wao.

Mkuu wa Mkoa kwa upande mwingine alijikaza kisabuni na kuamuru waondoke Githakwa. Aliamuru magari yasisimame shuleni. Alilenga kuwakwepa waandishi wa habari.

Hivyo, msafara wa magari ulianza safari ya kuikimbia Githakwa baada ya wanakijiji kushinda mpambano huu.

Walipofika shuleni Githakwa, kamera zilikuwa zikitema vimulimuli kwa hasira kama mvua yenye radi, kupiga picha magari ya waheshimiwa wale

waliokuwa wamejiingiza kwenye shughuli isiyo na heshima.

Ukichangia na mbwembwe za wapigapicha, wanakijiji ambao wengi wao walikuwa hawajawahi kupigwa picha, walifaidi si kawaida. Ilikuwa ni kama mashindano ya kupiga picha.

Yule mpigapicha mwanamke aliyekuwa amevalia suruali aliwaacha hoi wanakijiji. Maana kama yangekuwa mashindano ya nani kapiga picha nyingi angechukua taji mama yule.

Kwa mara ya kwanza walishuhudia waheshimiwa waliozoea kuamini walikuwa hawatishiki, wakiwa wamelowa kama wezi waliokutwa wakiiba!

Kwa mara ya kwanza kwa wananchi wa Githakwa walishuhudia waheshimiwa wakitishwa na kutimuliwa na watu waliokuwa wakiwatisha na kuwadharau siku zote.

Mlevi Ndirangu alijisemea, "Leo wajanja wamekutana, yetu macho. Kunguru wakipigana si haba panzi hupata upenyo na hii si bure. Hatima yetu sasa itajulikana". Alicheka na kuendelea, "Nami msinisahau, nipige japo moja hata kama ni mlevi."

Mpigapicha aliyekuwa karibu alimpigapicha na kuanza kumhoji.

Mpiga picha, "Mzee, jina lako nani?" Ndirangu hakusita alijibu, "Mimi si mzee ni dhiki ndugu yangu. Naitwa Ndirangu, maarufu kwa jina la mlevi msemambovu."

"Kwanini unapenda kujiita mlevi?" Aliuliza Mpiga picha.

Ndirangu alijibu, "Bila kuwa mlevi Mizengwe hii utaishi ndugu yangu? Matatizo ya hawa waheshimiwa ndiyo yalinifanya niwe mlevi. Kazi hakuna. Haki hakuna. Maana ya maisha hakuna, sasa unategemea nifanyeje?" Ndirangu alimalizia kwa kuuliza swali.

Kutokana na kwamba magari hayakuonyesha nia ya kusimama, yule mwandishi aliachana na Ndirangu na kuanza kuyafukuzia magari kwa kamera yake.

Hawakusimama. Walipita kwa kasi, kama gari la wagonjwa, wasijue wasingefika mbali. Maana daraja la Mto Chania lilikuwa limeishavunjwa na mbao zake kufichwa. Hivyo, mbio zao za kutaka kutoroka zilikuwa za sakafuni, wasijue zingeishia uvunguni.

Wananchi nao hawakuficha hasira zao. Waliwazomea kama wezi! Hakika siku hiyo Githakwa iliamka na kujisimamia dhidi ya uovu wa mchana.

Ndirangu alianza kujitapa, "Nyie huwa mnaniona kama sikusoma na sijulikani! Mmeona vitu vyangu? Najua baadaye wataniita. Nitatoboa uchafu wote tuliokuwa tukifanyiwa na hawa watawala wachafu hapa kijijini."

Alijitapa na kuendelea kushangaa, kama wananchi wengine, jinsi waandishi wa habari na waheshimiwa walivyokuwa wakitoana jasho, mmoja akimuwinda mwenzake.

Kwa upande wao, Mzee Njema na wanamapinduzi wenzake, waandishi wa habari na watetezi wa mazingira na haki za binadamu hawakuwa na wasiwasi. Maana walikuwa wakijua kuwa hapakuwa na daraja.

Hivyo, baadhi ya wapigapicha na waandishi wa habari walishatangulia na kutia kambi mtoni Chania kungojea mawindo yao.

Kitendo cha kupita shuleni na kuelekea Mto Chania kiliwapa faraja wakubwa wakijua angalau wasingehojiwa.

Wakati magari yakitimka kuondoka Githakwa, mawazo ya Mkuu wa Mkoa yalikuwa mbioni kadhalika.

Alifikiria jinsi ya kuupamba mpango wake na kuihusisha serikali akiishawishi kuwa haukuwa na rushwa wala harufu ya rushwa.

Alipanga akipata faragha awasiliane vizuri na Waziri waliyekuwa wamesuka naye mpango ule ambaye alikwishamtumia ujumbe mfupi kwa simu ya mkononi kutangaza mradi ule kwenye Gazeti la Serikali ili kuuhalalisha na kuzima shutuma za waandishi wa habari na wanaharakati wa mazingira na haki za binadamu watakapoanza kulipua bomu lao kwenye magazeti.

Alijipa moyo kuwa wangefanikiwa. Kwanza, Rais aliyependa sana kufanya ziara nje, hakuwapo Mizengwe. Alikuwa ziarani yeye, mke na watoto wake kwenye nchi ya Lusembagi ambako inasemekana alikuwa ameficha mamilioni ya fedha.

Hata hivyo, kutokana na kukua kwa teknolojia ya mawasiliano, Rais alipata taarifa.

Wakati akihutubia raia wa Mizengwe waliokuwa wakiishi nchini Lusembagi aliligusia suala la Githakwa.

Aliwahakikishia wananchi hao kuwa hapakuwa na rushwa wala hujuma bali chokochoko za wapinzani kutaka serikali yake ionekane mbaya.

Hivyo, aliwatoa wananchi hao wasiwasi na kuwashauri wachume pesa ughaibuni na kuja kuwekeza Mizengwe. Ingawa wananchi hawakumpinga, walijua wazi ukweli na uongo ulikuwa upi. Maana walikuwa wakijua hali halisi nchini mwao hasa kutokana na ndugu zao kuwa wanawalalamikia, wakiomba angalau wawatumie pesa kidogo kwa ajili ya shida mbalimbali.

Magari ya wakubwa yalipofika kwenye daraja la Mto Chania ambalo lilikwishageuka historia, walishangaa kuona kamera zikiwamulika na kundi la waandishi wa habari na wanaharakati likiwavamia.

Mshangao uliowaacha hoi ni pale walipogundua kuwa kumbe daraja lilikuwa limekwenda.

Mkuu wa Mkoa alisikika akisema "wanaharamu hawa kumbe mahiri!"

Wakubwa hawakukubali kusalimu amri kirahisi, waliamua kuvuka hivyohivyo wasijue kulikuwa na misumari kwenye sakafu ya mto.

Waliamini wangalivuka kwa vile magari yao yalikuwa 4WD na land rover. Lakini, Mto Chania nao ulikuwa umeishaanza kuonja joto la uchafuzi wa mazingira. Kwani, ulijaa tope zito kama uji ambao ulikuwa ukifunikwa na maji kidogo. Hivyo, gari la kwanza lilipojaribu kuvuka lilijikuta magurudumu yake yote yakifunikwa na tope zito tena lenye harufu mbaya kutokana na wingi wa zebaki na mabaki ya viumbe wa majini waliokuwa wameuawa na zebaki na uchafuzi kwa ujumla.

Hivyo na mto wenyewe ulikuwa unawachukia waheshimiwa. Maana ni matumbo yao yaliyousababishia ukame na uchafuzi huu. Hivyo nao ulipata nafasi ya kujikomboa.

Mkuu wa Mkoa alipoona kuwa wasingeweza kuvuka, alimwamuru dereva wake kutozima gari ili aendelee kukaa mle wakati viyoyozi vikifanya kazi.

Aliamini wapigapicha wasingeipata sura yake maana gari lake lilikuwa na vioo ambavyo huwezi kuona ndani ukiwa nje.

Waandishi walikuja dirishani wasione ndani. Hili kidogo liliwachanganya kuwa wangekosa picha ya mtu waliyekuwa wanamtaka kwa udi na uvumba.

Walianza kupiga namba na maandishi ya gari la Mkuu wa Mkoa. Namba ya SG yaani Serikali ya Mizengwe, ilipigwa picha kama sabini hivi. Bendera ya Mizengwe ambayo ilikuwa imetundikwa mbele ya gari la Mkuu wa Mkoa nayo iligeuka kivutio kwa wapigapicha.

Awali walikuwa wamefanikiwa kupata picha ya kamanda wa polisi na mbunge tu.

Wakati wakizidi kufikiria la kufanya,Ithaka aliwatoa wasiwasi. Kwani alijua kutokana na shangingi kuunguza mafuta mengi kwa muda mfupi,

magari ya wakubwa yangeishiwa mafuta na joto lingewaamuru wafungue vioo vya madirisha kwa hiari yao wenyewe.

Hivyo, hawakujihangaisha zaidi ya kungoja muda wao wa kupata mawindo yao utakapofika.

Kama mtu aliyeharibikiwa na gari kwenye mbuga ya wanayama, katikati ya kundi la simba wenye njaa ya siku nyingi, wakubwa na waandishi na wanaharakati waliwindana kila mmoja akingoja zamu yake.

Haukupita muda magari moja baada ya jingine yalianza kuishiwa mafuta. Lilianza gari la mbunge. Mara ilisikika nguuuu kabwaya! Baada ya kama dakika tano, mbunge alifungua kioo cha gari lake kidogo kama milimeta chache kupitisha hewa huku akiwa amejaa shanga za jasho.

Mara lilifuatia la Mkuu wa Mkoa. Shangingi lake nalo lilitoa kilio kuashiria pumzi yake ya mwisho. Nguuu-nguu-mara-kabwaya-nga-nga, hilo lilizimika. Naye kama mbunge, alifungua vioo kidogo kuruhusu hewa safi kupita.

Joto lilizidi kwenye magari yote huku jasho likiendelea kuwachuruzika waliokuwamo ndani.

Baada kama ya dakika ishirini joto lilikuwa halivumiliki. Mara ghafla vioo vya gari la Mkuu wa Mkoa vilifunguka! Hii ndiyo nafasi iliyokuwa imengojewa kwa muda mrefu. Huu ndio wasaa uliokuwa umeunguza mamilioni ya pesa kukodi helikopta.

Mara Mkuu wa Mkoa anajikuta katikati ya kamera na waandishi na wanaharakati huku kamera zikizidi kutema miali.

Hamadi! Kumbe Mkuu wa Mkoa na mkuu wa msafara Jasiri ni watu wanaojuana!

Hili lilimpa matumaini Mkuu wa Mkoa aliyesema, "Kumbe ni wewe ndugu yangu!" Alishusha pumzi na kusema, "Zimwi likujualo" Akiwa na

maana kuwa angeweza kumshawishi Jasiri achukue kitu kidogo halafu mpango mzima uishe.

Jasiri hakustuka wala kuonyesha kuwa walikuwa wakijuana. Ni kwamba Jasiri na Gibbons walisoma sekondari moja, tena wakiishi chumba kimoja na wakiwa marafiki waliotenganishwa na taaluma zao.

Walikuwa na mawasiliano kwa muda mrefu wakati Dikupatile akiwa mwanajeshi wa kawaida. Lakini, baada ya kupanda cheo jeshini na kuteuliwa kwenye ulaji wa kisiasa, ghafla alikatisha mawasiliano.

Kila Jasiri alipokumbushia urafiki wake hakupata jibu. Hivyo, huo ulikuwa ndio mwisho wa kuonana hadi walipokutanishwa na kashfa ya upanuzi wa mgodi wa uchimbaji vito. Kweli hujafa, hujaumbika.

Waandishi wa habari, kama kawaida yao, walianza kumtupia maswali ya maudhi Mkuu wa Mkoa ambaye hakujibu hata moja ukiachia mbali kumwashiria Jasiri aingie kwenye gari.

Ili kumpata vizuri Mkuu wa Mkoa, Jasiri aliingia garini ambako Mkuu wa Mkoa alimnong'oneza waongee na kuyamaliza.

Alimwambia kwa sauti ya chini, "Ndugu yangu na rafiki yangu, kwa nini tunaumbuana. Naomba tuyamalize, nitatoa pesa yoyote utakayotaka."

Jasiri, kwa kuujua mchezo mzima, hakukataa. Maana alijua kinasasauti chake kwenye mfuko wa koti kilikuwa kazini.

Ili apate mawindo yake aliongea kwa sauti ya juu, "Unatakaje?"

Mkuu wa Mkoa alijibu, "Ongea taratibu nataka isirekodiwe."

Alichokuwa akikitaka Jasiri kimejileta, tena kiulaini. Naye alimuuliza, "Una maanisha nini?"

Mkuu wa Mkoa alijibu, tena kwa kumnong'oneza huku kamera zikifanya kazi yake, "tutafute faragha tuyamalize ndugu yangu." Alimalizia Mkuu

wa Mkoa akiwa anaonekana kuogopa na kuchanganyikiwa.

"Oke." Jasiri alimjibu.

Jasiri harakaharaka alishuka garini na kuwamuru wapiga picha huku akiwafinyia jicho waache kupiga picha na wala wasikaribie gari.

Hii ilimpa moyo Mkuu wa Mkoa na wakubwa wenzake. Kwani walijua kwa jinsi watu wa Mizengwe walivyo hodari wa kuchuuzana, angefanikiwa kumkatia chake na kufunika kombe, asijue ndiyo alikuwa akijishindilia kwenye shimo, tena kiulaini!

Wenzie Jasiri walimwelewa kwa kile wazungu waitacho lugha ya kiungwana. Hivyo, walitii amri yake.

Alirejea garini akiwa hana wasiwasi. "Mkuu wa Mkoa hakungoja, alisema, "Ama kweli nilijua nimekwisha tena kwa aibu." Alitabasamu na kuendelea, "Ndugu yangu, siwezi kukuficha unajua kila kitu. Yaliyosemwa hayana ukweli. Ninachotaka kufanya ni kuepusha wapinzani wetu kupata sababu. Hivyo, naomba unielewe kuwa sijitetei wala kuficha baya lolote ila vyombo vyenu huwa si vizuri, hata huripoti uongo."

"Una maana gani" Aliuliza tena Jasiri.

Mkuu wa Mkoa alimjibu, "Maana yangu ni kwamba mlipewa taarifa za uongo na wabaya wetu kiasi cha kuwakodishia helikopta ili mje kutuumbua kutokana na hisia zisizo na msingi. Hivyo, nilitaka niwalipe gharama za kukodi mashine yenu na usumbufu halafu tukae tuweke kumbukumbu sawa."

"Sijakuelewa. Unataka kuniambia kuwa huna mpango wa kumpa mwekezaji ardhi ya wanakijiji si kwa faida ya taifa bali waroho wenzako wachache?" Jasiri aliuliza kwa ukali na ujasiri akiwa amemtolea macho Mkuu wa Mkoa.

"Hayo maneno. Kusema ukweli ule wa Mungu, ni kwamba huu mradi hauna hata harufu ya rushwa acha rushwa yenyewe." Alijibu Mkuu wa Mkoa akitaka kujaribu kumzidi maarifa Jasiri, asijue hicho si kitu kipya kwake.

Ilikuwa ni vita kati ya mwanasiasa na mwandishi wa habari. Wajuaji walikuwa wamekutana tena patamu. Jasiri alikuwa kwenye upande mzuri. Kwani uheshimiwa wa Mkuu wa Mkoa ulikuwa umemkimbia, akibembeleza na kujishusha ili angalau aweze kuiepuka aibu na adhabu.

"Sawa. Kama ni hivyo, huna haja ya kuogopa chochote." Alijibu Jasiri akionyesha kuudhika kidogo.

Baada ya kugundua kuwa hakuwa na haja ya kuzungusha mambo, aliendelea, "Mkuu wa Mkoa." Kabla ya kuendelea Mkuu wa Mkoa alimkatiza, "Niite Gibbons, wewe ni rafiki yangu." Alishauri asijue kuwa Jasiri alikuwa anataka baadaye Gibbons asije kumruka. Pia, alitaka wasikilizaji baadaye wasipate shida ya kutafsiri mahojiano yao. Mtambo wake ulikuwa ukirekodi kila kitu.

"Wewe ni Mkuu wa Mkoa, si Gibbons. Gibbons ni nyumbani kwako na mkeo. Hebu kwanza tuache mambo ya majina. Alizidi kumkazia macho na kuendelea, "Sasa, kama unaniona miye ni mwanafunzi wa taaluma yangu ukanificha ukweli, basi nitakukaanga badala ya kukusaidia. Maana kama umeniamini kama rafiki yako uniambie ukweli nijue jinsi ya kukusaidia kwa vijana wangu." Jasiri Alimalizia.

27

Maongezi ya Mkuu wa Mkoa na Jasiri baadaye yalihama kutoka kwenye kupimana akili hadi kwenye ukweli.

Kilichotokea ni mwandishi wa habari kumzidi maarifa mwanasiasa. Kilichosaidia ni ile hali ya Mkuu wa Mkoa kutojua kuwa kulikuwa na kinasasauti kikirekodi kila kitu. Kutokana na masahibu ambayo Mkuu wa Mkoa alikuwa ameyapitia, hakuweza kukumbuka kuwa katika hali ile na kwenye suala kama lile, kumwamini mwandishi wa habari ilikuwa ni sawa na kujitia kitanzi.

Kwani baada ya kubanwa sana alikiri kuwapo kwa mpango wa kuwahamisha wananchi kupisha upanuzi wa mgodi. Lakini, aliendelea kushikilia msimamo kuwa mradi ule ulikuwa umeridhiwa na serikali naye alikuwa pale kihalali kuiwakilisha serikali likiwa ni mojawapo ya majukumu yake halali kama Mkuu wa Mkoa.

Alipoulizwa ni kwa nini alikuwa tayari kurudisha gharama za kukodisha helikopta, alijitetea kuwa hakutaka wapinzani wao watumie nafasi hii vibaya kabla mradi haujafanikiwa. Kwani hali hii ingeuchelewesha mradi kutokana na wadau mbalimbali kujiingiza kwa maslahi tofauti.

Sababu nyingine aliyoitoa ilikuwa ni kutaka kutokwamisha mradi kwa vile serikali ilikuwa imeishapangia matumizi ya pesa ambayo ingepatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hivyo, kuuchelewesha mradi kwenye malumbano ya kisiasa kungewanyima wananchi haki yao ya kupata huduma walizokuwa wakizihitaji.

Baada ya vita vya kukwepana baina ya Mkuu wa Mkoa na Jasiri kufikia mwisho kwa Mkuu wa Mkoa kukiri na kuomba Jasiri akubali kuchukua rushwa, Mkuu wa Mkoa alizimia tena baada ya kusikia chombo cha kurekodia kikilia "kati!"

Uzuri ni kwamba alikuwa ameishatoboa siri nyingi juu ya mradi hewa uliolenga kuwauza wananchi kwa kuwaneemesha waroho wachache na mabwana zao huko Ulaya.

Kilichofuatia ni historia ya aibu kwake na bosi wake. Maana baada ya kuona kuwa magari yangechukua muda kukwamuliwa, waandishi wa habari na wanaharakati wa haki za binadamu na mazingira walimpakiza Dikupatile kumpeleka Fikira. Walipofika walimkabidhi Ikulu kabla ya kumpeleka hospitali.

Rais, bahati mbaya hakukatiza ziara yake. Aliporejea alilichukulia jambo hili kisiasa kiasi cha kuungana na Mkuu wa Mkoa kuwasukumizia lawama wapinzani.

Hili halikuwavunja moyo wapinzani wala wananchi wa Githakwa. Waliendelea kuhimizana kutokipigia kura Chama cha Wote.

Baadaye Dikupatile alipelekwa Ulaya kutibiwa na kupoteza lengo kabla ya kupangiwa kazi nyingine.

Ilikuwa ni aibu kwa serikali yote. Ilichukua muda mrefu watu wakisimulia kupatikana kwa Dikupatile na wote wenye matendo na maisha kama yake.

Katika maongezi yao ambayo yalichapishwa kwenye gazeti la Mizengwe, *The Politicos,* Mkuu wa Mkoa alikuwa ameanika uchafu wote. Alikiri kuwa yeye na wenzake walikuwa wamehongwa dola milioni sita. Yaani, waliamua kuwauza watu wao kwa dola milioni sita!

Hali hii iliwaacha wananchi vinywa wazi. Kwani licha ya kuwa kidogo, hakuna ajuaye thamani ya binadamu. Kweli umdhaniaye ndiye siye na si vyote ving'aravyo ni dhahabu.

Maneno ya Matatizo kuwa wanyama walikuwa wakiwazidi binadamu akili yalitimia. Kwani simba hawezi kula nyama ya simba mwenzie wala fisi pamoja na sifa yake ya uroho, hawezi kula nyama ya fisi mwenzie.

Baada ya vyombo vya habari vya ndani na vya nje kuandika kashfa hii wakitegemea Dikupatile angefukuzwa kazi hata kufungwa, dunia ilishangaa Dikupatile alipoachishwa ukuu wa mkoa na kuteuliwa balozi Ulaya tena kwenye nchi ya Sucker!

Ajabu ya maajabu hata nchi za Ulaya ambazo zilikuwa na tabia ya kujifanya walimu wa uwajibikaji, kiasi hata cha kukataa baadhi ya mabalozi, hazikupinga kuteuliwa kwa Dikupatile.

Watu wanasema nchi hizo zisingemkataa wala kumwekea pingamizi kwa vile alikuwa ni kuwadi wao, aliyesaidiana na wenzake kurahisisha unyonyaji na ukaliaji wa nchi changa. Walikuwa wanamkaanga samaki kwa mafuta yake mwenyewe.

Asasi zisizo za serikali (ASIZE) ziliishinikiza serikali iwaadhibu wahalifu hawa bila mafanikio.

Hali hii iliamsha hasira za wananchi ambao ulipofika uchaguzi uliofuatia walikiangusha vibaya chama cha Dikupatile cha *Minzengwe Citizenry Congress* (MCC), ikiwa ni njia yao ya kulipiza kisasi.

Hayawi, hayawi! Wahenge walisema, "Simbuliko halisimbuliki ila kwa mikukuriko na penye nia pana njia. Pia, hakuna lisilowezekana kama mja atajikusuru. Kwani bila ya kutarijiwa MCC ilianguka mwereka wa mende."
Mambo mengi makubwa, ya kuudhi na machafu yalifumka kiasi cha kuwaacha wananchi vinywa wazi!

Pamoja na watu wa Mizengwe kufurahika na kushereheka, hakuna aliyepokea tukio hili la kihistoria kwa shangwe na cherekochereko, nderemo, hoihoi na vifijo kama wanakijiji wa Githakwa, hasa Mzee Njema na wakombozi wenzake. Usiku kucha walikesha wakiimba na kupongezana wakisema, "HAKIKA SAA YA UKOMBOZI IMEFIKA TUKIWA HAI NA HOI."

Siku hii ya kukumbukwa ilikuwa chungu kwa tabaka la watawala wezi na mabarakala wao. Siku hii mzee Kupata hakutoka nje. Alijifungia ndani

akitamani dunia ipasuke immeze, kwani mwisho wa zama zao ulikuwa hatimaye umewadia bila kutarajia. Ama kweli chenye mwanzo shurti kiwe na mwisho na kipaacho hutua. Kwani hakuna aliyetegemea mambo yangebadilika kwa kasi na namna ya ajabu hivi.

Wakati wananchi wakisherehekea, serikali ya zamani ilikuwa ikijiandaa kupambana na ukweli iliokuwa ikiupuuzia. Mawaziri walianza kutafuta njia ya kutorokea. Kadhalika na washirika wao, yaani, magenge ya wafanyabiashara za shaka na wezi na kila aina ya vibaka waliokuwa wakiishi migongoni mwa wananchi wakiwanyonya na kuwadharau wasijue siku za mwizi siku zote ni arubaini. Arubaini yao ilikuwa imetimu na upanga wa umma ukatao bila upendeleo ulikuwa kazini kuwafyeka kupe na fisi wote walioneemeka kwa kuudhoofisha umma.

Baada ya Chama cha Wote kupoteza madaraka na Chama cha Ukombozi kuchukua serikali hakikufanya ajizi. Kiliingia kazini kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidi matunda ya ukombozi na jasho lao. Kiliunda dira mpya ya taifa kikijua wazi kuwa wananchi walikuwa wamerudisha nchi yao mikononi mwao.

Makosa yote yaliyokuwa yamefanywa na utawala uliopita yaliorodheshwa na Mahakama Kuu ikapewa jukumu la kusikiliza kesi hii ya aina yake na kuwaadhibu wahalifu.

Ili kuondokana na historia chafu na yenye machungu mengi kwa wananchi jina la nchi lilibadilishwa. Iliitwa Tazamia badala ya Mizengwe. Maana ya Tazamia ni kuwa na matumaini kwa mambo yajayo kama ambavyo baadaye ilikuja kuwa. Tazamia ilikuwa Tazamia kweli. Kwani, matumaini ya wananchi waliokuwa wamekata tamaa yalirejea na kutekelezwa vilivyo. Mizengwe iligeuka historia na kovu kwao.

Huu umekuwa ni mfano kwa serikali iliyomo madarakani ambao umetoa somo kubwa kwa nchi nzima.

Mzee Njema na wanakijiji wenzake hawakuhama na waliwatimua viongozi wote wa kijiji na kuchagua wengine ambapo Kilimwengu alichaguliwa

mwenyekiti huku Mzee Njema akichaguliwa kuwa mbunge kuchukua nafasi ya Heri Kupata ambaye alikimbilia Ulaya kwa shemeji zake.

Matatizo aliishia kuwa Ofisa Tarafa aliyeleta mafanikio ya ajabu. Alianzisha vikundi vya kujitegemea vya vijana akitumia uzoefu wake wa kudandia meli uliowasaidia vijana waliokuwa na mawazo ya kufanya hivyo.

Serikali mpya iliyoingia madarakani iliwapa Mzee Njema na wanakijiji wa Githakwa na waandishi wa habari na wanaharakati za kutetea haki za binadamu na mazingira Nishani ya Taifa ya Uaminifu, Utumishi Uliotukuka, Ujasiri na Ukombozi yenye hadhi ya juu na thamani kuliko zote katika nchi ya Tazamia.

Vijana waliachana na mawazo ya kudandia meli. Badala yake walijiunga pamoja na kuanzisha miradi ya pamoja ambayo iliboreshea maisha yao.

Rais mpya wa Mizengwe aliyechukua madaraka alifanya ziara kijijini Githakwa kutoa shukurani zake kwa Wanagithakwa kwa kuanzisha mapambano ya ukombozi ulioangusha serikali dhalimu kwa njia ya amani na ya kidemokrasia kupitia sanduku la kura.

Siku hizi Tazamia inapeleka waangalizi wake kwenye uchaguzi katika sehemu/nchi mbalimbali duniani zikiwamo hata za nchi zilizoendelea. Maana tangu kuuzika mfumo mkongwe wa kinyonyaji, Tazamia sasa inakaribia kuingia kwenye ulimwengu wa nchi zilizoendelea kutokana na kutokopa wala kuomba.

Baada ya serikali kushika usukani akina Dikupatile na wale wote waliokuwa wameihujumu Mizengwe walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Baadhi walinyongwa na wengine kukatiwa vifungo vya maisha.

Kuepusha historia chafu ya nchi, Katiba ilibadilishwa na kuhakikisha kila haki ya mwananchi inawekwa kwenye katiba ya nchi.

Mateso alijifungua mtoto wa kiume aliyeitwa UKOMBOZI. Alikuwa amebadilika. Hakuwa tena mtu wa kukata tamaa bali mwenye kutazamia

kama jina la nchi yake mpya maendeleo na furaha ya maisha.
Hakuwa tena Mateso wa kuteseka kwenda kuombaomba mitumba wala kaukanikuvae.
Matatizo, mumewe, licha ya kuwa na kazi alikuwa ameachana na biashara ya kufyeka magogo na kuwekeza kwenye kilimo kiasi cha kujenga nyumba bora na kuwa na maisha ya uhakika.

Kadhalika na mzee Shida alijenga nyumba ya matofali ya kuchoma na si yule wa kulalamikalalamika kama wakati wa Mizengwe. Anatazamia mengi pamoja na uzee wake.

Mzee Kupata na baadhi ya watoto wake walipatikana na hatia mbalimbali za ujambazi, wizi na ubadhirifu na kufungwa vifungo kuanzia miaka 20 hadi 100.

Mali zote za akina Kupata na viongozi zilizokuwa zimepatikana kutokana na kuwaibia wananchi zilirejeshwa kwa serikali, huku pesa nyingi zilizokuwa zimefichwa ughaibuni kurejeshwa.

Siri nyingi zilifichuka. Majumba, akaunti zenye pesa za kigeni, magari hata ndege na mashamba na ardhi viligundulika na kutaifishwa, kwani vilikuwa vimeibiwa kutoka kwa wananchi. Kimsingi, viongozi wengi wa Mizengwe walikuwa ni viongozi wa kuiba na si kuongoza nchi.

Kuna matukio ya kutisha na kufadhaisha yaligunduliwa. Kwani watu walikuwa wameandikisha mali zao kwa majina ya mifugo hata watoto wachanga!

Kwenye kisa kimoja mtoto wa miezi sita alipatikana akiwa ameandikishwa kuwa na mabilioni ya kwenje kiasi cha kuwa mtoto tajiri kuliko hata wale waliokuwa wakiifadhili Mizengwe! Kuna mbwa mmoja naye alikutwa akiwa na utajiri usio wa kawaida!

Rais, mkewe, watoto, jamaa na maofisa wake walikutwa wakiwa na utajiri mkubwa na pesa nje yenye thamani ya kuweza kuiendesha Mizengwe kwa miaka kumi.

Hivyo, mali hiyo ilikamatwa na kurejeshwa kwenye hazina ya taifa na

kutoa huduma za jamii thabiti na za uhakika.
Hiki ndicho chanzo kikuu cha kuwataka watendaji wa umma kutaja na kuzitolea maelezo mali na kipato chao na ndugu zao.

Sheria inawataka kila mmoja kutaja mali zake kabla na baada ya kuwa madarakani.

Uchumi wa Tazamia ulikuwa kwa asilimia kumi na tano na kufanya maisha ya wananchi kuwa bora. Bei za mazao zilipanda huku kilimo kikipewa mkazo. Elimu ilikuja kuwa bure kiasi cha kumlazimisha Matatizo na mkewe na Kili na mkewe kurejea shuleni ili kufaidi matunda waliyokuwa wameporwa na kuyapigania na kuyarejesha.

Pia, mfumo wa utawala ulibadilishwa. Kila mkoa ulipewa mamlaka ya kuendesha shughuli zake na kusimamiwa na serikali kuu.

Nchi ya Tazamia sasa ni nchi ya kupigiwa mfano. Kwani kwa kushirikiana na mataifa ya Amerika ya Kati yakiongozwa na Venezuela iliamua kuachana na siasa za kukopakopa na kubabaisha na kujenga mfumo ulioitwa *usawa* ambao unatishia mfumo wa unyonyaji wa wezi ziitwazo *tajiri* wa utandawizi na utoroshaji na ujambazi uitwao *ubinafsishaji.*

Chanzo cha mgogoro ambacho ni upanuzi wa mradi wa uchimbaji vito nacho kilibadilika.

Wachimbaji wadogowadogo wa Githakwa na wengine kutoka Tazamia walimilikishwa machimbo yale na kupewa mitaji na nyenzo za kisasa na ujuzi.

Utaratibu huu uliwaepusha vijana na hatari ya kukimbilia mijini ambako waliishi kwenye makazi yasiyopimwa huku wakikosa kipato na huduma muhimu na za lazima. Wakati vijana wakihangaika hivi, wakubwa wachache walikuwa wakiishi maisha ghali kwenye maeneo maalumu yaliyokuwa yamepimwa kwa pesa ya walipa kodi.

Sheria hii ilipunguza msongamano wa watu kwenye makazi yasiyopimwa

ambayo yalikuwa viwanda vya kutengeneza magonjwa na jinai mbalimbali, ukiachia mbali umaskini.

Mitaa hii ya mabanda haikuwa na utambulisho muhimu wala kupimwa. Kwa sasa maneno "wazururaji" na "wamachinga" yametoweka. Badala yake kuna lugha ya "wafanyakazi" na "wajenga nchi." Nani atazurura iwapo kuna mipango na juhudi madhubuti, tena ya kudumu na sera za kutengeneza ajira na fursa?
Uhaba wa kazi sasa ni historia.

Hakuna kupokea na, wala kutoa rushwa, ili kupata kazi. Baada ya sheria hii kutungwa na kupitishwa wananchi walichangamkia na kuhamasika kuijenga nchi yao upya, huku kila mmoja akijivunia kufanya hivyo akiwa na uhakika wa kupata ulinzi na huduma kutoka kwenye jamii.

Baada ya miaka mitatu, nchi ilikuwa ikiingiza mabilioni ya kwenje kutokana na uuzaji wa *Tazarald,* jina jipya la *Zengwerald.*

Akina Sucker walinyang'anywa kila kitu na kutupwa jela walikotumikia vifungo vyao na kupewa amri ya kuhama nchi ndani ya saa ishirini na nne. Iligundulika kuwa kumbe kampuni nyingi zilikuwa ni za kitapeli na mfukoni zikishirikiana na watawala wachoyo. Kwani kilichokuwa kikifanyika ni kutuma watoto wao au ndugu zao nje kwenda kusajili kampuni hewa na kuzipa ulaji nchini Mizengwe. Hazikuwa kampuni chochote bali mirija ya kutoroshea pesa iliyoletwa na kutumia na malaya wachache wa kiuchumi waliokuwa wakiuza utu wa ndugu zao.

Ule wizi uliokuwa umegeuka sehemu ya maisha ulibakia kuwa historia. Kwani ilipitishwa sheria kuwa atakayeibia umma anyongwe. Sheria hii isiyobagua ilirejesha heshima na imani ya nchi.

Baada ya katiba kubalidilishwa, Rais hakuwa tena juu ya sheria wala kuwa na mamlaka yasiyo na mipaka, yaliyokuwa yanatumiwa vibaya kuhudumia kundi dogo la marafiki na wapambe wa Rais.

Rais hakuwa tena na mamlaka ya kujiteulia anayemtaka kwa sababu anazozijua. Badala yake uteuzi wowote ulikuwa ukiridhiwa na kupitishwa na Bunge la wananchi. Heshima ya Bunge imerejea na halikuwa likitumiwa tena wala kumwogopa mtu yeyote wala kuathiriwa mamlaka na uamuzi wake na yeyote.

Sambamba na hili, kinga ya viongozi wastaafu ilifutwa ili kuwafanya wawajibike kwa umma wanapokuwa madarakani.

Kwani uzoefu huko nyuma ulionyesha kuwa mtu angejifanyia madudu atakavyo, akijua akistaafu hatachukuliwa hatua za kisheria kwa vile atakuwa na kinga. Hii kinga kumbe ilikuwa chanzo cha ubadhirifu. Hata marupurupu yao yaliwekewa masharti kuwa bila kuwajibika hakuna marupurupu.

Hii ilizalisha viongozi wanaowajibika vilivyo na kustahiki haki baada ya kustaafu badala ya kuwa mzigo kwa walipa kodi kama ilivyokuwa huko nyuma.

Idadi ya viongozi wanaostahili marupurupu ilipunguzwa. Sheria ya sasa inawatambua viongozi wa kuchaguliwa tu yaani Rais na Makamu wake. Hapa kuna sharti. Ili kupata marupurupu na haki yoyote mhusika lazima awe ameacha ofisi bila makosa yoyote yanayohusiana na haki za binadamu au wizi wa pesa ya umma.

Kwa upande mwingine, Katiba mpya haiishii kwa Rais tu. Imeangalia mihimili yote ya dola. Wabunge hawaruhusiwi na sheria kuwatumikia mabwana wawili, yaani, wapiga kura na Rais kama ilivyokuwa mwanzo. Rais haruhusiwi na katiba kuteua wabunge kwa kazi zake.

Hata majaji na wanajeshi hawaruhusiwi tena na katiba kufanya kazi za kisiasa.

Pia, katiba hii imefuta ubunge uliojulikana kama ubunge wa msukule ambapo Rais aliteua watu wake ili kuwatumia anavyotaka pale anapotaka. Inasema wazi kuwa lazima kila mbunge, licha ya kutokana na kura, lazima

awe na jimbo. Sheria hii imeokoa mabilioni ya kwenje.

Aina nyingine ya ubunge ni ile ya ubunge wa makundi. Nao licha ya kuwa wabunge msukule,walikuwa ni mzigo kwa mlipa kodi.

Nao sawa na wale wa kuteuliwa na Rais, iligundulika kuwa walikuwa wakipatikana kwa mizengwe, rushwa na kujuana. Walikuwa wakilijaza bunge huku wakiwa wanawakilisha maslahi yao na wale waliowadhamini kupata ulaji ule.

Badala ya kuwapo nafasi hizi, katiba inatamka waziwazi kuwa yajengwe mazingira ya ushindani ili wabunge wote wapatikane kwa haki na kisheria, yaani, kuwa na majimbo. Hii imeondoa tabia ya kikundi cha watu wachache kufadhiliana na kuajiriana kwa kutumia mgongo wa walipa kodi. Pia, katiba inakataza mbunge wa kuteuliwa kuwa waziri. Maana, huu ni ukiukaji wa mgawanyo wa madaraka wa mihimili mitatu ya dola ambayo inasema wazi kuwa mtu mmoja asitumikie mihimili miwili kwa wakati mmoja.

Wanaomtuma bungeni ni wapiga kura na si Rais. Hata ule utamaduni wa kununulia wabunge magari ya bei mbaya wakati wananchi wakiteseka kwa magonjwa yanayotibika, yasiyolingana na hali ya uchumi wa nchi ulifutwa. Badala yake, sheria ya sasa inatamka waziwazi kuwa wafanyakazi wa umma wawe na zana zinazofanana na mfuko na uwezo wa jamii.

Ile ndoa baina ya serikali na wafanyabiashara na taasisi za kidini ilivunjwa na badala yake serikali ni serikali na asasi zisizo za serikali zinatimiza matakwa yote.

Katiba pia ililiona hili inasema wazi kuwa dola na dini ni vitu visivyopaswa kuchanganywa. Dini zinadhibitiwa vilivyo. Hakuna migongano wala migawanyo ya watu kwa misingi ya dini. Hakuna anayetumia dini yake vibaya kama ilivyokuwa mwanzo, ambapo viongozi wa kidini walishirikiana na wezi serikalini kuwaumiza wananchi.

Serikali sasa ni mali ya wote na si mali ya wajanja wachache kama ilivyokuwa huko nyuma.

Katiba inatamka waziwazi kuwa, kwa mfano, kabla ya mtu kupendekezwa kugombea ubunge, lazima achunguzwe vyanzo vyake vya mapato. Pia Katiba inazuia wadhamini binafsi.

Ule uovu wa wafanyabiashara kutumia mifuko yao kupandikiza na kudhamini watu wao ulitoweka na haki ilirejea. Uongozi ulianza kuzingatia sifa badala ya kipato au uongo na kila aina ya hila. Sharti la kutaka mtu awe na ofisi moja badala ya nyingi, ilivyokuwa kama huko nyuma liliwapangua wezi wote waliokuwa wanakimbilia kwenye siasa kujipatia mlo wao.

Katiba pia inatamka waziwazi kuwa wagombea wa nafasi za umma wawe wa chama tawala au upinzani watagharimiwa na kudhaminiwa na serikali kuu bila ubaguzi wala upendeleo wowote. Hii imeondoa rushwa kwenye siasa. Siasa si chaka la wababaishaji, matapeli na wasasi wa ngawira kama ilivyokuwa mwanzo.

Vyama vya upinzani vilivyokuwa vimedhoofu kutokana na kukosa maelewano kulikosababishwa na kugombea ruzuku iliyotumiwa na serikali kama chambo, vimeshamiri na vinafanya shughuli zake bila kusumbuliwa wala kubaguliwa.

Katiba ya sasa inakwenda mbele na kutamka waziwazi kuwa siasa zilenge kwenye kuwajibika kwa jamii badala ya kulindana na kukomoana. Hapa ndipo dawa ya wizi wa kura ilipatikana. Hakuna kuburuzana tena wala kuoneana kwa kutumia vibaya vyombo vya dola.

Kwa upande wa matumizi ya serikali kuu na za mitaa, kulifanyika mapinduzi makubwa. Hesabu za wizara zote, hata Ikulu zinakaguliwa na kutangazwa. Wizara ambazo zilikuwa zimezoea kuiba na kutumia vibaya pesa ya umma zimetoweka. Hii ni baada ya wahalifu kufunguliwa mashtaka na kufungwa, huku wakifilisiwa bila huruma yoyote. Mapato ya serikali na huduma, licha ya kuridhisha, vinaendana.

Wake wa wakubwa hawajihusishi tena kwenye siasa wala biashara kwa kutumia migongo ya waume zao. Hata zile nafasi za upendeleo bungeni zilifutwa na kujenga mazingira mazuri ya ushindani baina ya makundi

yote ya wananchi. Wanawake hawapendelewi tena bali wanashiriki bega kwa bega kwenye siasa na wanaume kwa usawa.
Pia, katiba iliamuru wizara za serikali, mikoa, wilaya na majimbo ya uchaguzi kupunguzwa ili kutoa fursa za kiuchumi badala ya za kisiasa. Tazamia inakimbia tofauti na ilivyokuwa ikichechemea.

Bunge na Mahakama ni huru na vina nguvu na mamlaka sawa na Serikali. Utawala wa sheria umerejea, huku mgawanyo wa madaraka ukizingatiwa. Serikali mpya haijifanyii mambo kwa usiri na vitisho kama ile ya zamani. Bunge hukagua kila shughuli ya serikali. Hata ile mikataba ya akina Sucker na wezi wenzake ilisitishwa na kufanyika upya kwa kuridhiwa na Bunge. Haikuwa na usiri wala uchochoro wa watu wachache kuwachuuza wengi tena. Kila kitu kilikuwa hadharani kwa yeyote wakati wowote. Madini yaliingiza mabilioni ya kwenje kiasi cha kipato cha wananchi kukua mara kumi ya awali.

Huduma za jamii ziliimarishwa. Barabara, shule, hospitali, maktaba na vituo vya mapumziko na burudani vilijengwa kwa wingi. Viwanja vyote vilikuwa vimeibwa na watawala wa zamani zilirejeshwa kwa umma. Iligundulika kuwa viwanja vingi vya shule, hospitali na wazi vilikuwa vimenyakuliwa na watawala wa zamani.

Vyama vyote vya kisiasa vina haki sawa mbele kwa mali ya umma. Vyombo vya habari na vikundi vya kutetea haki za binadamu vilivyowezesha yote haya kwa kushirikiana na wananchi havikusahaulika. Vinaheshimiwa, kusikilizwa na kupata habari ni haki ya kila raia wa taifa hili lililozaliwa upya.

Rais aliyepoteza madaraka alikufa kwa kihoro baada ya mwaka mmoja akifuatiwa na wenzake wengi waliokuwa hawaamini yaliyotokea. Hii ni baada ya mikasa kumkumba. Kwani mkewe alikufa siku ya kuanguka kwa chama chake huku mwanawe aliyemtegemea akijitandika risasi kutokana na kutoamini kilichotokea. Kwani, kwake Mizengwe ilikuwa nchi ya baba yake na wezi wenzake. Kwa ujumla familia nzima ya Rais wa zamani ilivurugika. Maana watoto wake watatu, mmoja wa kike na wawili wa kiume walikutwa na kashfa nyingi za mauaji na uhujumu uchumi.

Walifungwa vifungo virefu kuanzia miaka 37 hadi 150.

Wakuu wa Mizengwe walikuwa wanatenda makosa mengi hata ambayo hayakuwa na sababu. Kwa mfano, mkuu wa zamani wa polisi licha ya kuiba na kujilimbikizia mali nyingi, alipatikana na hatia ya kumbaka msichana wake wa nyumbani! Wananchi hawakuamini kuwa mtu mwenye cheo kama hiki angetenda kitendo cha ubakaji kama mbwa!

Serikali mpya iliyochukua nafasi ya serikali yake ilimwamuru arudishe mali za umma, kuomba msamaha na kushirikiana nayo kufichua uchafu wote. Naye hakufanya matata wala ubishi zaidi ya kushirikiana kuwafichua wale wote waliomwangusha ingawa yeye alikuwa amewaamini na kuwaamini.

Kuepuka kurudia makosa ya Mizengwe, serikali mpya ya Tazamia ilipitisha sheria ya maofisa wa serikali na ofisi zote za umma kutaja mali zao si tu wakati wa kuingia na kutoka madarakani bali kila wanapotakiwa na wananchi kufanya hivyo wakati wowote.

Miiko ya uongozi ilianza kufundishwa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Utaifa ulirejea kwa kishindo na maendeleo yalionekana kiasi cha Tazamia kuacha kuomba na kukopa. Kwani uchumi wake na jitihada za watu wake viliineemesha ikawa nchi ya kutolewa mfano. Utamaduni wa kuwa na ofisi mbili au mishahara zaidi ya mmoja ulifutwa na ule wa mtumishi wa umma kuwa na mshahara mmoja unaojulikana na mali zake na familia yake vilianzishwa. Wizi kwenye ofisi na taasisi za umma ulitoweka haraka sana.

Ziara na biashara za binafsi za viongozi nje ya nchi vilipunguzwa na kudhibitiwa. Hakuna kiongozi anayeiba wala kujilimbikizia mali. Kila mtu anakula jasho lake halali.

Rushwa ndiyo usiseme. Ilipigwa vita si ya kawaida.
Utaratibu huu uliozuia mfanyakazi wa umma kuwa na kipato zaidi ya kimoja uliokoa mashirika na taasisi nyingi za umma zilizokuwa zimekufa au kukaribia kufa.

Kabla ya utaratibu huu, ilikuwa jambo la kawaida kwa mfano, kumkuta daktari akifanya kazi kwenye hospitali ya umma huku akiwa na hospitali yake binafsi.
Hali ilikuwa mbaya sana na ya kutisha. Ilifikia mahali wagonjwa wakawa wanalazwa sakafuni au watatu au zaidi kwenye kitanda kimoja.

Pia, kulikuwa na tatizo la mgonjwa kuandikiwa akanunue dawa kwenye maduka ya binafsi ambayo mengi yake yalimilkiwa na madaktari walewale waliokuwa wakiwahimiza na kuwaandikia wagonjwa kwenda kununua dawa kwenye hospitali zao.

Lile tishio la mtu kuingia hospitalini na ugonjwa mmoja na kuondoka na mengi lilitoweka.

Kwa Mizengwe kuruhusu uhuria kichaa kama huu ilijikuta matatani. Kwani huu ulikuwa ni upenyo wa ushawishi wa kuiba mali za umma zikiishia kwenye taasisi binafsi.

Halikuwa jambo la ajabu, tena wala kuvunja sheria, kukuta daktari akiiba dawa kutoka kwenye hospitali aliyokuwa akifanyia kazi na kupeleka kwenye zahanati au hospitali yake binafsi.

Jeshi la polisi na taasisi nyingine vilirekebishwa. Hapakuwa na malalamiko ya watu kutishwa,kupigwa au kubambikiziwa kesi tena. Polisi na wanajeshi walianza kuwatumikia watu badala ya kuwatisha. Wananchi wa Tanzania hawawaogopi wala kuwachukia wanajeshi na polisi. Kwani majeshi haya yamedhihirisha kwa vitendo kuwa ya wananchi na si kikundi cha watu wachache waliokuwa wakitumia madaraka vibaya na kiujanjaujanja. Wanajeshi hawateuliwi tena kwenye vyeo vya kisiasa.

Matukio ya ujambazi na unyang'anyi yamebakia kuwa historia chafu iliyozikwa kitambo. Watu wanaweza kulala bila kufunga hata milango. Nani aibe ilhali kila mwananchi anapata kipato chake halali baada ya kujengwa mazingira bora yanayoheshimu haki na wajibu wa mtu?

Kumbe ujambazi ulikuwa ukisababishwa na ubadhirifu na mipango michafu ya watawala wababaishaji na wezi? Maana tangu ukombozi urejee Tazamia, wananchi wote wana vitambulisho na wanatambua umuhimu wa utaifa wao. Hawaruhusu wageni haramu kuja kuwaibia na kuwanyonya kama ilivyokuwa mwanzoni ambapo kila mtu alijifanyia alivyokuwa akiona ilmradi aishi hata kwa kuhatarisha usalama wa nchi yake mwenyewe. Kumbe mjenga na mbomoa nchi ni mwananchi mwenyewe. Kwani, iligundulika kuwa wageni wengi wezi waliokuwa wameivamia Mizengwe walikuwa wakishirikiana na watawala habithi waliowatumia kufanya biashara zao haramu. Waliwaamini sana wageni kwa vile ilikuwa rahisi kuwatimua mambo yalipotibuka.

Maandamano na migomo viliruhusiwa ili kuiamsha serikali inapolala. Isitoshe uongozi wa sasa wa Tazamia haulali wala kungoja kuamshwa kwa maandamano na migomo.

Kila mapato yaliripotiwa serikalini ili kukatwa kodi ya mali na mapato. Rais naye aliamriwa na sheria kulipa kodi sawa na watu wengine na hakuwa juu ya sheria kama ilivyokuwa huko nyuma. Aidha, mali zake na familia zake hutangazwa kila mwaka ili kuondoa wasiwasi kwa jamii.

Hii iliwezesha uwajibikaji wa mtu mmojammoja na jamii kwa ujumla ambapo kila mtu aliwajibika na kupewa haki kutoka kwenye hifadhi ya jamii bila ubaguzi wala upendeleo. Viongozi wanawajibika kwa wananchi na wanaaminiana na wananchi.

Pia, sheria kali ilitungwa kupambana na wezi kwenye ofisi na taasisi za umma. Adhabu kali, kuanzia kifungo cha maisha hadi hata kunyongwa, ilipitishwa kuhakikisha uchafu huu haurudiwi.

Sheria zote za kiwizi na kiimla zilifutwa. Kila mtu ana haki ya kuishi vilivyo na si kama ilivyokuwa awali ambapo alijiishia kutegemea na watawala wachafu walivyotaka. Utawala umetoweka. Umerejea uongozi ambapo hakuna mtu aliye juu ya sheria na sheria haibagui wala haki haiuzwi tena wala kulanguliwa na walafi wachache.

Hii ilitokana na kuundwa Tume Huru ya Upatanishi na Maridhiano. Nchi za jirani zilituma watu wake kujifunza jinsi watu wa Tazamia walivyofanikiwa kujikomboa bila kumwaga damu wala kulipiza visasi.

Hata waliofungwa na kufilisiwa walifanyiwa hivyo kwa mujibu wa sheria na si visasi wala chuki au upendeleo.

Githakwa kwa upande wake ilibadilika kutoka kwenye kijiji cha vumbi na kuwa mji mdogo wenye kila huduma kuanzia umeme, hospitali, barabara za lami, viwanda vidogovidogo, benki na shule za msingi na sekondari na kadhalika. Kwa sasa Githakwa, kwa kutumia mapato yake, inajenga chuo kikuu cha ufundi.

Vijana na Wanagithakwa waliokuwa wamekimbilia mijini walirejea kiasi cha idadi ya watu kuongezeka. Utawala mpya ulijenga mazingira ya kujitegemea kwa kuilima ardhi badala ya kuitambaa na bidhaa dhaifu kutoka ugenini. Vijana hawa wamejikomboa kiasi cha kusahau kuchomwa moto na kuitwa wamachinga na vibaka. Wana mori na jeuri ya kuijenga nchi yao inayojengeka vilivyo kwa vitendo si maneno kama ilivyokuwa awali ilipokuwa Mizengwe. Wana matazamio makubwa ya kusonga mbele kimaisha na kimaendeleo. Wanakula na kusaza huku wakioa na kuolewa. Hivi ni vitu ambavyo hapo nyuma vilikuwa kama ndoto za mchana.

Siasa za majaribio zimetokomezwa milele na kila mtu anawajibika sawa na serikali.

Kilimo kilifufuliwa kiasi cha kurejea kuwa uti wa mgongo wa Githakwa na taifa huku mashamba mengi yakianzishwa, bidhaa kusindikwa kwa ajili ya kuuza nje na msitu wa Kololo ulipewa hadhi ya Hifadhi ya Taifa na miti ilirejea. Hivyo, tishio la mazingira lililokuwa linaikabili Githakwa na Tazamia lilitoweka.

Mto Chania ulirejesha hadhi yake. Si ule uliokuwa ukitishiwa na uchafuzi wa mazingira.

Wanakijiji wa Githakwa wamefanikiwa kuuzika ukuku wa kula usichozalisha na kuzalisha usichokula. Kwani hawategemei tena vyakula vichafu na vilivyokwisha muda wake vilivyoagizwa kutoka nchi nyingine tena zenye ardhi hafifu na kidogo. Wanajilisha kiasi cha kuuza nje. Juzijuzi walitoa msaada kwa nchi jirani iliyokuwa imekumbwa na uhaba wa chakula kutokana na kuwa na utawala mchafu usio na mipango madhubuti.
Kwenye magunia ya nafaka yaliyotolewa msaada kwa nchi hii jirani waliandika, "Nanyi Achaneni na Ukuku. Msimame, mnaweza kujikomboa kama sisi. Saa ya ukombozi ni sasa."

Githakwa na vijiji vingine vya Tazamia havikuwa tena na wakimbizi wakimbiao dhiki zaidi ya idadi ya wakazi wake kuongezeka na kuwa na uhakika wa maisha.

Kweli, hujafa hujaumbika na lolote linawezekana. Kwani penye nia pana njia na hakuna limshindalo mja, kama amedhamiria na kuamua. Hivyo, ukombozi ni suala la uamuzi wa mtu au jamii kwa ujumla. Ni kujiamini na kuchukua hatua mujarabu. Matokeo ni dhahiri kama ilivyojidhihirisha kwa wanakijiji hiki adhimu na muhimu katika historia ya nchi yake.

Githakwa imebakia imesimama kama mama wa mapambano ya ukombozi. Mnara wa kumbukumbu ya mapambano ya ukombozi wa pili ulijengwa. Bado mnara huu wa kumbukumbu ya mapinduzi yasiyo na umwagaji damu umesimama katika viwanja vya shule yalipoanzia mapambano haya ya kufuta uchafu uliokuwa umeota mizizi kwenye nchi. Mnara huo umeandikwa kwa maandishi ya dhahabu yanayosema SAA YA UKOMBOZI NI SASA na hakika saa ya ukombozi ni sasa.

Hii i
Nchi
waliv

Hata
na si

Gith
kuw
za l
kad
kiku

Vij
kia
ya
kut
mc
ncl
aw
kir
Hi

Si
na

K
na
aj
n
n

M
v

Riwaya hii inaudurusu na kuzulu uhuru na dhima nzima ya kuwa huru. Inaona shaka na uhuru wa baadhi ya nchi barani Afrika unaowanufaisha watawala waliojigeuza miungu pwamwe na walamba viatu wao. Watu wa kawaida hawaruhusiwi kutia mkono kwenye deste nao wale halua!

Riwaya inahimiza wengi au umma kushika hatamu. Inashadidisha umma uutathimini na kuuhoji upya uhuru wanaoambiwa ni wao wakati si wao. Katika kufanikisha hili, tofauti na mapambano ya mtutu wa bunduki, mauaji na ghasia, riwaya hii inawahimiza waathirika waishio kwa matumaini kuupigania na kuupata uhuru wa kweli kupitia kwenye sanduku la kura.

Riwaya inahimiza watawaliwa kuhakikisha wanawawajibisha watawala kama sehemu ya uwajibikaji wao. Kila mmoja awajibike kwa mwenzake. Inawataka watawala wawatumikie watawaliwa badala ya kuwatumia kama punda wa kuwabeba wao na mizigo yao.

Riwaya inapinga ufisi, ukuku, umbwa, ukondoo, usindano, ukijiko na tabia nyingine kama hizo; inashajihisha usimba, umizani na utambuzi, utendaji na ulinzi wa haki.

Hapo ndipo utamwona mhusika mkuu, Mzee Njema, akipambana na uongozi mbovu kuanzia kijijini mwake hadi wilaya na, hatimaye, taifa. Cheche ya shujaa inawasha moto unaouamsha na kuukengeua umma kiasi cha kuangusha serikali dhalimu ya Mizengwe kupitia sanduku la kura.

ISBN 978 9987 07 039 8

TANZANIA EDUCATIONAL PUBLISHERS LTD